ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Moja - Tarehe 28 Juni, 2013

(Kikao Kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mgeni Hassan Juma) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 115

Uingizaji Mizigo Zanzibar Kutoka Tanzania Bara Bila Upekuzi

Mhe. Mohammed Haji Khalid - Aliuliza:-

Usafiri wa bahari kuanzia Dar es Salaam, Unguja, Pemba, Tanga na Tanga/Pemba, Unguja/Dar es Salaam uko wazi tena (*free*) na hakuna upekuzi wa kitaalamu wa mizigo ya abiria unaofanyika, jambo ambalo linaweza kusababisha uingizwaji wa madawa haramu ya kulevya pamoja na silaha kwa ajili ya kufanya uhalifu hapa Zanzibar.

(a) Je, kwa miaka hii ya 2010–2013 ni kesi ngapi zimekamatwa za uingizaji wa madawa ya kulevya pamoja na silaha.

(b) Kuna mpango gani wa kudhibiti na kufanya upekuzi wa kina kwa mizigo inayoingia Zanzibar kutoka maeneo hayo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 115 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Mwenyekiti, upo utaratibu wa kawaida wa kitaalamu unaofanyika katika zile bandari rasmi, aidha upo utaratibu maalumu wa doria za mara kwa mara na mbinu nyenginezo za kiaskari zinazofanyika katika maeneo ya bandari zisizo rasmi, hivyo bandari zetu haziko *free* kama alivyosema Mhe. Mwakilishi. Bali zina utaratibu wa ulinzi kama nilivyoeleza. Katika mwaka 2010 – 2013 jumla ya kesi 5 za kupatikana na dawa za kulevya zilikamatwa, kati

ya hizo kesi 1 ni ya kupatikana na bangi, kesi 2 ni dawa aina ya *Heroin*, kesi 1 kupatikana na mirungi na kesi 1 ni ya kupatikana na *Charas*, hakuna silaha zilizokamatwa.

b) Mhe. Mwenyekiti, suala la kudhibiti na kufanya upelelezi wa kina kwa mizigo inayoingia Zanzibar linafanywa kwa mashirikiano baina ya vyombo kadhaa vyenye mamlaka kama Polisi, *TRA*, *ZRB*, bandari, KMKM nakadhalika. Suala hili linafanywa kila siku, lakini hupewa nguvu zaidi pale ambapo kuna taarifa za ki - *intelligency* juu ya tuhuma yoyote. Hivyo hatua mbali mbali zinachukuliwa kudhibiti uingizwaji wa madawa haramu ya kulevya pamoja na silaha haramu na mambo mengine yote yasiyoruhusiwa nchini.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi hii kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa pili wa Rais kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kama suala la msingi lilivyoeleza la Mhe. Mohammed Haji Khalid kwamba usafiri wa Unguja na Pemba, Tanga na Dar-es-Salaam, uko wazi sana yaani katumia *free* hakuna upekuzi wa kitaalamu wa abiria unaofanyika. Swali langu lipo hapa.

Mhe. Mwenyekiti, katika siku za hivi karibuni tumepata taarifa kwamba kuna kampuni moja ya usafirishaji ya abiria baharini wana mpango wa kuanza kuchukua mizigo ya abiria kutoka katika maghala yao wakawasafirishia na kuwapelekea mpaka aidha kwenye maghala yao sehemu nyengine au kwenye maduka yao.

Suala hili Mhe. Mwenyekiti, ni suala ambalo linaweza likaleta athari kubwa sana, kwa sababu kama kuna wahalifu ambao wanasafirisha mizigo yao wakapita nayo bandarini wakapekuliwa, matokeo yake mizigo ile ikabebwa na ile kampuni na inaweza ikasababisha kuwaficha wale wahalifu walioingiza aidha silaha au madawa ya kulevya. Mhe. Mwenyekiti, je, suala hili serikali inalijua na kama inalijua je, imeridhika nalo na kama haijaridhika nalo itachukua hatua gani ya kuhakikisha kwamba kila abiria mwenye mzigo wake apite nao bandarini na atoke nao bandarini aende nao nyumbani kwake, ili chochote kitakachotokezea kiwe kinamuhusu yeye mwenyewe ambaye amesafirisha mzigo huo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba ushauri huu tuupokee, tuende tukaufanyie kazi kwa kina, ni kweli hili zoezi lipo lakini *concern* ya Mhe. Hamza Hassan Juma inafaa kufanyiwa kazi zaidi ili tuujue uhalisia wake na namna ya utaratibu mzima

unaotumika ya mizigo inayoingia mpaka kufika kwa huyo muhusika mwenyewe ima kwenye duka au ghala lake. Kama taratibu haziendi vizuri za upekuzi kuanzia pale bandarini na ukajulikana kila mzigo wa nani na unakwenda wapi kwa mashirikiano na mwenye meli au kwa mashirikiano na wafanyakazi wenye meli, itatubidi tukutane, tulifuatilie jambo hili tujue athari yake kwa undani. Kwa ufupi niseme ushauri huo tunaupokea na kwenda kuufanyia kazi.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, napenda kumuuliza Mhe. Waziri suala moja la nyongeza. Mhe. Waziri katika jibu lake mama alisema ni kesi tano ambazo zimekamatwa. Lakini je, kati ya kesi tano hizo ni kesi ngapi ambazo zimeshafika Mahakamani na kesi ngapi ambazo bado hazijafika Mahakamani. Na kati ya kesi hizo kesi gani ambayo imefika Mahakamani ya madawa ya kulevya au ya kukamatwa na silaha au nyengine. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa sina uhakika ni kesi ngapi zimeweza kufikishwa Mahakamani, kwa hivyo naomba nilichukue swali lake na nimjibu kwa maandishi ili kupata uhalisia. Maana utaratibu huu wa Mahakama una matatizo yake, wakati mwengine polisi wanasema iko Mahakamani kumbe ndio kwanza ipo kwa *DPP*, kwa hiyo ni lazima nipate taarifa vizuri kwa kuwasiliana na *DPP* wao wanihakikishie kwamba kesi gani na gani tayari ipo Mahakamani na kesi gani na gani bado haijenda Mahakamani ama ushahidi wake hautoshi kupelekwa Mahakamani.

Kwa hivyo naomba Mhe. Mwakilishi awe na subra nimjibu kwa maandishi suala hili kwa kulifanyia kazi kwa kina.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hivi sasa kumekuwa kuna unga unasafirishwa kutoka Zanzibar kupelekwa nje ya nchi na kukaguliwa katika mashine na mtu anawekwa katika *departure room*. Je, mashine pale zilizokuwepo hivi sasa macho yake ni makengeza.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba Mhe. Jaku Hashim Ayoub arudie na asemee kwenye spika kwa sababu humu ndani kuna tatizo la *echo*, samahani sana Mhe. Jaku.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa unga unasafirishwa kutoka Zanzibar kwenda nje ya nchi na watuhumiwa wakiwa katika *departure room* katika kuondoka na pale pana mashine zinakagua. Nauliza zile mashine zilizokuwepo pale macho yake yamekuwa ni makengeza.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza sijui unga gani alioukusudia, huu unga wa kawaida wa ngano au unga wa madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri ulikuwa ni unga ambao unaoambatana na suala lenyewe.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli tunalo tatizo kubwa la uingiaji nchini na utokaji nchini wa madawa haya ya kulevya, kitu ambacho kinaharibu sana sana sura ya Zanzibar, heshima yake na hadhi yake. Na sio hivi tu bali jambo hili linaathiri sana vijana wetu ambao ndio hasa msingi wa taifa lolote duniani.

Jambo hili limekuwa gumu sana, ningeomba sana kwamba viongozi, wananchi tukashirikiana kwa pamoja. Maana waletaji, wauzaji na wasafirishaji, hawawezi kukaa mbinguni bali wanakaa na sisi wengine ni majirani zetu, rafiki zetu au ndugu zetu. Ufike wakati wa kila ambaye anahusika na biashara hii haramu tumseme, tumtambue na sote tusimuhurumie.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na swali la Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwamba tutalifanyia uchunguzi kwa kina kama pale bandarini ama Airport kuna mbinu mbali mbali zinazotumika za kusafirisha unga basi hatua zilizomadhubuti zaidi zitaendelea kuchukuliwa kuhakikisha kwamba vitendo hivyo havitokei katika bandari zetu.

Ningependa nitoe wito kwa wafanyakazi wetu, wale wanaofanya kazi katika mamlaka hizi husika kwamba yeyote yule atakayeshirikiana na wahalifu hawa akafanya vitendo ima vya kuingiza unga wa madawa ya kulevya ama kusafirisha madawa haya ya kulevya sio tu tutamfukuza kazi lakini na hatua kali za kisheria zitachukuliwa. Kwa sasa hatutomvumia yeyote wala kumuhurumia yeyote yule anayefanya vitendo hivi ni muuwaji na atashughulikiwa kikamilifu kwa mujibu wa sheria.

Nam 79

Uharibifu wa Barabara Unaofanywa na Kampuni za Ujenzi

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:

Ninaipongeza serikali ya awamu ya sita kwa kujenga barabara ya kiwango cha lami kati ya Machomane na Vitongoji. Kwa kuwa makampuni ya ujenzi

hasa makampuni ya nje ya nchi hupitisha zana zao za magari makubwa na hatimae huzidi uzito barabara hiyo, jambo ambalo tayari limeleta uchakavu mkubwa katika barabara hiyo ambayo awali ilikuwa ikiteleza kama mgongo wa ngisi

1. Je, serikali inalitambua tatizo hilo.

2. Ni lini serikali itazibana kampuni hizi kufanya ukarabati wa barabara hii kabla ya kurudi makwao pale wanapomaliza shughuli zao za ujenzi

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nam 79 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Suala la maharibiko ya barabara zinazopita magari makubwa ya ujenzi, serikali inalitambua tatizo hilo. Kwa mujibu wa mikataba iliyokuwepo hakuna sehemu inalolizungumza suala hili. Lakini Wizara linapotokea tatizo hilo, huwa tunakaa pamoja na wakandarasi ili kuzifanyia matangenezo barabara zinazoharibika.

Kwa mfano hivi sasa tunaendelea na mazungumzo na Kampuni ya *H Young* kuhusu kusaidia kuzifanyia matengenezo barabara ya Kipangani- Madungani kupitia Mzambarau Takao hadi Bahanasa ambayo inaendelea kuathirika vibaya.

Suala la barabara ya Machomane na Vitongoji inatumia takriban kampuni zote zinazofanya kazi za barabara na miradi ya maji. Tunaendelea kuwasiliana na Wizara husika kuhusu kulipatia ufumbuzi suala hili la maharibiko ya barabara.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa mazungumzo ndiyo yanaanza sasa na hatujui kama yatafanikiwa au hayafanikiwi ya kuweza kuifanyia matengenezo ile barabara. Na kwa kuwa makampuni ni mengi na umekiri kwamba makampuni ni mengi yaliyokuwa yanafanya kazi na yanapitisha magari hayo makubwa na kuiharibu barabara ile.

Je, kwa kiasi gani wizara yako itachukua hatua za haraka haraka ili kufanya marekebisho katika barabara ile ambayo ni muhimu sana kwa ajili ya

wanafunzi, wapiganaji wetu wanaokuja jeshini pale pamoja na madaktari wetu wanapotoka hospitali kwenda juu. Ni hatua gani za dharura zitakazochukuliwa ili kuona kwamba hili tatizo hususan katika maeneo hayo ya hapa karibu na Ngerengere ambapo pameshaanza kuharibika sana, mtayafanyia marekebisho kabla hali haijawa mbaya zaidi.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru naomba nimjibu Mhe. Saleh Nassor Juma swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjuulishe Mhe. Mwakilishi kwamba kama ilivyo demokrasia basi na maendeleo vile vile yanagharama zake, tunavyotaka maendeleo vile vile zina gharama zake. Sasa kama tulivyosema kwamba hii barabara ni muhimu, inatumiwa na karibu magari ya aina zote za mzigo kwa sababu ndio kwenye Kware, hata sisi Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu Kware yetu ilikuwa ni Vitongoji. Kwa hivyo umuhimu wa barabara hii tunaujua.

Kutokana hiyo gharama za kwamba maendeleo yana gharama tutahakikisha kwamba sehemu zinazoharibika hatungojei mazungumzo. Tunacho kitengo chetu cha (*UUB*) yaani Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara tunafanya *maintenance* ya kawaida na tunafanya ukarabati wa dharura. Kwa hivyo namuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba suala hilo linashughulikiwa, matokeo yake atawapa karibuni.

Ninahakikisha kwamba *maintenance* hiyo itafanywa na wajenzi wa kufanya *maintenance* hiyo katika kipindi hichi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alivyokuwa akijibu swali la msingi alisema mazungumzo yanaendelea katika Kampuni ya *H-Young* wananchi wa Vitongoji na Machomane wanataka kujua mazungumzo hayo yameanza lini na siku gani yatamalizika.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kaninukuu vibaya, nilisema kwamba njia ya Vitongoji ina watumiaji wengi, kwa hivyo huwezi kufanya mazungumzo na kila mmoja. Njia tuliyoifanyia mazungumzo na *H - Young* ni zile tulizozitaja ambazo wao *special* ndio wanazotumia.

Kuhusu njia ya Machomane, Vitongoji watumizi ni wengi, kwa hivyo huwa tunafanya mazungumzo na Wizara husika pamoja na wale wakandarasi kwa mfano Wizara ya Maji na Nishati, ina wakandarasi wengi wa ujenzi wa matangi na miundo mbinu ya maji hivi sasa na wanatumia magari makubwa

vile vile. Kama nilivyosema kwa barabara hii hata sisi Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano Kware yetu ambayo kuna mtambo wa *crusher* ya kokoto, mtambo wa kupikia lami, uko huko huko Vitongoji. Kwa hivyo barabara hii tunaijua na tunao uwezo wa kufanya *maintenance* bila ya haya mazungumzo.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kunipa fursa nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa barabara zetu za Zanziar zinazojengwa hazihimili kuchukua magari mazito na kwa kuwa makampuni yanayokuja kujengwa barabara yanakuwa na magari mazito ambayo yanakuwa ni zaidi ya tani 10.

Sasa je, namuuliza Mhe. Waziri wa Mawasiliano, wataangalia wanapotiliana mkataba na makampuni ya ujenzi wa barabara ili wanapozitumia barabara zikaharibika kama barabara ya Micheweni na barabara hiyo ya Vitongoji ili kuwalazimisha kama wanapoharibu warejeshe hali iliyokuwa. Ni lini hasa itaangalia suala hilo serikali.

Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa hili ndio pendekezo lake la leo, kwa hivyo mimi nalichukua tutaangalia kama kuna uwezekano huo na kama hizo barabara zetu zimewekewa sheria hiyo ya kutopita magari makubwa. Kwa hivyo ni suala la kwenda kuliangalia kiutaalamu na baadaye tutampa majibu yaliyokuwa sahihi ya kwenye maandishi.

Nam. 9

Mamlaka ya Mji Mkongwe Kushindwa Kusimamia Kazi Zake Ipasavyo kwa Mujibu wa Katiba

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Mamlaka ya Mji Mkongwe inatakiwa ifanye kazi zake kwa mujibu wa Sheria na Kuwatendea watu wote haki sawa kwa mujibu wa matakwa ya Katiba ya Zanzibar ya 1984, kifungu cha 12. Ni hivi karibuni tu Mamlaka hiyo imekuwa ikienda kinyume na misingi ya haki na usawa kwa kuwazuia baadhi ya wananchi wa Mji Mkongwe wasijenge madirisha ya nyumba zao kwa vioo, huku ikiwaachia wengine kufanya hivyo.

Je, Mamlaka hii haioni kuwa kufanya hivyo ni ubaguzi, kinyume na misingi ya Katiba yetu, kwa kuwakataza wananchi wengine kutotia madirisha ya vioo na wengine kuwaachia.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 9 kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, madirisha ya vioo ni neno linalotumika la jumla linaweza kutoa maana halisi, inategemea dirisha gani la vioo. Yapo madirisha ya vioo *frame* zake za mbao ambayo yana usanifu asilia na yanakubalika. Yapo madirisha ya vioo *frame* za *aluminium* usanifu wake hauna uasilia na madirisha haya hayakubaliki ndani ya Mji Mkongwe.

Aidha mamlaka ya Mji Mkongwe ina fanya kazi zake katika misingi ya usawa nilihisi kwamba ilifanyiwa matengenezo kwa mujibu wa Sheria ya Mji Mkongwe, pamoja na mpango mkuu wa uhifadhi. Aidha hatua kali za kisheria huchukuliwa kwa wale wote wanaokwenda kinyume na utaratibu wa uhifadhi zilizowekwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuuliza swali langu la nyongeza Mhe. Waziri ningemuomba kwanza angefanya utaalamu na watendaji wake, hichi ambacho kinachojibiwa ndani ya Baraza. Hichi ni chombo cha wananchi na haya majibu huyu mzee wangu Mhe. Rama ni ya kusikitisha na ya kukatisha tamaa. Pana mifano hai tulikuwa tunaipigia kelele hapa Barazani na hakuna hatua zinazochukuliwa na hata kama tukitoa *hansard* itakuwa ni mtihani mtupu mheshimiwa.

Pamoja na hayo je, Sheria ya Hifadhi ya Mji Mkongwe inasimamia vipi kama wafanyabiashara wakubwa wanajenga majengo kwa hiari yao.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, majengo ya Mji Mkongwe yana mandhari yake maalum unapojenga leo ni kweli hutopeleka kifusi na mawe Mji Mkongwe kujenga utatumia vifaa vile unavyotumia hivi sasa, lakini unapofika kwenye *finishing* lazima jengo lako lilingane na majengo ya Mji Mkongwe yalivyo. Kwa hivyo haya unaowaona wanajenga majengo hivi sasa Mji Mkongwe unasimamia na unatembelea kila siku na anapofika kwenye *finishing* ataona kwamba kama atakwenda kuchukua mambo ambayo hayalingani na Mji Mkongwe basi Mamlaka ya Mji Mkongwe itamwambia hii *finishing* yako hailingani na mandhari ya Mji Mkongwe kabisa.

Mhe. Shadiya Mohammed Suleiman: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza.

Mhe. Waziri hapo Mji Mkongwe kuna majengo mengi huona wameajiriwa Wachina kama Skuli ya Tumekuja, Skuli ya Forodhani na hata Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Je, hili nalo pia ni kufuata maelekezo ya Mji Mkongwe.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli pale Skuli ya Tumekuja pamefanyiwa matengenezo makubwa pamoja na Skuli ya Forodhani, na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imeanza msingi chini na imejengwa jengo zuri la kisasa. Lakini madirisha yake ni ya mbao lakini kwa ndani yameficha vioo. Kwa hivyo unaweza ukaweka *air condition*, kila kitu bila ya tatizo lolote.

Lakini dirisha lile kwa sababu linafunguliwa kwa nje basi likifungwa unaona mandhari ile ya Mji Mkongwe, lakini wanapokuwepo ndani kule kuna vioo na kila kitu. Na hii haikatazwi, mandhari inatakiwa ifanane na Mji Mkongwe.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri pamoja na majibu yake mazuri, naomba kumuuliza swali moja la nyongeza.

a) Mhe. Waziri, naamini ipo sheria ambayo watu wanajenga bila ya kufuata ramani ya Mji Mkongwe, wakajenga vile wanavyotaka wao wenyewe. Je, Mhe. Waziri, sheria hiyo inakwenda na wakati na kama haiendi na wakati kwa nini mheshimiwa usituletee tukaweza kuibadilisha.

b) Mheshimiwa kuna watu wengi ambao sasa hivi wameugeuza Mji Mkongwe kuufanya kama ni mji ambao uko nyuma. Huoni mheshimiwa kutokana na hali kama hiyo tutakosa wafadhili ambao wanatusaidia hivi sasa katika kuleta mema ya Mji Mkongwe.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, Sheria ya Mji Mkongwe ni sheria yetu sisi wenyewe na tumeipitisha katika Baraza hili na halafu tumeipeleka *UNESCO* ili iendane na urithi wa kimataifa na wame-*improve* kwamba sheria ile kama itasimamiwa vizuri basi itaendana na urithi wa kimataifa.

Mji Mkongwe ni vizuri ubakie katika sura ile lakini usiwe na majengo mabovu. Yaani jengo lolote litakalojengwa jipya basi lilingane na sura ya majengo ya Mji Mkongwe na urefu wa kwenda juu ya majengo yake na ndivyo tunavyofanya na ndivyo sheria inavyosimamiwa.

Swali lake la pili ni kwamba wafadhili wanapokuja Mji Mkongwe wanajua wanakuja wapi, wanajua wanakuja mahala ambapo panafuata sheria ya ya urithi wa kimataifa. Kwa hivyo wanapoomba kujenga basi lazima kwanza wakubaliane na Mamlaka ya Mji Mkongwe na ramani zao wazipeleke na zionekane kwamba zitajengwa nyumba kwa mujibu wa matakwa ya Mji Mkongwe ili *heritage* iendelee kubakia. Ndio maana wazungu wanapenda kutembea Mji Mkongwe kwa sababu pamoja na kujenga majengo mapya lakini sura haijabadilika.

Nam. 73

Ujenzi wa Ghala Kuu la Madawa Pemba

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Kwa kuwa madawa yanahitaji mazingira mazuri ya uhifadhi wake sambamba na kuwepo wataalamu wazuri katika fani ya madawa. Na kwa kuwa ghala kuu la madawa lililopo Wete Pemba halikidhi haja kimazingira, kiutendaji pamoja na kiusafiri.

Je, ni lini SMZ itatoa kipaumbele katika sekta ya tiba kwa kujenga au kuboresha ghala kuu la madawa Pemba.

Mhe. Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Saleh Nassor Juma swali lake namba 73 kama ifuatavyo:-

Kujenga maghala ya dawa Unguja na Pemba ni mpango unaotekelezwa na Wizara ya Afya. Mpango huo unatekelezwa kwa awamu ili hatimae dawa zetu ambazo tunazinunua kwa gharama kubwa ziweze kutunzwa vizuri.

Serikali imeshatenga milioni 80 kwa mwaka ujao wa fedha 2013/2014 ikiwa ni mchango wake kwa ajili ya ujenzi wa ghala kuu la dawa Pemba. Ghala hilo litajengwa kwa kushirikiana na wahisani na wizara iko katika mchakato wa kupendekeza eneo la kujengwa na wanasubiriwa wataalamu kwenda kuthibitisha kama litafaa.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa madawa ya Pemba hulazimika kusafirishwa kutoka katika Bohari Unguja na kuja kuhifadhiwa katika bohari la madawa liliopo Wete na hukaa kwa kipindi kirefu. Na kwa kuwa hizi dawa ni *chemical*

zinakuwa *degraded* kwa kutumia njia za kienyeji na zinahitaji *specific range temperature* ili ziweze kuhimili zisije zikaharibika. Na kwa kuwa ghala la Wete sehemu ni ndogo na hawana sehemu ya kuhifadhi hizi dawa ili zisije zikaharibika kutokana na mwangaza wa jua pamoja na *temperature* iliyokuwa si ya kawaida.

Na kwa kuwa shilingi milioni 80 zimetengwa kwa ajili ya ile ghala ambalo hatujui litachukua miaka mingapi ndio limalizike la Pemba. Je, ni hatua gani za dharura atakazochukua Mhe. Waziri ili kuona zile dawa zilizopo na zitakazoletwa haziharibiki.

Pili, kwa sababu wafanyakazi wa lile ghala la Pemba hulazimika kuja kufuata dawa kutoka Unguja kuja Mkoani wakati hawana vipando kutoka pale Wete kuja kufuata dawa kwenye meli pale Mkoani. Je kuna hatua zozote za dharura zitakazochukuliwa kuwapatia usafiri wale vijana pale.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, suala la kwanza la hatua za dharura ni kwamba hivi sasa dawa kwa muda wote zinakwenda Pemba na huwa zinatoka Unguja kwa taratibu za kawaida. Hatua za dharura ni kuharakisha ujenzi wa ghala Pemba na kama mwaka ujao tumeshatenga milioni 80 na tuna ahadi zinazotegemewa kwamba wafadhili watalijenga lile la Pemba. Nadhani hatua za dharura ni kungojea limalizike kwa haraka iwezekanavyo. Hivi sasa utaratibu upo wa kupokelewa dawa Pemba kama ule tulionao na mara nyingi huwa tunatumia usafiri uliokuwepo katika nchi yetu.

Kwa wale vijana ambao wanaokwenda kupokea dawa kule Mkoani, huwa tunatumia gari za Wizara au kama ni lazima huwa tunakodi lakini hatuna hata wakati mmoja dawa zilizotoka Unguja zikachelewa kufika katika ghala la Wete kwa sababu ya utaratibu uliokuwepo.

Lakini la tatu ni kwamba hivi sasa tuna mpango tuliyoibadilisha kwamba badala ya wananchi au mahospitali kungojea dawa tuzipeleke hivi sasa hospitali, huwa wanasema tu wanataka dawa za aina gani mpango huo unaitwa ZINC na unaendelea vizuri na nadhani baada ya mwaka mmoja hospitali zote hasa za vijijini zitakuwa tunazipelekea dawa zinazotaka kuliko dawa tunazowapelekea. Kwa hivyo utaratibu huo ni katika mfumo wa kutaka kubadilisha dawa zisifike haraka vituoni.

Pale inapoonekana dawa zimekawia ni kwa sababu na sisi huwa hatujazipokea kutoka ghala kuu kutoka Dar es Salaam.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Ninakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kunipa fursa nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti

ninamshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri na anajitahidi kutufahamisha ili tufahamu katika majibu yake. Lakini kwa kuwa kakiri kama Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetenga milioni 80 kwa ajili ya kujenga hilo ghala na akasema kama kuna wafadhili ambao watashirikiana nao kwa ajili ya ujenzi.

Sasa ninamuuliza Mhe. Waziri, je ni kiasi gani hasa cha fedha kinatazamiwa kujengea ambacho mpaka ghala hilo kukamilika. Na je hawa wafadhili ni kampuni gani ya wafadhili au ni Shirika gani ambalo limekubali kushirikiana na serikali kujenga ghala hilo.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, suala la gharama kiasi gani itategemea makisio ya ujenzi wa kiwanja na eneo tutakalopata na mahitaji ya dawa Pemba. Siwezi kusema bei halisi hivi sasa kwa sababu ndio kwanza tuko katika taratibu za kujenga. Tutapomaliza kutayarisha kitu kinachoitwa *bill of quantities.* Lakini kwa kukisia tu ghala la Pemba halitokuwa ukubwa wake kama lile tulilojenga Maruhubi, lile la Maruhubi tulijenga kwa bilioni moja na milioni mia mbili. Pengine la Pemba linaweza kuwa chini ya hapo lakini siwezi kusema bei halisi mpaka tumalize taratibu za makisio na ujenzi.

Ni wafadhili gani, ninachochelea kusema ni kwamba mazungumzo hayajaingia kwenye maandishi lakini katika vikao wameshakubali kujenga. Haingekuwa vizuri nikamkandamiza au nikamsisitiza mfadhili hivi sasa halafu akajanambia una maandishi gani niliyokupa. Lakini kuna kila uhakika na alikubali katika vikao vya majadiliano kwamba watajenga kama vile walivyotujengea Pemba. Haingekuwa hivi sasa nikalisema kabda hatujatiliana saini mikataba.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii kwa kumuuliza Mhe. Waziri swali moja na nyongeza. Kwa kuwa uhifadhi wa madawa unaendana sambamba na kufanyakazi katika mazingira hatarishi. Je, Mhe. Waziri wafanyakazi wanaofanyakazi katika ghala la madawa wanapatiwa posho gani la ziada. Lakini kama hawapatiwi je, Mhe. Waziri huoni wafanyakazi hawa ndio wanaohitaji posho maalum.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, jana nadhani lilikuja swali la maposho. Swali la maposho katika mazingira hatarishi hayako kwenye ghala la madawa tu liko kila mahala, kuna wale wanaofanya shughuli za *operation* kule wanachezea damu za kila aina. Kuna wale *orderly* ambao wanakusanya vitu tayari vichafu au vilivyotokana na hatari, tuna aina nyingi za posho hatarishi. Suala hili linashughulikiwa na ninakumbuka Mhe. Waziri wa Nchi, Utawala Bora jana alisema kwa kuwa hatua za karibuni kukamilika kuweza wafanyakazi kupata posho katika mazingira hatarishi, hapo itakapofika wakati

kila anayestahiki katika maeneo hatarishi atapata kile kitachoweza kuwasaidia.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2013/2014 - Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa) Mhe. Mwenyekiti kabla ya yote naomba kwanza nimuombe Mwenyezi Mungu anipe uwezo na pumzi wa kuweza kusoma maoni ya Kamati.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana kwa mara nyengine tena tukiwa wazima wa afya ambayo ni neema kubwa kwetu kwa lengo la kujadili bajeti ya mwaka 2013/2014 kwa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kukushukuru wewe binafsi kuweza kunipatia nafasi hii mbele ya Baraza lako tukufu kuweza kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa juu ya utekelezaji wa bajeti kwa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2013/2014.
Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuwasilisha maoni ya Kamati pia napenda kumshukuru Mhe Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na watendaji wa Ofisi hii kwa utendaji mzuri wa kazi zao ambao unaipelekea Kamati kuweza kutekeleza majukumu ya kazi zake za kila siku kwa ufanisi mzuri. Hata hivyo, napenda kuishukuru Ofisi hii kuweza kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu bajeti yake kwa mwaka 2013/2014 kwa umahiri mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, aidha nitakuwa mwizi wa fadhila nisipowashukuru Wajumbe wa Kamati yangu kwa kazi kubwa walioifanya kwa muda wote na ushirikiano wao pamoja na moyo wa dhati katika kutekeleza majukumu yao katika kufanikisha kazi za Kamati ikiwemo hii ya kuchambua bajeti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, sasa kwa ruksa yako naomba niwatambue wajumbe wa Kamati:-

1.	Mhe Hamza Hassan Juma	Mwenyekiti
2.	Mhe. Saleh Nassor Juma	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Ali Mzee Ali	Mjumbe

4. Mhe. Ashura Sharif Ali Mjumbe
5. Mhe.Shadya Mohammed Suleiman Mjumbe
6. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk Mjumbe
7. Mhe. Subeit Khamis Faki Mjumbe
8. Ndg. Rahma Kombo Mgeni Katibu Kamati
9. Ndg. Makame Salim Ali Katibu Kamati

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo naomba kutoa maoni ya Kamati kwa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa bajeti hii ya mwaka 2013/2014 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti**,** kamati yangu tunaungana na Mhe Waziri kwa kulaani tabia iliyoanza kujitokeza ya vitendo vya uvunjifu wa amani pamoja na uhalifu wa kumwagiwa watu tindikali au (*ACID*) na kuwaharibia maisha yao na hata kuondoa maisha ya watu mbali mbali yaliyotokezea hivi karibuni. Mhe. Mwenyekiti, ni vyema na sisi sote tuliomo humu ndani hatuna budi kulaani vitendo vyote hivyo, kwani sisi sote ni banadamu tunapaswa kulinda usalama wa maisha yetu sote kwani tusione yametokea kwa wenzetu tukayaona madogo lakini inawezekana siku nyingine yakatokezea kwetu, Mwenyezi Mungu atuepushie na hilo lakini ni vyema kama sisi ni viongozi basi wajibu wetu kutoa taaluma kwa wananchi wetu majimboni kwani huo ndio wajibu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana Mhe Waziri kwa utaratibu aliouanzisha wa kutoa *(summery*) ya utekelezaji wa maagizo ya wajumbe wako wa Baraza yaliyotolewa wakati alipowasilisha bajeti yake mwaka uliopita, staili hii itaweza kutusaidia sana kupata ufafanuzi wa mambo yote tuliyoiuliza wizara. Kwa niaba ya wananchi wetu jambo ambalo hata wananchi wetu wataridhika na utaratibu huu na huu ndio utawala bora, nampongeza sana waziri kwa hilo. Kwa hivyo ili kumpunguzia maswali waziri basi tuangalie viambatanisho alivyotuletea kwenye hotuba yake.

Mhe. Mwenyekiti, kama alivyoeleza Mhe Waziri mpango wa bajeti anayotumia *program* (*PBB*) ikiwemo *program* ya kuimarisha ushirikiano kikanda, kimataifa na wa Wazanzibari wanaoishi nchi za nje, (*DIASPORA*). Mhe. Mwenyekiti, eneo hili ni muhimu sana kwani tukiweza kujipanga vizuri basi nchi yetu inaweza kupiga hatua za haraka kwa maendeleo ya nchi yetu, kwani mashirikiano ya kimataifa kwa dunia ya leo ni kuangalia uchumi zaidi hasa kutokana na ongezeka la idadi ya watu hapa kwetu na duniani kote kwa ujumla, na chanagamoto ya ukosefu wa ajira duniani kote na uchumi wa dunia ya ulimwengu wa leo basi eneo hili la ushirikiano wa kikanda na kimataifa ni muhimu sana. Kwa hivyo ushauri wangu tuwatumie sana wenzetu Wazanzibari walioko nchi za nje ili kutusaidia kutuunganisha na

wawekezaji pamoja na wahisani na mashirika mbali mbali ili kusogeza maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, hapa naomba tuungane kwa pamoja kuacha mambo yetu yote na tujikite zaidi katika kuangalia nini tufanye ili kuliondoa taifa letu katika orodha ya nchi maskini na kuiweka katika nchi za wastani wa kati na hatimae kuingia katika nchi zilizoendelea, na uwezo huo upo ikiwa sote tutakuwa kitu kimoja, kwani nchi yetu ni ndogo na hata idadi yetu pia ni ndogo sana. Kwa hivyo namshauri eneo hili tujitahidi sana.

Mhe. Mwenyekiti, pia miongoni mwa *program* hizo ni kuimarisha ulinzi na usalama. Mhe. Mwenyekiti, eneo hili ndio muhimu sana kuliko maeneo yote kwani nchi yoyote duniani hata iwe tajiri vipi lakini kama hakuna amani na utulivu, basi hata maendeleo yake hayawezi kupatikana, kwani tumeshuhudia hivi sasa miongoni mwa nchi zilizokuwa na utajiri mkubwa na amani na utulivu, lakini leo miji yao imekuwa magofu na wananchi wao wamekuwa wahanga wakubwa wa maafa, wengi wao wamepata ulemavu wa kudumu, vifo vya kila siku, uharibifu wa mali zao, wameingia kwenye umaskini wa maisha, na hata mitaji na biashara zao nyingi zimefilisika kabisa kutokana na vita na vurugu za kila siku kila kukicha mabomu, mizinga na kadhalika. Kwa mfano kama Libya, Misri, Syria, Iraq, na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, na sisi tumuombe Mwenyezi Mungu asije kutupeleka huko, kwa hivyo katika *program* hiyo kamati yangu inaomba kufanyike utafiti huo na kuangalia vishawishi vyote vinavyoashiria dalili za uvunjifu wa amani na kutomuonea haya mtu yeyote ambaye atakayeonekana kama ni chanzo cha vurugu za aina yoyote na kumchukulia hatua za kisheria kwa haraka sana. Kutokana na kuwa nchi yetu ndani ya miaka miwili ijayo inategemea kupita katika mkondo mkubwa wa wimbi la mabadiliko makubwa ya mfumo wa utawala na sheria za nchi zetu. Kwa hivyo, hiki ni kipindi kifupi cha mpito lakini kiutawala ni kipindi kikubwa cha maisha na uhai wa taifa letu na maisha ya watu wetu. Kwa hivyo, ni vyema kwa sasa na iko haja ya kuongeza bajeti ya vikosi vyetu vya ulinzi na usalama, kuongeza ulinzi katika mipaka yetu, anga yetu, bahari yetu na hata mitaani kwetu na namuomba Mhe Waziri, akija aje atueleze je serikali imejiandaa vipi na kukabiliana na kipindi hiki cha mpito na kuna bajeti yoyote ya akiba iliyoandaliwa kwa ajili ya kuihami nchi yetu kwa lolote litakalojitokeza ili kuwahakikishia usalama wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kama alivyoeleza Mhe Waziri mwakani tunategemea kusherehekea sherehe za kutimiza miaka 50 ya mapinduzi ya Zanzibar, ambapo vimeandaliwa vipindi kwenye redio na TV kuelimisha wananchi mafanikio ya mapinduzi. Lakini pia naomba ushauri wa kamati pia kuandaa makongamano ya vijana, akinamama, wazee pamoja na wasomi ili kutoa

maoni yao na kutuelezea nini tufanye ili kuweza kuendeleza na kuboresha malengo ya mapinduzi. Lakini vile vile tunaomba maandalizi hayo yawe mapema na pia kuangalia hali ya uwanja wetu wa Amani au uwanja mwengine wowote utakaotumika katika kusherehekea sherehe hizo, kwani tuna wasi wasi wananchi wengi watahitaji kushiriki wao wenyewe ili kuona nini kinachoenedelea, ushauri wangu pamoja na kamati yangu ni vyema kutafuta mapema ma-*SCREEN* makubwa, *BILL BOARD* na kuyaweka kwenye viwanja vya mpira mbali mbali unguja na Pemba mijini na vijijini ili kuweza kushuhudia moja kwa moja kile kitakachokuwa kikiendelea hapo uwanjani. Sasa sijui hili kama serikali wameliangalia au vipi.

Mhe. Mwenyekiti, pia Mhe Waziri katika kutekeleza *program* zake mbali mbali ambazo amezipanga ambazo ni nyingi nitawaachia wajumbe kuzichambua lakini kubwa ninalotaka kumkumbusha Waziri kuwa kuharakisha sheria ya Serikali za Mitaa ili kuzijengea uwezo Halmashauri, pamoja na Mabaraza ya Miji ili ziweze kujitegemea na kuweza kujipangia malengo na kujisimamia wenyewe, kwani hivi sasa sheria inawabana na kushindwa hata kuingia mikataba moja kwa moja na taasisi za nyengine, kitu ambacho kinawarejesha nyuma katika shughuli zao za maendeleo. Lakini pia kamati yangu inaikumbusha serikali kuwasomesha na kuwajengea uwezo watendaji wa Halmashauri na Mabaraza ya Miji kwani mageuzi ya Serikali za Mitaa yanahitaji wataalamu wa kubuni miradi, mipango miji, wanasheria kwa ajili ya kusimamia mikataba ya kisheria, wachumi na wengineo ili kuziwezesha kukabiliana na changamoto za mabadiliko hayo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile Kamati yangu inapenda kusisitiza Halmashauri zote kuweza kusimamia mapato na kubuni vianzio vipya ili kuweza kupata mapato yatakayowawezesha kuendesha Halmashauri zao na kuweza kusaidia ujenzi wa barabara za ndani na pia kuboresha mitaro ya maji machafu. Hata hivyo, kutokana na hali ya uchafu unaoongezeka kila siku katika maeneo ya miji na vijijini Kamati inashauri kuandaa utaratibu wa kuweka maeneo maalum ya taka lakini pia kuandaa mipango ya kuzoa taka hizo na kupeleka kwenye klabu za kutupia taka. Lakini pia Kamati inapenda kushauri Halmashauri ya Wilaya ya Chake-Chake na Baraza la Mji Mkoani kuangalia upya vianzio vyao vya mapato kwani vipo chini sana. Vile vile Baraza la Mji Chake-Chake kwa kushirikiana na Idara ya Ardhi na Mipango Miji, Kamati inashauri kutafuta eneo la kuegeshea magari ili kuondoa tatizo la msongamano la magari katika soko la Chake-Chake.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Baraza la Manispaa Kamati inasisitiza kukamilisha mpango wa kujenga *shopping mall* hapo Darajani ili kuweza kuondoa tatizo la msongamano la wafanyabiashara wadogo wadogo katika maeneo ya Darajani na Mchangani.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe Waziri tunaipongeza Serikali kwa kuweza kutafuta eneo huko Kibele kwa ajili ya kutupa taka kwani hivi sasa katika mji wetu wa Zanzibar, taka imekuwa ni tatizo kubwa sana na ndio maana hata watendaji wa *Municipal* hupata usumbufu kwa wananchi, zinapokwenda kujengwa silabi za taka wanakuwa wagumu kwani hakuna uhakika wa kuzolewa kwa taka hizo. Kwa hivyo, tunamtaka Waziri ajitahidi kukamilisha zoezi la upatikanaji eneo hilo ili hizo taka ziweze kwenda kuhifadhiwa, lakini vile vile si vyema kuweka silabi za taka kwenye maeneo ya skuli kwani huwakosesha raha na utulivu watoto wetu wanaosoma kwenye skuli hizo, lakini hasa wakati wa mvua husababisha nzi wengi na harufu mbaya kwa walimu na wanafunzi wanaosoma katika maeneo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, pia kuhusu mradi wa *ZUSP* tunamtaka Waziri kujitahidi kuharakisha utekelezaji wa mradi huo kwani umepitishwa siku nyingi na gharama za vifaa kila siku zinaongezeka na zaidi katika ujenzi wa mitaro ya kupitishia maji machafu hasa ujenzi wa mtaro Kwamtipura, Shaurimoyo na Saateni ambao katika kitabu chake amesahau kuutaja, sijui kwa makosa au ndio ameshautoa kwenye mpango, naomba jawabu kwa hilo kwani mtaro huo unaathiri maisha ya wananchi waishio pembezoni mwa unapopita mtaro huo hasa wakati wa mvua kubwa na zile za masika, hivyo iko haja ya kuharakisha hatua za ujenzi huo, kwani mimi ninavyojua mtaro ulikuwemo tangu hatua za mwanzo za mradi huu.

Mhe. Mwenyekiti, pia tunaitaka Serikali kuyaboresha makaazi ya Wakuu wa Mikoa na Wilaya ili kuweza kuishi katika mazingira yanayolingana na hadhi yao. Sambamba na uboreshaji wa sehemu zao za kufanyia kazi ikiwemo ofisi na vitendea kazi katika ofisi hizo. Tunaishukuru Serikali kwa kuwapatia usafiri Wakuu wa Mikoa na Wilaya wote. Tunaomba magari hayo yafanyiwe *service* kwa muda muafaka kwani magari mengi ya Serikali huharibika mapema kutokana na kutofanyiwa *service* kwa wakati.

Mhe. Mwenyekiti, pia tunapongeza Serikali kwa kuboresha uwekaji taa za barabarani pia tunaomba mpango huu uende sambamba na taa za kuongozea magari lakini pia kuwa na mpango wa kuweka *CCTV CAMERA* ili kuzuia na kuweza kupata taarifa hasa za uvunjifu wa amani na vitendo vya uvunjifu wa sheria katika nchi yetu wakati umefika hasa kwa dunia ya leo kuweka *CCTV CAMERA*, husaidia sana katika kuwatambua na kuwakamata wahalifu kupitia kamera hizo. Kwani tumeshuhudia hata hivi karibuni kule Buston Marekani ambapo kulitokea milipuko kwenye mbio za *marathon* ambapo watuhumiwa walipatikanwa kupitia kwa msaada mkubwa wa *CCTV CAMERA*, kwa hivyo ni jambo jema na la busara kuweka kamera hizo ili kulinda usalama wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inapongeza jitihada zinazochukuliwa na Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kwa kuweka mikakati ya kuziboresha huduma zao kwani zinaimarika kila siku tunaona jitihada za Kamishna na tumefurahi sana kusikia kuwa tayari wameshapatiwa eneo katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Zanzibar, ili kuimarisha huduma za Zimamoto katika uwanja wetu wa ndege ambao tunategemea kuongezeka kwa huduma zake hivi karibuni tu mara baada ya kukamilika kwake.

Lakini pia tunapongeza jitihada hizo kwa kutiliana saini upatikanaji wa magari manne ya kuzimia moto pamoja na vifaa vyengine ambavyo yataweza kusaidia sana kuokoa mali na maisha ya wananchi wetu pale moto utakapotokea. Lakini pia mkazo uwekwe katika kuwapatia eneo muafaka na kuwajengea jengo la Zimamoto katika kiwanja cha ndege cha Pemba kwani yale makaazi yao hayaridhishi hata kidogo, kwani wanapata taabu sana hasa wakati wa mvua zinaponesha. Lakini pia kamati yangu kwa kushirikiana Shirika la Bandari tunaomba kupatikana mahala maalum kikosi hicho pale bandarini kwani pale walipo hapakidhi mahitaji hasa kwa shughuli zao za kila siku. Kwa hivyo hili naomba wahusika wakae na uongozi wa shirika la bandari ili kuweza kulitafutia ufumbuzi wa kudumu suala hilo.

Mhe. Mwenyekiti**,** kamati yangu inashukuru pamoja na kazi kubwa inayofanywa na Idara ya Faragha na kukabiliwa na ufinyu wa bajeti, lakini iko haja ya kuboresha Ikulu ya Mkokotoni alau kwa kuanzia na ukuta au *fence* ili kuiweka katika hali ya ulinzi pamoja na usalama wa eneo hilo kamati inapongeza jitihada zilizofanywa na Idara hii kwa kuweza kufanya ukarabati mkubwa wa Ikulu ya Mkoani Pemba ambapo ilikuwa imechakaa sana.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe Waziri ameelezea ziara za Mhe Rais wa Zanzibar nje na ndani na kwa zile za nje ametueleza kuwa ameomba makampuni ya China kuja kuekeza hapa Zanzibar, suala je tayari tunayo *master plan* ya hayo maeneo ya uwekezaji hapa Zanzibar? na je tayari tumekwishaweka miundo mbinu katika maeneo ya uwekezaji au wakija tena kama kawaida yetu tuwapeleke kwa wananchi wakalipe fidia na kusumbuliwa kama wawekezaji wengine tunavyowafanyia? Jambo ambalo natahadharisha ni kuwa wenzetu Wachina sio watu wa masihara kwani wanalosema ndilo wanafanya hufanya na hawawezi danadana kama hiyo, maeneo hayo tujiandae vya kutosha kwani sera ya China hivi sasa ni kuimarisha masoko ya kimataifa na makampuni ya China kuekeza nje ya nchi yao na kwa hilo wako tayari sana kwani leo dunia nzima kuanzia Asia, Amerika na hata Ulaya kuna makampuni mengi tu ya China yanaendelea kuekeza huko, kwa hivyo na sisi isijekuwa tunaandaa kuwaita lakini kumbe hatujawa tayari kuwapokea.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kamati yangu jambo ambalo linatusikitisha kuwa katika ziara ya Mhe Rais amekuwa akitoa maagizo mengi lakini hatua za utekelezaji haziridhishi wakati huambatana na jopo la viongozi wa Serikali, miongoni mwa maagizo hayo ni lile suala la viongozi wa Mikoa na Wilaya kuyamaliza matatizo ya migogoro ya ardí, jambo ambalo limekuwa donda ndugu hadi leo kamati yangu inaendelea kupokea malalamiko ya migogoro ya ardhi ambayo hayaishi. Sasa naomba Waziri kuwasimamia viongozi wa mikoa na wilaya kuyamaliza matatizo hayo, kwani kuna baadhi ya maeneo wananchi hunyang'anywa maeneo hayo na hawapati msaada wowote, kwa hiyo naomba Waziri kulivalia njuga suala hilo.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Baraza la Mapinduzi limeendaa kufanya kazi zake vizuri lakini kamati yangu inawataka kuharakisha upatikanaji wa hati miliki ya majengo yote ya Ikulu hapa Zanzibar, kwani hilo ni jambo la lazima hasa kwa wakati huu, tunawapongeza kwa kukamilisha upatikanaji wa hati ya Ikulu ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti**,** Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari waishio nchi za nje, Idara hii ina kazi kubwa ya kuwatafuta na kuwatambua na kuwaunganisha mawasiliano yao moja kwa moja na Serikali, lakini kamati yangu bado inasisitiza kufanywa kwa jitihada kubwa za kuwatafuta kwani tunajua kuwa Wazanzibari wako wengi sana nchi za nje na kuna wataalamu wengi ambao wana ujuzi na utaalamu mkubwa lakini bado hadi leo Idara haijaweza kuwatafuta. Wazanzibari hawa wanazitumikia nchi za watu na kutumia utaalamu wao huko nje. Kwa hivyo kamati yangu inaitaka Serikali kuiwezesha Idara hii kufanya ziara za makusudi hasa katika nchi za Canada, Marekani , Oman, Uingereza na nchi ambazo kuna Wazanzibari wengi na kwenda kukaa nao na kuzungumza nao na kuwasikiliza nini ushauri wao na kuja kufanyia kazi, kwani hawa huleta pesa nyingi kwa ndugu na jamaa zao lakini katika njia zisizokuwa rasmi kitu ambacho kinaikosesha Serikali mapato ambayo yangeliweza kuchangia hata pato la taifa letu. Hapa Serikali iweke mikakati maalum kwani kamati haikuridhika na uingizwaji wa fedha katika Idara hii kwani hadi Machi ni 41% ya fedha tulizoidhinisha ndizo zilizopatikana kwa hali hii hatutegemei kama lile lengo lililokusudiwa kama litafikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, Waziri ametuelezea ushiriki wa Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa katika mikutano mbali mbali ikiwemo *Indian Ocean Rim*, labda waziri angelikuja kutuelezea ni fursa gani zilizopo katika jumuia hii ya (*IOR*) na Zanzibar tumezitumia vipi. Pia kamati yangu inashauri kuwa Idara itafute jengo au ofisi ambayo itakuwa nje ya jengo la Ikulu kwani mazingira ya hawa *Diaspora* hasa wale wanaokuja kutembelea Zanzibar inakuwa ni vigumu kwao kwenda Ikulu kwani mazingira ya Ikulu ni mazingira maalum na sio

kila mtu anapaswa kuingia kule hasa kama shughuli zake hazihusiani na Ikulu.

Mhe. Mwenyekiti, Kitengo cha Usalama wa Serikali (*GSO*) tunawapongeza kwa kazi kubwa wanazozifanya, na tunaziomba taasisi zote za serikali wanapokuwa na shughuli zao hasa za ajira na mafunzo ya maadili ya kazi basi kukitumia kitengo hiki, lakini kamati yangu bado haijaridhika na uingizwaji wa fedha hauridhishwi kwani kazi zao ni kubwa na nyeti lakini kuna uhaba wa fedha na pia kutokana na kazi zao nyingi hufanya nje ya ofisi yao wakati mwingine hata hutumia usafiri wao wenyewe bila ya kufidiwa mafuta wanayotumia kutokana na uhaba wa usafiri katika ofisi yao na hii hupelekea kufanya kazi zao katika mazingira magumu.

Mhe. Mwenyekiti, Afisi ya Usajili na Kadi za Vitambulisho vya Uzanzibari, kamati yangu inaipongeza kwa kazi kubwa na ngumu wanayoifanya kwa Wazanzibari, kamati yangu inasikitishwa na kitendo cha Wizara cha kuwanyima posho nyeti kwa muda mrefu ambalo walistahili kupatiwa jambo ambalo tumelishauri kila tunapokutana na Wizara na Waziri amekuwa akituahidi kuwa atawapatia, lakini hadi leo posho yao hiyo hawajapatiwa. Kwa hiyo tunamuomba Waziri kuhakikisha suala hilo linapatiwa ufumbuzi wa kudumu kwani hiyo ni haki yao na wala sio sadaka. Kwani tukiweza kuwalipa vizuri watendaji wetu ndio watakapoongeza bidii ya kufanya kazi. Kamati yangu inapongeza mpango maalum wa kuwapatia vitambulisho wageni wanaoishi Zanzibar. Hili ni jambo jema ambalo litasaidia kuweka usalama wa wananchi yetu. Pia kamati yangu inawapongeza Idara kwa kuendelea kutoa vitambulisho vyenye kiwango cha kimataifa ambacho kinatambulika duniani kote.

Mhe. Mwenyekiti**,** Idara ya Serikali za Mitaa kamati yangu inaitaka kuharakisha mchakato wa kurekebisha sheria ya vileo kwani hivi sasa kumekuwa na malalamiko mengi kwa mabaa yalioko mitaani jambo ambalo kutokana na mila na desturi yetu Wazanzibari kwanza pombe ni haramu. Kwa hivyo kuruhusu kuweka mabaa kwenye maeneo ya makaazi ya watu hupelekea vitendo vya aibu na fedheha vinavyofanywa na watu wakishalewa lakini pia wakati mwengine matusi na vurugu zinavyotokea baada ya watu kulewa inawasumbua sana wananchi wanaoishi katika maeneo hayo. Kwa hiyo, tunaitaka Idara kuharakisha mchakato wa marekebisho hayo ili kuweza kuiokoa jamii kuepuka usumbufu wanaoupata kwenye mitaa yao.

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa wa Mjini/Magharibi, kamati yangu inashauri kamati ya ulinzi na usalama kuimarisha ulinzi katika Mkoa huu kwani mkoa huu ndio chimbuko la kila kitu mazuri yapo mkoa huu, mabaya pia yako mkoa huu, kwa hivyo ni vyema kuwa na ulinzi imara pamoja na kuwa Waziri

ameturipotia kuwa vitendo vya uhalifu vimepungua lakini tusibweteke, kwani katika siku za hivi karibuni kumeanza kujitokeza vitendo vya uvunjifu wa amani, pamoja na mauaji, pia kamati yangu inautaka mkoa huu , kuhakikisha agizo la Mhe. Rais la kuondoa wanyama wote wanaohatarisha usalama wa barabarani kwa mifugo hiyo kuzurura barabarani jambo ambalo linaweza kusababisha ajali wakati wowote, tunaomba zoezi hili liwe endelevu na isiwe la muda tu.

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa wa Kaskazini Unguja kamati yangu unawashauri kuzidisha ulinzi kwani majahazi hupakia na kuingiza abiria kupitia bandari bubu ambazo hazijatambuliwa kisheria na Serikali, lakini pia katika eneo la Nungwi kunahitajika kufanyika kwa tathmini maalum kuhusu wageni walioko kule na kuwatambua wote na kuwapatia vitambulisho maalum vya Mkoa ili wale wageni wote watambulike na Mkoa ili jambo lolote litakalotokezea basi iwe ni rahisi kuweza kudhibiti, lakini pia kuwashirikisha katika kulinda usalama wa eneo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa wa Kusini Unguja, tunawapongeza Mkoa huu kwa kazi wanazozifanya kuwatumikia wananchi wetu, kamati yangu inaiagiza Ofisi ya Mkuu wa Mkoa pamoja na Wilaya zake kuhakikisha wanazitambua nyumba zote za wananchi zilizokodishwa wageni kutoka nje na kuziripoti Idara ya Uhamiaji pamoja na *ZRB*, kwani wageni hawa hukodishwa nyumba hizo lakini Serikali haifaidiki na kodi yoyote kutoka kwao jambo ambalo ni kinyume na Sheria. Lakini pia ni hatari kwa nchi yetu kwani hatuwezi kujua wageni hao wanajishughulisha na nini na wanakutana na watu wa aina gani, na pia wana mikakati gani kwani hakuna nchi inayokubali kuwaachia wageni wakiishi ndani ya nchi na kukwepa taratibu za nchi husika.

Mhe. Mwenyekiti**,** Mkoa wa Kusini Pemba, tunawapongeza kwa kazi nzuri wanazofanya kuwahudumia wananchi wetu, pia tunawapongeza kwa kuweza kukamilisha upatikanaji wa kiwanja cha kujenga nyumba ya Mkuu wa Mkoa. Kwa hivyo kamati yangu inaitaka wizara kuhakikisha wanaanzisha ujenzi wa makaazi hayo kwa haraka ili kuweza kuwapatia makaazi yanayolingana na hadhi ya Ofisi hiyo.

IDARA YA URATIBU YA IDARA MAALUM:

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu pia inawapongeza Tume ya Utumishi na Idara ya Maalum kwa kuweza kukamilisha *Scheme of Service* kwa askari wetu wa vikosi vya SMZ kwani kwa muda mrefu askari wetu wamekuwa wakipata mshahara mdogo pamoja na stahiki zao nyengine mbali mbali. Kamati yangu inaamini kukamilika kwa *Scheme* hii sasa alau na wao wanaweza kutononoka kimapato na kuweza kufanya kazi zao kwa ufanisi

mkubwa. Kwa hivyo, kwa kuwa Waziri ametueleza kuwa hivi sasa wameshaipeleka Serikalini, Wizara ya Utumishi wa Umma jambo ambalo linahitaji marekebisho. Kwa hivyo tunaitaka Serikali kupitia Wizara ya Utumishi wa Umma wakamilishe mapitio hayo ili marekebisho hayo yaingie kwenye bajeti hii tunayoipitisha. Hivyo tunamtaka Waziri wa Utumishi wa Umma atupatie ufafanuzi katika hili kabla ya kusomwa bajet yake.

KMKM:

Mhe. Mwenyekiti**,** kamati yangu inawapongeza makamanda wote kwa kazi kubwa ya kutulindia mipaka yetu hasa huko baharini, pia pongezi kwa kuweza kutafuta vifaa kwa ajili ya kazi ya uokozi ikiwemo kuwapatia mafunzo askari wetu wa *KMKM* pia na huduma wanayoitoa kwa hospitali yao iliyopo Kibweni, hili ni jambo la faraja. Kamati yangu inaomba kutengwa fungu maalum ili kuweza kuwapatia posho maalum askari wetu wazamiaji pale inapotokea kazi maalum ya kuzamia baharini na kuokoa maisha ya watu na mali zao kwani tumeona ugumu wa kazi yao lakini inakuwa hakuna hata huduma ya chakula au maji kuwapatia askari wetu mpaka kusubiri Idara ya Maafa.

JKU:

Mhe. Mwenyekiti**,** tunawapongeza makamanda wote wa kikosi hiki kwa kazi kubwa ya kuwalea vijana wetu kuwapatia mafunzo ya ukakamavu kabla ya kuanza ajira, pia tunawataka kuendeleza mashirikiano walioanzisha baina yao na JKT ya Tanzania Bara kwani wameweza kuchota ujuzi mwingi kutoka kwa wenzao, ushauri wetu yale mazuri wanayoyakuta kwa wenzao JKT basi waje kuanzisha hapa kwetu Zanzibar. Kwa mfano JKT wameanzisha kampuni ya JKT ambayo hufanya miradi mbali mbali ikwemo kuanzisha kampuni ya ulinzi na kuchukua *tender* ya kulinda kwenye mahoteli na makampuni mbali mbali ya watu binafsi kitu ambacho kinawasaidia kutoa ajira binafsi nje ya jeshi. Kwa hivyo, hapa kwetu itaweza kusaidia kutoa ulinzi kwenye mahoteli yetu ya kitalii na kuliondoa tatizo la uvamizi wa mara kwa mara unaofanywa kwenye mahoteli ya kitalii.

KIKOSI CHA ZIMAMOTO:

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inawapongeza makamanda wote wa kikosi hiki kwa kazi kubwa wanayofanya kuokoa mali na maisha ya watu pale yanayotokea majanga mbali mbali ya moto na ajali nyingine kwa kuuwa. Mwanzoni nilieleza kuridhika na hatua waliofikia kwa kuweza kupatikana eneo la kuweka kituo chao hapo uwanja wa ndege wa Zanzibar, sina haja ya kurudia tena lakini naomba sana Kamishna wa kikosi hiki kuendelea

kushirikiana na taasisi nyingine ikiwemo Halmashauri na Mabaraza ya Miji hasa katika kusimamia taratibu za ujenzi wa nyumba za makaazi, kwani watu huachiwa kujenga na kuweka. Aidha njia nyembamba au kuziba kabisa jambo ambalo wakati ukitokea moto inakuwa ni vigumu kuweza kufika kwa wakati kama malengo yao walivyojiwekea ndani ya dakika 15. Kwa hivyo kamati yangu inawapongeza pia kikosi kuwajengea uwezo askari wetu wa kikosi hiki.

KIKOSI CHA VALANTIA (KVZ)

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inawapongeza makamanda wote kwa kazi kubwa wanayoifanya kwa kulinda taifa letu ikiwemo mali zetu, kamati yangu bado inashauri kikosi hiki kuweza kuharakisha upatikanaji wa hati miliki ya maeneo yao Unguja na Pemba na pia kuweza kuboresha makaazi ya askari wetu. Vile vile kuhakikisha mgao wa fedha kwa upande wa Pemba unafanywa kwa wakati lakini pia kuhakikisha madeni mengi ya muda mrefu kule Pemba yanalipwa ili kuweka heshima na taaswira nzuri kwa makamanda hasa kule Pemba lakini pia mkazo uwekwe kwa kuimarishwa kwa makaazi ya makamanda na wapiganaji katika kikosi hiki.

CHUO CHA MAFUNZO:

Mhe. Mwenyekiti**,** kamati yangu inapongeza kikosi hiki kwanza kwa kuwa wabunifu wa miradi lakini pia wasikivu kwa yale maelekezo tunayopeana wakati wa ziara za kamati, kwani kila siku zinavyoenda wanajitahidi kuboresha makaazi wa wanafunzi (wafungwa) ikiwemo kuwajengea vyoo, lakini pia kuwatenganisha wanafunzi watoto, mbali ya watu wazima, pia kuimarika kwa huduma za kisheria wanazowapatia wanafunzi ili kuwasaidia katika kukata rufaa na kuwapatia wanafunzi vyombo vya kupata habari ikiwemo *TV* na *Radio*, ambapo mambo hayo yote hapo mwanzo yalikuwa hayapatikani, pamoja na hayo wamejaribu pia kuongeza milo kutoka miwili hadi mitatu kwa siku jambo ambalo huleta faraja na kutofautisha kuwafanya wanafunzi kuhisi wako Chuo cha Mafunzo na sio jela kama vile zamani.

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa maboresho hayo hatuna budi kutoa shukrani zangu za dhati kwa makamanda kwa kazi kubwa wanayoifanya kuboresha makaazi ya wanafunzi, pamoja na hayo kamati yangu ilishauri kikosi hiki kujenga uzio katika Chuo cha Mafunzo Kinu Moshi na Langoni ili kuviweka vyuo vile katika hali ya usalama zaidi na kuwapunguzia kazi askari wetu, lakini pia kuwapatia posho la kazi ngumu wale askari wanaokwenda kuwalinda wanafunzi hasa wanapokuwa maporini kwani wakati wowote wanaweza kutorokwa, kwani askari wetu wanakuwa wakiwalinda wanafunzi karibu kutwa nzima ikiwa jua au mvua, lakini pia kamati yangu imeishauri kikosi

hiki kulijenga lango kuu la Chuo cha Mafunzo cha Ubago na kukipandisha hadhi kuwa ni Gereza la Mkoa ili kupunguza msongamano wa wanafunzi katika Chuo cha Mafunzo hapo mjini lakini pia kupunguza gharama za kuwasafirisha wanafunzi kutoka Mkoa wa Kusini. Kamati yangu pia inakitaka kikosi hiki kuzifanyia ukarabati mkubwa nyumba za askari zilizoko Kangani kwani askari huvujiwa wakati wa mvua wakati wanafunzi wao hawavujiwi jambo ambalo huwafanya askari wetu kujihisi kama na wao wako Chuo cha Mafunzo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia naomba sana ndani ya bajet hii Serikali ihakikishe inaongeza maslahi ya askari wetu kwani wao ndio walinzi wetu, huwezi kuwa na walinzi ambao huwajali kwenye maslahi yao.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache naomba wajumbe wenzangu tuichangie, tuiboreshe na baadae tuipitishe bajeti hii ili waende wakayatekeleze hayo yote tuliyowaagiza.

Ahsante sana, naomba kuwasilisha.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi asubuhi ya leo hii kuweza kuchangia hotuba hii na hasa leo ni siku ya Ijumaa na sisi wengine tuna ukoo wa Kisharifu na katika kuchangia hii ya leo *assakheri* pengine mambo yatakuwa mazuri mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikupongeze wewe kwanza kwa ujasiri wako, nimpongeze sana Mwenyekiti wangu ambaye ni mwanamama aliyetoa taarifa kwa ufanisi kabisa, kwa umahiri kabisa, nimpe hongera sana, kumbe akinamama mkitaka mnaweza, nashukuru sana, hasa namuona Waziri yupo anapiga kofi kwa uangalifu kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kuwa kuna jambo ambalo muliweke mbele kwenye ukurasa wa 39, halafu nitakwenda kwa utaratibu ninaoutaka mimi mwenyewe. Katika ukurasa huu Mhe. Waziri ameeleza jinsi ambavyo anavyoshirikiana na polisi jamii kwenye Shehia. Mhe. Waziri niseme ukweli na msema ukweli siku zote anakuwa mpenzi wa Mwenyezi Mungu, msema kweli siku zote anakuwa anachukiwa na binadamu, mambo haya mawili yapo. Mimi bora niende kwa Mwenyezi Mungu anipende kwa kusema ukweli kuliko binadamu potolea mbali na anichukie binadamu, anifanye kila analosema potolea mbali.

Mhe. Mwenyekiti, hili neno la nadharia hasa unaposema polisi jamii kwenye Serikali yetu bado hatujalipa kipaumbele. Hili nasema sana tu na hapa ndipo nitakapomnyang'anya mshahara Mhe. Waziri, sasa wenye kujua watasema *dah* Waziri atatumia nini leo kumnyang'anya mshahara, hapa nataka

nimnyanganye mshahara kama sikupata maneno matamu sana ya polisi jamii mimi mshahara wako mimi nauchukua. Sasa kama Wizara itaendelea kufanya kazi sijui.

Mhe. Mwenyekiti, dhana hii imetoka kwa wenzetu wa Polisi ikiongozwa kwa upande wa Zanzibar, Kamishna mwenyewe, upande wa kule *IGP* mwenyewe kwa nia nzuri tu na vijana wetu wamejishajihisha kwa wingi sana, tumeshawatumia kipindi kirefu sana, wanafanya kazi ngumu hawana mawasiliano, hawana chochote lakini wamekubali tu na tunaona jinsi gani matukio yaliyokuwa makubwa wanayatatua, lakini hatujawasaidia. Mhe. Mwenyekiti, nimeona sentensi ndogo inasema Kwaalinatu polisi jamii wa hapa niseme kuwa ni nambari *one,* ambayo imeshikamana imejitahidi kufanya kazi ngumu sana katika jimbo lile hakuna mtu asiyejua, lakini Mhe. Waziri nikwambie Sheha wako wa Kwaalinatu anawabughudhi hawa polisi jamii, tena anawabughudhi kabisa na ndio maana nikasema nakunyang'anya mshahara kupitia Sheha wako, Sheha huyu sie polisi jamii hapa jamii ielewe, anawabughudhi sana.

Mhe. Mwenyekiti, vijana wanatafuta eneo la kutaka kujenga kituo cha polisi jamii, sio sehemu ya kupigia ngoma, *disco* au rusha roho, mnawabughudhi hamuwapi nafasi anawahangaisha anawapiga mpira huku anawatoa huku, yeye haoni kama anasaidiwa kazi. Wana wa Kwaalinatu wamenituma na hasa hawa polisi jamii wanasema Sheha huyo hatumtaki kwa kupitia kiongozi wao ndio mimi. Mhe. Mwenyekiti, tuwe *serious* katika kuijenga polisi jamii, tuwe *very serious* tusifanye mzaha mzaha, hizi sheria haya mambo tunayotunga halafu tunafanya mzaha mzaha yatatu-*cost* kweli, kwa sababu wale ni watu wanaojitolea wakasaidia jamii, na kweli zamani Kwahani ulikuwa hupiti hivi hivi upuuzi upuuzi unaringa na kidani chako, lakini leo angalau inafika hatua nyumba ya kwanza ya tatu ya nne hujanyang'anywa kwa kupitia hawa vijana. Mhe. Waziri, kauli yako nataka uje uniambie kuwa Mshimba vijana wakajenge.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije kwenye sehemu ya vitambulisho. Namshukuru sana Mkurugenzi na mimi siku zote nakwambia panapo uzuri nitasema na panapo ubaya nitasema. Nimshkuru sana huyu Mkurugenzi wa Vitambulisho na mimi mwenyewe nilikuwa shuhuda nilisema sana hapa Barazani kuwa Mkurugenzi huyu afanye ziara, kuna mambo humu awapige msasa hawa Masheha wetu, mtu ambaye anastahiki kwa mujibu wa sheria apewe kitambulisho, sasa mutuambie hivi nataka nikuchekesheni, Sheha huyu wa Kwaalinatu mtu awe anakaa ubavuni anasema hamtambui, huzimii, anamkatalia anasema mimi sikujui na saa zote anamuona pale akizaliwa, lakini namshukuru Mkurugenzi amewaelimisha vipi taratibu za utekelezaji, ndivyo inavyotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo ambayo mimi sikuyaona humu wale wenzetu wa vitambulisho wanatumia sana mionzi, sijaona mimi sehemu ya kuwapa hiyo *risk allowance* kama macho, mimi sikuvaa miwani basi utanisaidia, hatujawatendea haki si kitu cha mchezo tusiwaone tukawatumia kwa masuala mengine tu lakini na hili tuwapongeze *anytime* wanaweza wakapata *cancer*, matitabu yenyewe ndio hayo hapa kwetu Zanzibar, tuna rufaa lakini baadhi ya dawa nyengine hatuna. Sasa tu-*solve* mapema na kuwapeleka India hatuwezi hatuna uwezo huo.

Mhe. Mwenyekiti, ninamuomba sana Mkurugenzi wangu wa Vitambulisho aendele na jitihada hiyo hiyo azunguke Zanzibar, nasikia ameanza Pemba, ameingia sasa hivi mjini humu, anaanza mashamba basi namuomba sana na sasa hivi vitambulisho vinachukuliwa, baadhi ya asilimia imepunguka sasa hivi baada ya kuingia yeye mwenyewe, hatuoni ujasiri wake huyu jamani, anahimiza mtu haki yake njooni mchukue kwa mujibu wa utaratibu moja mbili tatu basi na sheria zipo. Mimi nakaa Fuoni lakini nilipoondoka Fuoni na nilipohama nimemtaarifu Sheha wangu nakwenda kuhamia mji mwengine kuna kasoro gani.

Mhe. Mwenyekiti, niende sasa kwenye vikosi hivi. Kwanza nataka nimshukuru sana Mhe. Marehemu Abeid Amani Karume aliyaona haya. Leo Mhe. Waziri ana vikosi vyake *special* hakuna nchi dunia ya leo Zanzibar ndio tunaona haya maajabu. Hili sikubaliani mimi mwambieni Mhe. Rais, Rais wa Zanzibar Dkt. Shein si mtu tabu, lakini tunashindwa kumwambia kama hamuwezi basi tuiteni sisi twende, kwani kuna tabu gani mimi ni Rais wangu yule, nimempigia kura, kama hamuwezi kumwambia tupelekeni sisi. Ni jambo la kushangaza sana kuona Zanzibar hatuna Waziri wa Vikosi ni aibu. Vikosi vinakwenda kujitia kwenye jamii, tunalishusha hadhi jeshi letu, polisi tunamtia kwenye mitaa ndio maana yake eti.

Mhe. Waziri naomba sana hakuna sababu ya kuwa na Waziri kabisa, hawa wakiwa na Waziri wao haya mambo yote yanafutika, wakaondokana watu kuchangishwa fedha kiholela kwa sababu watakuwa na *special uniform* kwenye bajeti kama tunavyokupitishia leo mabilioni ya fedha hapa basi naamini na wao wangekuwa leo wao Waziri yuko hapa tunampigia hoja jinsi gani anavyoliendesha hili jeshi letu la hapa Zanzibar, vikosi maalum maana sheria imemkataza lakini tunata vikosi maalum, hii hatuendi kabisa kwa mujibu wa sheria ya Katiba yetu na sasa hivi katika hiyo rasimu ndio kabisa imeshatuelekeza tunangoja nini Mhe. Waziri, uangalie hilo, leo mpaka Polisi itakuwa unayo wewe, polisi kweli ukamtie halmashauri. Hivyo naomba sana Mhe. Waziri, kwa hili nitaondoa shilingi kabisa uje kuniambia maneno mazuri ushampigia simu Dkt. Shein nshamwambia kuwa kishakubali nakurejeshea shilingi yako. Mhe. Waziri, naomba sana hilo suala kuwa vikosi

vyetu tunawavunjia heshima hata cheo, leo Meja anapata shilingi laki nne ni sawa sawa na *staff surgent* wa jeshi, na wanafanya kazi katika mazingira magumu sana kusema la ukweli, wallahi hamko *serious* kweli kwa kuendesha hivi vikosi, hatari hii, hawa watu sio wa kuchezea chezea kabisa. Mhe. Waziri naomba mishahara atakuja kuniambia leo Waziri wa Utumishi na kama mshahara kidogo haiwezekani nitaondoa hata mshahara wangu mimi nitaupeleka kwa hao, lazima tuhakikishe mshahara wao umepanda mara hii. Mhe. Mwenyekiti, maisha magumu, wanapata watu mishahara mtu anapata laki moja na tisini kweli mtu huyu tunamkadiria anafanya kazi gani, wanafanya kazi mazingira mpaka usiku, hawana *allowance* kulipwa hawalipwi, wenzetu polisi wanalipwa wao hawalipwi wakati na wao ni jeshi wanalinda, tunawapeleka wapi.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kuna fungu la chakula na vinywaji Mhe. Waziri nataka uje unieleze kifungu hichi mimi nazuia, kifungu cha kasma 220201 nataka uje unieleze uje unipitishe fungu lako. Jengine lolote sikusikii kitu lakini viburudishaji kama chakula na maji unaambiwa *three hundred*, naomba sana Mhe. Waziri nakujua wewe utanipa maelezo mazuri ili niridhike na suala hili ili nikuachie kifungu chako. Naomba sana fungu hili Mhe. Waziri aje kunipa maelezo mazuri ili niweze kumkubalia tumpishie na *three hundred millions and three millions.*

Mhe. Mwenyekiti, lakini tunakwenda kwenye vikosi kwa mfano, kwenye vikosi vyetu kuna mambo ambayo siridhiki nayo na kwa sababu siridhiki nayo kwenye bajeti tunakuwa tunawatilia zile fedha, vyenginevyo waziri aje anipe maelezo yaliyokuwa matamu. Wanachangisha pesa za michezo mimi sikubaliani nalo hilo na kama wananisikia wenyewe nasema wasitoe. Kwa sababu kuna fungu ambalo tumeshawapitishia humu kwenye bajeti. Kwa mfano, KMKM wana shilingi 30 milioni halafu leo tunawatoza pesa. Hivi karibu tu Mhe. Waziri yaumu shaka sina uhakika zaidi, nimeambiwa tayari askari wanafanyiwa mchango upya wa shilingi elfu saba, elfu kumi na elfu kumi na tano kwa muda wa miezi sita, sikubaliani nalo Mhe. Waziri hilo, pesa zenyewe hawana maskini ya Mungu kile kikia cha mbuzi mnataka mkikate?

Mhe. Mwenyekiti, *sports* ni kitu cha hiari, nimejaribu kutafuta sheria za uaskari hakuna kitu kinachozungumza mtu *sports* ni lazima, wala hakioneshi hasa kifungu hicho ndio wanatupeleka wapi. Nimesharanda mote sijaona kitu hicho, hiki ni kitu cha hiari lakini vile vile wanasema wapo wanaokatwa shilingi elfu moja, elfu mbili mpaka elfu tatu, zinakwenda wapi zile leo, wameshachoka hawa jamani. Wanakuja askari wengi maafisa wana kila kitu, nasema washachoka mshahara wenyewe hawana tuwahurumieni, tusiwakate kipuuzi puuzi.

Mhe. Mwenyekiti, ukija kwenye Kikosi cha Zimamoto wenyewe wanakwambia tunakula buku, tunakula buku wakati huku kuna fedha za chakula si kidogo, shilingi milioni mia moja za chakula askari anapewa shilingi elfu moja. Mhe. Wairi kama bajeti ndogo tunakuomba sana Wizara ya Fedha wakuongezee bajeti usitenge bajeti iliyokuwa ndogo kutokana na askari wako, kumlisha kwa siku shilingi elfu moja haimtoshi hiyo. Tunaomba sana Mhe. Mwenyekiti, kama wanaona bajeti hii ndogo kifungu hiki kasma ya 211204 Huduma ya Chakula, hii naomba sana Zimamoto hiyo, naomba fedha hizi kama kidogo aje tumuombee lakini askari sasa asipewe buku, basi atafika kweli, angalau aseme shilingi 11,000 na 15,000 tunakwenda kumpa buku shilingi elfu moja kwa Kiswahili chengine.

Lakini pia kuna mambo ya vifaa vya michezo, kuna shilingi 32 milioni. Mhe. Waziri msikivu sana, mwaka fulani tumesema askari wanachangishwa shilingi elfu moja moja, alihamaki sana mara moja akakatisha akasema kuwa hakuna, na hii nayo nataka iondoke. Nimeshafanya *research* nimekwenda Polisi hawatozwi pesa hizo, nimekwenda wapi hawatozwi pesa hizo sisi tu, isijekuwa mradi maalum huu wa baadhi ya watu, kama wenyewe watanuna na wanune potelea mbali mimi natetea wananchi nimekamata msahafu, nimekula kiapo hapa, na hiki leo nakihitimisha msahafu hautoniadhibu kabisa kwa sababu naifanya kazi ipasavyo ili kuwatetea wanyonge.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inasema suala la halmashauri. Halmashauri zetu nafikiri zinafanya kazi kwa uadilifu, lakini kuna mambo sheria zinawapinga kwa kukosa mapato. Tunaomba sana Mhe. Waziri zisaidiwe halmashauri zetu kwa kutengenezewa sheria za yale mambo ambayo kuna asilimia fulani na wao wanazitaka tunaona maendeleo yao kusema ukweli. Kwa sababu wao wakipata fedha wanawasaidia madiwani wetu katika kuleta maendeleo kwenye majimbo yetu, sasa kuna mambo ambayo tunaziona pesa zao zinafanya kazi Mhe. Mwenyekiti, tunaziona kabisa kazi zinavyofanyika.

Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, niseme kuwa haya matamko ya Mhe. Rais mpaka sasa hivi Mkuu wa Mkoa wangu wa Kaskazini kuanzia ma-*DC* wa Wilaya za Kaskazini 'A' na 'B' nataka Mhe. Mkuu wa Mkoa hili tatizo la ardhi baadhi yao tumeshirikishwa wenyewe Wawakilishi tunaona kwamba yanakwenda vizuri. Sasa kilichobakia waziri husika kuweza kutekeleza kile baada ya malalamiko ambayo yamepelekwa kwa Mkuu wa Mkoa. Hili nalo naliomba Mhe. Mwenyekiti, hili suala tuliendeshe kwa ukweli kwa sababu tayari wakuu hawa wamefanya kazi ipasavyo. Rais amesema wilaya wanatekeleza kwa kupitia kupeleka mkoa, mkoa unamalizia kupeleka kwa wahusika. Sasa naomba sana kuwa wale wengine ambao bado hawajakuwa na utaratibu kama huo, kama Mkoa wa Kaskazini waje kule Kaskazini waone zile shughuli ambazo zishachukuliwa na kusaidia jamii, tena ni jambo

linakwenda haraka haraka, nina kesi kama tatu mimi nazijua, Mheshimiwa wangu amefanya kazi amezipeleka.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu yeye hana sheria ya kuanza wala kumalizia, tunasema Rais angesema tunakupeni sheria Wakuu wa Mikoa malizeni yote hayo sisi tuje kuwapa hati, basi nafikiri Mkoa wa Kaskazini ungekuwa nambari moja, yangekuwa yashamaliza kabisa hiyo kazi ambayo inatakiwa ifanywe.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka kumalizia na sasa hivi nakwenda ukingoni suala la ajira ya vijana. Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na ratiba iliyopangwa na serikali kutangaza na ndio utaratibu ambao tumeukubali huo. Lakini ninachoomba Mhe. Mwenyekiti, waziri sasa asikae kwenye kiti tu, aende kwenye vikosi akaangalie ule utaratibu tuliousema tunaufuata? hilo ndio suala lenyewe, lakini namshukuru sana mheshimiwa mhusika wa Tume ya Utumishi ametangaza nafasi hizo na watu wanafikiria *process* kama zinafanywa hazifanywi, wanajua wenyewe waziri atakuja kusema hapa, kama kweli utaratibu tumeshaufanya tumefikia kadhaa wa kadhaa. Namuomba sana Mhe. Waziri usimkubalie kwenye meza tu, kuna matatizo huko. Kwa hivyo, Mhe. Waziri naomba sana suala hili lifuatiliwe kwa uangalifu ili tuone hali halisi ilivyo na kazi zinavyofanywa na hao watendaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, nisisahau la mwisho suala la hawa Wazamiaji wa KMKM. Mheshimiwa hawa ni nuru yetu Zanzibar, naweza kusema nuru yetu ya Zanzibar kuwa kila majanga yanayotokezea wao wanakuwa ni nambari *one*. Lakini kuna maposho hawa fedha zao zinakuwaje sijui, ngojea nione kwa ghafla ghafla kuna *risk allowance* hiyo ya askari fidia shilingi milioni kumi? Mhe. Mwenyekiti, shilingi milioni kumi hujapigwa kwa pesa hizo; kwa kweli fungu hili la 272104 linasikitisha sana, haikidhi haja fidia hii hasa kwa wale wazamiaji kwenda mbele sana. Hata sifikirii kama wanapata ile.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu pesa za likizo. Pesa hizo wanapiga kelele hawapati KMKM wana shilingi 80 milioni kama sijakosea, lakini hawapati pesa zao za likizo wanapata watu wachache tu, shilingi 85 milioni Kasma 111104 wapeni pesa zao haki yao ya likizo. Tunawanyima nini ile ni haki yao basi hata kule kutoa hamtoi pesa za likizo. Mshahara mshawanyima basi hata za likizo hamuwapi. Naomba sana Mhe. Waziri ili nisifu na kwenye mshahara nakaribia Dokta wangu udokta upate ukinipa maneno mazuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, hayo ndio mambo ambayo nimeyaona kwa binafsi yangu na wananchi wangu wa Jimbo la Kitope, nawatetea haki yao kwa kupitia misingi ya wizara hii kubwa kwa Mheshimiwa mwenyewe Makamo Mwenyekiti wa Chama chetu cha Mapinduzi (CCM) na hii ni moja katika

kusimamia sera ya Chama cha Mapinduzi katika kupitia ilani ya utekelezaji. Sasa mimi kazi yangu kwa upande mwengine naisimamia ilani kwa utekelezaji wake, lakini akija Mhe. Waziri kwa mujibu Katiba mimi sheria inanipa matumizi kusimamia bajeti ambayo nimeipitisha hapa na kusimamia maendeleo yake yakoje. Sasa wale wanaojitia hawafahamu mimi ndio nawafahamisha wasikasirike hiyo ndio kazi yangu ninayoifanya. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kabla ya yote nichukue nafasi hii kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku hii ya leo kufika katika Baraza lako tukufu kwa hali ya uzima na afya njema.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukupongeza wewe binafsi jinsi unavyotuendesha na jinsi unavyokuwa makini ambapo ni mwanamke unatuonesha mfano kwa kuliendesha Baraza lako hili tukufu na Mwenyezi Mungu akusaidie.

Pia Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii nimpongeze Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jinsi anavyotekeleza majukumu yake ipasavyo, tena Mwenyezi Mungu kampa kipaji na amzidishie kwa utaratibu ambao anautumia namna gani ya kutekelza shughuli zake. Lakini sio havyo tu, hata kwa umakini na ustahamilivu ili kuonesha kwamba bado anawapenda wananchi wake katika kisiwa hiki cha Zanzibar.

Lakini nitakuwa mwizi wa fadhila Mhe. Mwenyekiti, kama sikumpongeza waziri ambaye amesoma hotuba yake hii kwa makini, nimpongeze yeye pamoja na watendaji wake wote ambao walimsaidia kwa namna moja au nyengine kwa kuweza kutuletea hotuba mwanana ambayo imetoa mwelekeo mzuri. Mimi hasa nimpongeze kwa vitabu vyake hivi ambavyo ametuletea kuonesha namna gani na amejirekebisha namna gani ya utendaji wake wa kazi.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, niingie katika dondoo za kuchangia. Kwanza nichukue tena nafasi hii Mhe. Mwenyekiti, nimefurahishwa sana katika kitabu hiki ambacho kimeandika stahili mbali mbali za wafanyakazi. Kwa kweli nichukue nafasi hii nimpongeze kwa dhati kabisa Mhe. Waziri kwamba sasa anaonesha mwenendo wake wa kutenda kazi zake kwa ufanisi na vizuri zaidi. Lakini niondoke hapa Mhe. Mwenyekiti, nije katika suala zima ambalo huwa sisi Wajumbe wako wa Baraza hili tunalipigia kelele kuhusu hati miliki.

Hati miliki Mhe. Mwenyekiti, ni kitu ambacho kinakupa wewe mwelekeo wa kuwa hiki ni changu na hiki sio changu ni cha mwengine. Lakini Mhe. Waziri

nakuomba sana kwamba katika majengo haya ya Ikulu ambayo umeshaanza kutafuta hati miliki namuomba sana suala hili alifuatilie ili tuhakikishe kwamba tunajua Ikulu pamoja na nyumba za serikali zimepata hatimiliki. Nimuombe waziri husika kwa sababu tatizo linajitokeza kwamba vitu vyetu vingi, majengo mengi ya serikali kuwa hayana hati miliki na kila kamati inapokwenda kukagua mambo yake basi utaona kwamba nyumba nyingi zimechukuliwa, maeneo mengi yamechukuliwa na maeneo mengine yanamegwa kidogo kidogo yote haya ni kutokana na na kutokuwa na hatimiliki. Sasa hapo unajitokeza unyonge baina ya wananchi na serikali yake. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kwamba hati miliki ni muhimu na nitamuomba atakapokuja hapa atueleze Ikulu zetu ngapi zimepata hati miliki, nyumba alizozitaja humu ni ngapi zimepata hati miliki na zile zilizokuwa hazijapata hati miliki basi azifuatilie kwa kina.

Lakini nikiwa hapo hapo nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa jinsi ya kuzisimamia Ikulu ambazo kwa kweli hasa Ikulu ya Mkoani. Ikulu ya Mkoani ni Ikulu yetu wenyewe. Kwa hivyo, nimpongeze sana kuona kwamba kuna haja nyumba ile ya Ikulu kufanyiwa ukarabati wa hali ya juu, lakini pia kutiwa uzio wa mawe, kwa sababu miti mingi imeshaanza kuporomoka na mvua yetu ya Pemba tunaielewa, kwa hivyo nimpongeze sana na namuomba hili alisimamie yeye mwenyewe kikamilifu ili tuhakikishe kwamba ile Ikulu tunaiokoa na hatari iliyonayo sasa hivi.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa kusomesha wafanyakazi, ameeleza mambo mazuri mengine sana humu, kwamba anachukua hatua mbali mbali kwa kuwasomesha wafanyakazi wa aina mbali mbali. Kwa hivyo, na mimi nichukue nafasi hii nimpongeze.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nije katika Baraza la Manispaa. Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hi nimpongeze sana Mhe. Rais kwa kumteuwa Mkurugenzi mwengine ambaye ataweza kufanya kazi zake katika ufanisi. Nimuombe Mkurugenzi wa Manispaa na nimuombee kwa Mwenyezi Mungu amjaalie kila la kheri ahakikishe anafanya kazi zake ipasavyo, ahakikishe anafanya kazi zake bila ya upendeleo, ahakikishe anafanya kazi zake ambazo za kuuweka mji wa Zanzibar uwe mji wa mfano. Lakini pia nimuombe Mhe. Waziri amsaidie sana Mkurugenzi huyu kwa sababu ni mtu ambaye hivi kidogo tu ameainisha kwamba kweli Manispaa itakuwa katika hali nzuri. Kwa hivyo, niwaombe wale wote ambao wako chini yake Madiwani na wale wa Ofisi ya Manispaa wamsaidie Mkurugenzi huyu ili tuepukane na mambo ya hapa na pale.

Nikiingia hapo hapo Mhe. Mwenyekiti, nimuombe tena Mhe. Waziri bado kuna haja ya kupitia tena masoko yetu yote. Niwapongeze kwanza kwa Soko

la Mwanakwerekwe jinsi walivyolipanga vizuri, nje sasa *Alhamdulillah*, tunaona magari yanaegeshwa vizuri lakini bado nije kwenye Soko la Mboga Mboga. Nimuombe sana Mhe. Waziri pamoja na Mkurugenzi wa Manispaa waende wakaangalie na wao wapate kujengewa vizuri ili wafanya kazi zao kwa ufanisi.

Saateni bado sijaridhika mimi na soko lile, kwa kweli Saateni bado hebu tubadilike tunasafiri kwenda katika nchi mbali mbali tunaona wenzetu jinsi wanavyojenga masoko yao. Nadhani sasa umefika wakati wa kubadilika na ninavyomjua Mhe. Waziri atafanya kazi hiyo ipasavyo. Lakini pia hata Soko Kuu ambalo lile ndio kioo kwa Zanzibar, lakini bado nalo lifanyiwe ukarabati mwengine wa hali ya juu ili kuonesha mandhari nzuri ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niseme kwamba nimuombe Mhe. Waziri jambo lolote likiwa zuri hata kama lilikuwa la ukoloni basi kama zuri tusiliache tu lile. Kwa nini Manispaa haifanyi kama enzi ya zamani kuweka *inspector* ambaye alikuwa anasaidiwa na Wizara ya Afya, huko nyuma ninavyokumbuka kuhakikisha kwamba kila mtaa wakashirikiana na Madiwani wetu kuhakikisha kwamba usafi wa mazingira unakuwepo, na ziwepo *by laws* ambazo zitasaidia, kuona kwamba kama mtu nyumba yake hakuiweka katika mazingira mazuri basi apigishwe faini ili tuhakikishe mji wetu unakuwa mzuri. Lakini Mhe. Mwenyekiti, utaona mji umejengwa mmoja kaelekeza mlango huku, mwengine kaelekeza kwake, maji yanapita hapo na zamani ilikuwa maji ukifua ndani mwako huruhusiwi kwenda nje ili usimkere mwenzako ambaye anafanya kazi ile. Kwa hivyo, mimi namuomba Mhe. Waziri suala hili alitafakari na ahakikishe anakaa na Wizara ya Afya pamoja na Manispaa ili kufanya uchambuzi maalum wa kuwaweka watu wetu hawa, kila mmoja anajulikana mtaa wake ni upi na tufanye *survey* ili kuonesha na kuhakikisha kwamba mji wetu unaingia katika hali ya usafi.

Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikumpongeza au sikuwapongeza Wakuu wa Mikoa wawili wa Pemba pamoja na Wakuu wa Wilaya zao, lakini hasa pongezi maalum zimwendee Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba jinsi alivyofanikisha mwenge, kwa sababu uliwashwa katika Mkoa wake. Kwa kweli alifanya kazi ngumu pamoja na Wakuu wa Wilaya ambao ni Mkuu wa Wilaya ya Chake-Chake pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Mkoani. Niwapongeze sana walifanikisha sherehe zile na hivyo natoa pongezi za dhati kabisa kwao ili na mara nyengine waweze kufanya kazi zao vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa sababu hali yangu sijisikii niseme tu, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na nitawaomba wenzangu na wao waunge mkono hoja. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Omar Ali Shehe ulikuwa hupo nikahisi hutowahi nikamuandaa Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Lakini kwa vile umesharudi basi utaendelea nakurejeshea nafasi yako.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunirejeshea nafasi yangu nikianza na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na afya na tukaweza kuhudhuria kikao hiki.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niipongeze Kamati yetu inayoongozwa na Mhe. Hamza Hassan Juma kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya katika kusimamia ofisi za viongozi wetu wa kitaifa. Pongezi maalum nimpe muwasilishaji wa leo wa hotuba hii kwa namna alivyowasilisha Mhe. Shadya Mohamed Suleiman ambaye ni mpiga kura wangu wa Jimbo la Chake Chake. Kawaida Chake Chake hawafanyi makosa. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza Mhe. Rais kwa kuwa ndani ya kipindi cha miaka miwili na nusu hii anavyoendelea kuliongoza taifa letu hili licha ya kuwepo kwa changamoto mbali mbali za kiuongozi, lakini hadi sasa tunaendelea kushuhudia amani na utulivu kwa juhudi za serikali katika kujinasua na hatua tuliyonayo ya kiuchumi. Kwa hivyo, naomba niitumie fursa hii nimpongeze kwa dhati Mhe. Rais.

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii ni moja kati ya wizara muhimu tulizonazo, kwa vile ni wizara inayoongozwa na mwenyewe Mhe. Rais. Rais wa Zanzibar ambaye ndiye Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ndio kiongozi wa nchi yetu hii. Umuhimu wa pili wa wizara hii ni kwamba ni wizara yenye vikosi vyetu vya ulinzi na usalama vya Zanzibar, ambavyo ndivyo vyenye dhima na dhamana ya kuweka hali ya amani na utulivu. Lakini pia katika wizara hii tuna tawala zetu za mikoa ambazo tawala hizo ndio zenye dhima ya kuweko utawala katika mikoa na wilaya zetu na huko mwisho tuna Idara ya Vitambulisho ambayo ina jukumu kubwa la kuwatambua Wazanzibari halisi na kuwapa haki yao kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, hali ya nchi kwa sasa imetengamaa na kadri tunavyozungumza kwamba imetengamaa maana yake hatuwezi tukasahau kwa sababu wakati wa amani ni wakati wa kujikumbusha mambo ambayo ni yenye kuleta vurugu ili tuendelee kutunza amani. Sasa tulikotoka kipindi cha nyuma kabla ya uongozi huu sote ni mashahidi kwamba tulikuwa na vurugu kubwa sana za kisiasa, vurugu zilizopelekea jamii yetu kuingia katika mitafaruku ya kisiasa, vurugu zilizopelekea uchumi wa nchi yetu mara nyingi kuyumba, vurugu zilizopelekea kwa kweli hata Baraza lako. Mhe. Mwenyekiti, takriban Baraza hili wengi sana ni wapya na wako wachache ambao walitoka katika Mabaraza yaliyopita. Wao ni mashahidi ambapo kuwa

tulikuwa katika Mabaraza yaliyopita Mjumbe na Mjumbe hatuwasiliani, hatusemeshani. Ukisimama na mwenzako kutoka Chama chengine ilikuwa ni vurugu kubwa na kushtumiana, lakini leo *Alhamdulillah* si rahisi kuweza kutofautisha *CUF* ni yupi na CCM ni yupi kwa kweli. Wengine wamekuwa na mahusiano ya karibu hadi katika familia zao.

Mhe. Mwenyekiti, yote hiyo ni matunda ya kuweko kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, kadri ninaposema haya siku zote sisahau wale waazilishi wa juhudi hizi. Mwenyezi Mungu awape umri mrefu walioko hai na awasamehe makosa yao wale yaliotangulia mbele ya haki.

Mhe. Mwenyekiti, maana ya kuwa na *GNU* ni kwamba tumefika pahala yale yote yaliyokuwa yakitufarakanisha tulikubaliana kwamba sasa tuyapigie mstari ili tuanze na zama mpya za siasa za kistaarabu. Katika siasa nchi yetu inaongozwa na viongozi, kuna kiongozi mmoja mkubwa Rais lakini yeye ana wasaidizi wake wawili. Kwa ufupi ni kwamba tuna viongozi watatu katika nchi hii wa kitaifa. Tunaye Mhe. Rais, Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais. Viongozi wote hawa ni viongozi wetu wa kitaifa. Imesadifu kwamba Mhe. Rais ni Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, lakini imesadifu pia Makamu wa Kwanza wa Rais ni Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi *CUF* na imesadifu pia kwamba Balozi, Makamu wa Pili wa Rais ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM. Kwa hivyo, viongozi wetu wote watatu wana kofi za vyama vyao na huwezi ukafika pahala ukasema Mhe. Rais anapokuwepo katika jukwaa kama Makamu Mwenyekiti ukasema yule si Rais wa Zanzibar yule ni Makamu Mwenyekiti wa CCM, hapa pia yupo kwenye jukwaa lake la kisiasa bado ni Rais wa Zanzibar.

Makamu wa Kwanza wa Rais hata akiwa ni Katibu Mkuu wa Chama yuko kwenye jukwaa la kisiasa kama Katibu Mkuu wa Chama bado ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar. Lakini na Balozi kama Makamu wa Pili wa Rais hata anapokuwa kwenye jukwaa la kisiasa kama Mjumbe wa Kamati Kuu bado ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, huwezi kuwatenganisha ukasema yule pale nimtukane kwa sababu Balozi ni Mjumbe wa Kamati Kuu mtukane haiwezekani, yule ni Makamu wa Pili wa Rais anapaswa kujengewa heshima kama Makamu wa Pili wa Rais wa serikali hii.

Kadhalika Dr. Ali Mohamed Shein anapokuwepo katika jukwaa la kisiasa kama Rais huwezi ukafika pahala ukamtukana kwa sababu ni Makamu Mwenyekiti wa CCM haiwezekani, yule ni Rais wa Zanzibar na lazima ujenge heshima. Lakini hivyo hivyo Makamu wa Kwanza wa Rais, Katibu Mkuu Maalim Seif Sharif Hamad, hata anapokuwa katika jukwaa la kisiasa kama Katibu Mkuu wa *CUF* huwezi ukasema yule ni Katibu Mkuu wa *CUF*

ufanye utakavyo aah! yule ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar; inapaswa kumuheshimu kwa namna yoyote kwa sababu yumo ndani ya Katiba na Katiba inamtambua.

Mimi binafsi kwa kweli kumsikia mtu yeyote yule anamtukana Dr. Ali Mohamed Shein, mimi ni mwanachama wa *CUF* kindakindaki, lakini pamoja na *UCUF* haiwezekani tukafika pahala tukaanza kumdharau Dr. Shein, ukaanza kumdharau Makamu wa Pili. Hivyo hivyo na sote tunapaswa tuone kwamba haiwezekani kufika pahala tukamdharau na kumtukana Maalim Seif Sharif kwa sababu ni Katibu Mkuu wa *CUF* pasina kujua kwamba yule ni Makamu wa Kwanza wa Rais, anastahiki ajengewe heshima kama ambavyo wengine tunastahiki nao tuwajengee heshima katika hilo.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi naanza kupata wasi wasi kwamba hizi tabia za kutukanana, kudharauliana zimetoka wapi, na tulikubaliana sote kwamba tuachane na tulikotoka sasa twende kwenye siasa za ustaarabu na kwenye siasa za kistaarabu hakuna ugomvi, hakuna kutukanana, kunakuwa na kujenga hoja kuuza sera kwa wananchi ndio wanaoamua katika siasa za kistaarabu.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi nimesikitishwa na hili tokeo la kwamba Katibu Mkuu wa *CUF* anataka kufanya mkutano wa chama chake na wakajitokeza watu wakafika pahala kwa kweli wakasema asifanye mkutano. Tena najiuliza ikiwa ardhi yote ni mali ya serikali kwa mujibu wa Katiba na sheria, hivyo wanavyojitokeza watu wakafika hapa wakasema wewe fanya, wewe usifanye. Makamu wa Kwanza wa Rais wewe usifanye ni yepi hao au ajitokeze tu Chake- Chake pale tumie uwanja pengine wa *Barcelona* au uwanja mwengine yote ina wenyewe hii. Lakini Makamu wa Pili atakaye kufanya mkutano Chake-Chake wajitokeze watu waseme kuwa huu ni uwanja wetu haiwezekani akataliwe, kwa sababu yule ni kiongozi wa nchi na lazima ashiriki kwani kuna tatizo gani.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mimi mwenyewe binafsi nasikitishwa sana na tabia hii. Nadhani mimi pamoja na u-*CUF* wangu, lakini CCM kwa kweli siidharau kwa sababu CCM ni chama halali kipo na ndicho kinachoongoza nchi, na simdharau CCM yeyote yule ni haki yake. Lakini vile vile nikimsikia mtu anamtukana CCM nadhani sikubaliani naye.

Pamoja na hili vile vile Chama cha *CUF* ndicho kinachoshirikiana na CCM kuongoza nchi hii. Nasema hili kwa sababu limewekwa katika Tawala za Mikoa. Nimepata taarifa kwamba Mkuu wa Mkoa akishirikiana na Mkuu wa Wilaya kazuia mkutano wa kesho. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atupe ufafanuzi, kwa sababu nasema ardhi ni mali ya Serikali. Leo tutapoanza

utamaduni huu wa kuwazuia viongozi wetu wasifanye. Nadhani hili halitotufikisha mbali na ustaarabu huu hatuupati.

Viongozi wote wana haki ya nchi hii ya Unguja na Pemba kufanya mikutano ama ni ya kiserikali au ni ya kisiasa pahala popote pale, haiwezekani sasa tukaanza kusema kwamba Mhe. Dr. Shein anapiga watu kule Chake-Chake hilo haliwezekani. Lakini pia haiwezekani na Makamu wa Kwanza wa Rais au Katibu Mkuu akakataliwa kufanya mkutano wake wa kisiasa huku ikaambiwa kuwa uwanja au ardhi yote ni mali ya Serikali. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anipe ufafanuzi juu ya suala hili kwa sababu hili haliashirii hatma njema kwa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, juzi wakati nachangia katika hotuba ya Makamu wa Pili wa Rais. Mimi niliuliza swali hili kwamba sasa hivi uandikishaji unaaza tarehe 29 yaani kesho na Mkoa wa Kaskazini kuna wengi ambao wana sifa zilizotajwa katika Sheria kwamba awe ni Mkaazi, awe ametimia miaka 18 na cheti cha kuzaliwa kinachothibitisha hiyo miaka, na hapa Mhe. Waziri akaja kuniambia si kweli.

Sasa nimeletewa orodha jimbo la Nungwi pekee lina watu zaidi ya mia nne na nane wana vyeti vya kuzaliwa na ni wakaazi wa jimbo la Nungwi. Watu hao hadi leo hawajapiga hata picha kwasababu Masheha wamekuwa wakiwakatalia na vile vile tayari nimeambiwa kuwa wameshapiga mpaka picha, lakini naambiwa kuwa vitambulisho vyao waende wakachukue mwezi wa 12. Wakati uandikishaji unaaza kesho kwa muda wa siku tatu.

Sasa Mhe. Waziri naomba utakapokuja hapa uje utupe hatma ya watu ambao wana sifa kamili na ambapo kesho uandikishaji utaanza na inavyoonekana kwa vyovyote vile hawa hawatawahi siku tatu za kuandikisha. Ukija hapa Mhe. Waziri naomba uje utupe hatma za hawa. Lakini vile vile pamoja na wale ambao tayari kwa sababu kule tulipokwenda na wewe Mhe. Waziri, Mkurugenzi wa Vitambulisho alituthibitishia kwamba mtu mpaka atakapofika hatua ya kupiga picha hatozidi wiki mbili. Leo kuna watu zaidi wa miezi mitatu wameshapiga picha, leo wanaambiwa mpaka mwezi wa 12 ndio waje wapate vitambulisho vyao.

Kwa hivyo, naomba Serikali baadae mbali ya Waziri lakini pia nipate msimamo wa Serikali kwamba zoezi hili litakuwa siku tatu katika maeneo yale taabani ni kwamba uandikishaji wao utawapita. Lini itakuwa ni hatma ya watu hawa ambao tayari wameshapiga picha na wale ambao wana vyeti vya kuzaliwa hatma yao katika kusajiliwa katika hilo buku la wapiga kura itakuwa vipi maana ni msimamo wa serikali katika hilo.

Na narudia kwamba hili ni lako Mhe. Waziri ndani ya Sheria ile wewe ndiye uliotajwa kwamba ni muhisika kwamba wewe ndiye utakayemuongoza Mkurugenzi. Lakini kama kutakuwa na pingamizi wewe ndiye utakayetoa kauli ya mwisho kwa mujibu wa sheria ile. Sasa sisi hatuwezi kwenda kwengine katika hatua yetu lazima wewe Mhe. Waziri utupe msimamo hapa. Kwa sababu wewe ndiye uliyetajwa kwa mujibu wa Sheria ndiye mwenye kauli ya mwisho katika hilo, na bahati mbaya sisi hapa hatuwezi kumwita Mkuu wa Wilaya akaingia ndani ya Ukumbi. Ukumbi huu kama Wawakilishi sisi wewe ndiye utakayetupa kauli katika hili.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niondoke kwenye Ofisi ya Vitambulisho. Mhe. Mwenyekiti, kuna suala letu la vikosi vyetu vya ulinzi na usalama ni vikosi muhimu sana hasa tunaposema kwamba Zanzibar ina mamlaka kamili. Hivi ni vikosi ambavyo vilikuwepo tangu kipindi cha nyuma na vina umuhimu wake kweli kweli. Sasa ni muhimu sana vikosi vyetu hivi tuvitunze, tuvipe nyenzo inasikitisha kwamba maslahi ya askari wetu hawa ni madogo sana. Leo askari anapokea sijui laki moja na arubaini na wakati askari yule ana njaa unampa silaha unategemea afanye nini.

Tushukuru Mwenyezi Mungu kwamba mpaka leo hayajazuka mambo haya makubwa ya askari kuweza kufyatua risasi. Lakini mtu mwenye njaa unampa rugu mtu mwenye njaa unampa silaha, mtu anaweza akakodisha tu. Tena nasema kwamba hii ni hatari kubwa sana kuviweka vikosi vyetu na njaa halafu tukaendelea kuwapa silaha za moto hatujui kesho na keshokutwa litatokea nini. lazima tuweze kujenga pahala kabla hatujapata athari.

Mimi wito wangu katika hilo lazima maslahi ya askari wetu yaongezwe na yaboroshwe ili kuwepo katika hali nzuri na si heshima kuwakuta askari wenye sare anapita njiani kuomba omba tu si heshima hata kidogo. Tumepata taarifa kwamba leo tarehe 28 maana yake ninavyodhani mimi katika mazingira ya sasa ni busara na vyema kwa Serikali hawa askari tuwatunze tulionao bila ya kuongeza watu wengine ndio hilo suala tunalosema ajira lazima tufike pahala tuangalie tuwatunze tulionao bila ya kufikiria kazi yetu sisi kuongeza askari tu wakati tuliona hatuwatunzi vizuri.

Leo tarehe 28 naomba Mhe. Waziri utakapokuja hapa unithibitishie kwamba katika makambi yetu ya Hanyegwa Mchana watapelekwa askari 300, leo hii wanaajiriwa. Hiki kikosi cha Dunga cha JKU kuna vijana kama 370 leo hii tarehe 28 wataingia katika vikosi kama askari wapya. Lakini leo hii katika kituo chetu cha Kitogani wenzetu wa Zimamoto wataingia askari 400 leo hii. Huko nyuma wacha huko leo hii. Sasa mbona tunafanya ajira hizi holela, ajira ambazo hazilingani kabisa na namna ya uboreshaji wa majaeshi yetu haya na Mhe. Waziri pesa nyingi za kuwaajiri hawa wapi utapata pesa hizi.

Mhe. Waziri tatizo hofu yetu ni kwamba vijana hawa watakapowekwa katika makambi hayo, mwisho wa siku mkaanza kuwababaisha lile vurugu tunalolihofia huenda likatokea. Kwa hivyo, Mhe. Waziri utakapokuja naomba uje ututhibitishie wapi mutapata fedha za kuwaajiri watu hawa, lakini nini hatma hasa ya maslahi ya askari wetu ambao kwa kweli wanaendelea kuzeeka katika majeshi haya wakiwa na maslahi duni sana.

Katika vikosi vile vile Mhe. Waziri kuna suala la watu kuajiriwa kwa mikataba, watu ambao kwa kweli hawana sifa. Mhe. Waziri hili ni tatizo kuna taarifa kwamba kuna baadhi ya watu wanatoka jeshini wameshastaafu halafu mnawaajiri na wala hawana sifa yoyote ni watu wa kawaida tu. Kuna watu mnawaajiri kwa mikataba zaidi ya miaka 5 na mnaendelea tu kuwapa mikataba na hawana lolote wengine hata kusoma na kuandika hawajui.

Sasa leo tunaambiwa sera ni kuwaajiri wale ambao ni wataalamu lakini leo tuna ushahidi kwamba wengine hawajui kusoma na kuandika na mnawapa mikataba zaidi ya miaka 5 mnaendelea kuwapa mikataba tu, kuna kitu gani hapa. Kwa hivyo, naomba na hili Mhe. Waziri utakapokuja utupe ufafanuzi juu ya hatma ya watu hawa na hili maana yake nini. Maana yake linawakosesha fursa ya kupandishwa vyeo watu ambao wanastahiki kupandishwa vyeo katika vikosi vyetu hivi. Jeshi la Wananchi hawakubali hata siku moja kumtoa mtu wao akiwa mtaalamu. Kwa hivyo, Mhe. Waziri kunakuwa na utaratibu kama huo tunaomba ufafanuzi wa dhati ili tufahamu hatma yao.

Lakini vile vile katika suala la vikosi Mhe. Waziri nimepata fomu hii inaitwa *DFF* ya 804 hati ya kiapo Jeshi la Ulinzi KMKM. Hii fomu Mhe. Waziri ikoje kwa sababu inaonekana hii ni fomu ya kuajiri katika kikosi hichi, na nilipoangalia tarehe inaonesha ya miaka hii 2000 yaani ya karibuni tu. Lakini moja kati ya sifa ya uajiri uliomo katika fomu hii katika kifungu cha 9 inauliza kuwa wewe ni mwanachama wa CCM? na kama ndio, maana yake pale atatia namba ya kadi. Sasa Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri akakapokuja aje anipe ufafanuzi wa fomu hii.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa mimi sitaki nizungumzie fungu lolote lile kwa sababu naamini wenzangu wameshatizama zaidi katika kupata ufafanuzi wa mafungu. Lakini nikiwa kama Mwenyekiti wa Kuchunguza na Kudhibiti Mahesabu ya Serikali naomba niseme tu kwamba Ofisi ya Rais ni wizara moja inayotengewa bajeti kubwa mpaka taasisi zilizomo kwenye Ofisi ya Rais.

Ripoti za Mdhibiti na ripoti zile za *PAC* zinaonesha kwamba huwa kuna matumizi makubwa sana na matumizi ya ovyo. Naomba nimetumia neno hili

maana matumizi haya hayafuati sheria tulizonazo wala hayaleti tija tunayoihitaji. Sasa na vile vile katika bajeti hii tulionayo Mhe. Mwenyekiti inaonekana kuwa ni hivyo, fedha zinaingizwa kwa wingi, lakini hasa katika miradi ambayo kwa kweli tayari imeshaingiziwa fedha nyingi.

Naomba nitabahishe tu kwamba Mhe. Waziri anapaswa awe makini sana katika matumizi ya fedha hizi, kwa sababu nachelea haileti sifa nzuri kwamba Ofisi kubwa kama ya Mhe. Rais kila siku ikiwa iko midomoni. Ofisi ambayo ilikuwa inatakiwa iwe na matumizi mazuri na sahihi ni Ofisi ya Rais kwa sababu yeye ndiye kiongozi wetu wa nchi, yeye ndiye *symbol* yetu. Jana hapa ilizungumzwa kwamba Makamu wa Kwanza wa Rais anapandishiwa bajeti.

Lakini Makamu wa Kwanza hajui chochote, waziri ndiye anayehusika pamoja na watendaji wake. Ile picha inayojengwa inaweza ikamuathiri yeye moja kwa moja. Sasa na hii nachelea kwamba isije ikaonekana Mhe. Rais ndiye aliyekuwa na mafungu haya, huyu Mhe. Rais hajui chochote kinachoendelea. Nnachosisitiza hapa maana yake watendaji katika Ofisi ya Rais wanapaswa wawe makini sana katika matumizi ya fedha ili kujenga heshima ya ofisi muhimu sana katika nchi yetu. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*).

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa siku hii ya leo Ijumaa kumshukuru Mwenyezi Mungu Muumba wa yote, mtukufu kwa kutuamsha tukiwa hai na wazima tukiwa tuko hapa tunaendelea na shughuli ambazo wananchi Wazanzibari wametuchagua. Mhe. Mwenyekiti, naomba nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii.

Mimi niungane na mama yangu Mhe. Asha Bakar Makame kukupongeza kwa jinsi unavyofanya kazi yako kwa uenyeji mkubwa. Si rahisi Mhe. Mwenyekiti, kuingia Baraza kipindi cha kwanza ukapewa dhamana ya Uenyekiti ukaliongoza Baraza namna unavyoliongoza. Nakupongeza sana. Nataka nikuhakikishie ukiwepo hapo juu ukilivaa hilo joho unapendeza kweli kweli kwenye kiti chako.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti Baraza la Mapinduzi Dr. Mwinyi Haji Makame kwa kuwasilisha bajeti yake vizuri sana jana. Na akiwa amejipanga na vitabu vyake vinne, kitabu cha bajeti pamoja na vitabu hivi vya utelekezaji wa maagizo ya Wajumbe wa Baraza yametolewa katika kuwasilisha bajeti 2012 na jadweli ya utekelezaji wa malengo ya utekeelzaji wa Serikali za Mitaa kwa mwaka mwa fedha 2012/2013 na malengo ya bajeti ya mwaka wa fedha 2013/2014 pamoja na maelezo ya bajeti inayotumia programu kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Ni matumaini yangu Mhe. Mwenyekiti, kama ilivyokuwa vitabu hivi vizuri na vimepangika basi na utendaji wa kazi *inshaalla* na watendaji wa kazi na wasaidizi wake utakuwa namna hivyo hivyo. Mhe. Mwenyekiti, tunajadili bajeti ya Ofisi wa Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi haitakuwa haki na wala si uungawana kuchukua fursa hii kumpongeza na kumshukuru kiongozi wetu Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dr. Ali Mohd Shein.

Dhamana ya kuongoza nchi si kazi nyepesi Mhe. Mwenyekiti, na hasa nchi ambayo kwa muda mrefu ilikuwa katika misukosuko ya kisiasa. Lakini mwenzetu Mhe. Rais wetu alipata bahati yeye alipopewa dhamana ya uongozi kutoka kwa mwenzake mtangulizi wake Mhe. Aman Abeid Aman Karume, Rais Mstaafu akiwa nchi ameiacha katika hali ya utulivu na amani kufuatia maridhiano ya Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza mpaka sasa hivi amejitahidi kuendeleza ile hali aliyoikuta. Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema Mhe. Omar Ali Shehe hatuwezi kuacha kuwasahau watu ambao walianzisha utaratibu uliopelekea kupata maridhiano ya kisiasa Zanzibar na hatimae kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mimi nataka niendelee kuwashukuru kuwapongeza na kuwaombea dua kwa Mwenyezi Mungu awe na umri mrefu, awape afya aliyekuwa Rais wa Zanzibar Mhe. Aman Karume na Katibu Mkuu wa *CUF* Maalim Seif Sharif Hamad kwa kuanzisha mazungumzo ya kamati ya maridhiano iliokuwa chini ya mzee wetu mmoja katika Wajumbe wa mwanzo wa Baraza la Mapinduzi Mzee Hassan Nassor Moyo na mimi nilipata bahati nikiwa mmoja katika Wajumbe wake.

Lakini itakuwa hazikamiliki shukurani zetu kama sikulipongeza Baraza hili na kamati ambayo imeundwa chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Ali Mzee Ali ambaye alipewa jukumu la kasimamia kazi ya utekelezaji au uendeshaji wa kura ya maoni baada ya kazi kubwa iliyofanywa na aliyekuwa kiongozi wa upinzani wakati huo Mhe. Abubakar Khamis Bakary baada ya kuleta hoja binafsi katika Baraza kuomba kwamba mazungumzo yale yaliofanyika na viongozi wawili wale yaridhiwe na Baraza na Baraza litoe muongozo wa namna ya kuyatekeleza.

Kwa hivyo, nawapongeza wote nawaombea umri mrefu na afya njema. Ustaarabu ulioje kwamba Mzee wetu Mhe. Ali Mzee bado tunaye katika Baraza hili na Mhe. Rais ameona umuhimu wake na akaendelea kumteuwa ili kila tukitaka kupotea atukumbushe, kwa sababu kamati yake imefanya kazi kubwa sana haikuwa na kazi ndogo kuwajengea hoja Wazanzibari mpaka

wakakubali hatimae thuluthi mbili ya Wazanzibari asilimia 66 wakapiga kura ya ndio kuunga mkono uanzishwaji huo mpya Zanzibar, nawapongeza sana.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema haya nimuombe Mhe. Rais awe na hadhari sana na baadhi ya washauri wake na wasaidizi wake. Kuna baadhi ya vitendo vinavyofanyika haviashirii lengo zuri la kutaka kuiendeleza hii hali ambayo aliikuta.

Mhe. Mwenyekiti, sitaki kuchukua muda mrefu kuyazungumza hayo. Lakini moja amelizungumza mwezangu Mhe. Omar Ali Shehe kwamba mambo ya kuzuiliana kufanya mikutano ya hadhara ni mambo ambayo yameshapitwa na wakati katika zama hizi, hayapendezi na kasema kwamba itakuwa ni jambo la ajabu ikiwa mtu katika eneo lake aseme hataki kwa sababu hili ni la upande fulani. Hasa ikija kutokezea kwa upande wa *CUF* ukasema basi kwa upande wa CCM Pemba isifanye mkutano utakaa vipi, si tutarudi kule kule Mhe. Mwenyekiti.

Katika hili mimi nawapongeza Jeshi la Polisi katika kadhia hii inayozungumzwa. Jeshi la Polisi limeonesha uaminifu mkubwa lakini viongozi na Wakuu wa Wilaya wameridhika katika hili wanataka kumuharibia Mhe. Rais, lakini niombe Mhe. Rais na nimuombe kaka yangu vile vile Mhe. Dr. Mwinyi Haji Makame kwa sababu yeye ndiye msaidizi wake mkubwa katika nchi. Yale matukio yamekuwa kama kawaida pale Darajani kila baada ya siku mbili tatu kwenda kuvamiwa wafanyakabiasha pale mpaka zikapigwa risasi za moto. Mhe. Mwenyekiti, tangu litokee hili sijaligusa haidhuru limetokea katika jimbo langu. Mara nyengine ukisema unayachochea, lakini leo nataka niyaseme na namuomba sana Mhe. Waziri katika hili mara nyengine kauli zake zile za kuashiria kuwa anashajihisha kutokee vile.

Siku moja alipokuwa akijibu swali alitamka pengine kateleza ulimi tu kwamba ushindane na serikali. Sasa kauli kama zile inawezekana katoa kwa nia njema kabisa lakini ikatafsiriwa vyengine kwa watendaji. Mimi hapa naomba akija kufunga bajeti hii Mhe. Waziri atoe kauli na tuone kwenye vitabu vyake, mimi sikatai kweli pana vurugu na inasababisha hali inakuwa mbaya. Lakini tutafute njia za kisiasa na za kistarabu za kushughulikia na njia moja aliwahi kuizungumza Mhe. Asha Bakar Makame kwamba tutafe njia kwanza kabla ya kuwafanyia vile vishindo vya kuwaondosha tuwajengee mazingira mazuri hapo tutakapotaka kuwapeleka wakafanye kazi.

Lakini pale wanatafuta riski baada ya kutuomba sisi tumeshindwa kuwatafutia ajira wamejiajiri wenyewe. Sasa inawezekana utaratibu si mzuri basi tujenge utaratibu mzuri na madhali wanatafuta ajira siku zote wafanyabiashara pale

walipo ndio walipo wateja na pale ndio imekuwa panapo harakati zote. Sasa alisema Mhe. Waziri hivi karibuni wanafikiri kuondoa kituo cha daladala pale eneo la Darajani. Mimi namuunga mkono katika lile na mimi mwenyewe kama Mwakilishi niliwahi kuitwa Baraza la Manispaa na Mkuu wa Wilaya alikuwepo wa Mjini wakasema lengo tushirikiane nikawapa fikra kwamba pale panapo kituo cha daladala ndipo panapopatikana wateja wanaokwenda katika maeneo yote wa nje wanakuja pale. Tunaweza kuweka utaratibu mzuri.

Mimi nakubali kama ni Mwakilishi kwamba mazingira pale pana skuli si vizuri inakuwa vigumu pale wanafunzi kuweza kusoma. Lakini na bado hatujakiondosha kile kituo bado wafanyabiashara watabaki pale pale. Kwa hivyo, nilikuwa naomba utaratibu pale Darajani kiwe ni kituo cha kupita na kuteremesha abiria halafu daladala zinakwenda katika kituo kikuu. Yako maeneo hapa nimetaja eneo ambalo liko mbali na mji Mpendae. Lakini kuna eneo jengine Michenzani pale karibu na Kisonge. Pale eneo zuri Ofisi ya Manispaa iliniambia nikasema wazo zuri, kwa sababu pako mjini penye harakati na tukihamishia pale itakuwa tushafika mjini na bado tutakuwa tuna soko.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri katika hili yale marisasi ya moto yanayolia kila wakati pale Darajani yanaharibu taswira nzuri ya eneo lile. Leo utalii mmeuzungumza sana na kwa ukali hapa kama unaharibika kwa fujo hasa kwa matukio kama yale yanaleta hasara na mimi siamini kwamba askari wale wanakwenda kwa utashi wao watakuwa wanaagizwa. Katika nchi inafuata utawala wa sheria wanafika wanavaa ninja wanavaa masoksi anabakisha macho tu, kama kunakataza hakuna vitendo vya uhalifu na ugaidi, lakini kwa sura inaonekana vipo.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kwa heshima na taadhima hebu hili lisimamie kaa na watendaji wako muone vipi mnaweza kulikwamua. Lakini kama nilivyosema hapa muwatafutie mbadala zaidi wale ikawa kuna huduma zote zinazohitajika mimi naamini watakuwa na ushirikiano mkubwa sana. Kwa hivyo, kwenda kuwavamia na kuwanyang'anya riski zao pale litakuwa jambo sio zuri. Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka nilizungumze hilo. Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Rais hili alitizame vizuri ili watendaji na washauri wake na wasaidizi wake wasije wakalikoroga, hali hii aliyorithi kuwa katika hali nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo naomba Mhe. Waziri akija anisaidie katika hotuba yake katwambia kuwa mwaka jana wamefanya matengenezo makubwa ya majengo mbali mbali ya serikali hasa ya Ikulu. Bila shaka viongozi wetu wanataka kukaa kwenye mazingira mazuri kwa sababu

kiongozi wa nchi ni taswira ya nchi, lakini napata wasi wasi tu kwamba fungu hili linakuwa kila mwaka vipi na linaendelea. Nataka akija Mhe. Waziri atusaidie maelezo kidogo katika hili kwa sababu upande wa wenzetu Jamhuri ya Muungano iliwahi kuja kadhia moja ikawa kashfa, kwamba fedha zinatengwa kila mwaka za matumizi kwa ajili ya matengenezo maana yake zinaishia katika mifuko ya watu. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nasema hebu akija aturidhishe juu ya matumizi gani yaliyofanyika na bado yepi hayajafanyika ambayo yanaingiziwa fedha zile. Mimi sizungumzi kifungu kimoja kimoja nazungumzia kwa ujumla hapa.

Mhe. Mwenyekiti, tatu naomba niende kwenye Baraza la Manispaa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, kitovu cha Manispaa ya Zanzibar ni Mji Mkongwe na mwenyewe Mhe. Waziri analitambua hili pale ndio panapo sura ya nchi yote. Kwanza Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri katika ripoti yetu ya kutengeneza Manispaa kuna swali moja tumelizungumza mle na Mhe. Waziri nakumbuka tulipomwita tukamwambia akasema alikuwa hana kumbukumbu nalo lakini atalifanyia kazi. Suala la kuwa na ramani ya Manispaa ya Zanzibar, katika ile sheria ya Manispaa. Kutakuwa na ramani inayoonesha mipaka na ramani ya Manispaa ya Zanzibar. Akatwambia kuwa ata-*review* kwa sababu ile sheria ilikuwepo na nakumbuka Mhe. Salmin Awadhi alifanya kazi kubwa akatumia udhoefu pale akasema hili halipo mpaka leo. Akatwambia kuwa Mhe. Waziri kwamba atalifanyia kazi hebu akija anisaidie amelifanyia kazi au vipi hatujui.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi kama nilivyosema ni hali ya utendaji katika Baraza la Manispaa kwa ujumla Mji Mkongwe unanihusu lakini na hili pia. Bado Mhe. Mwenyekiti, tunashindwa kusimamia sheria na kanuni za viongozi wa Baraza la Manispaa. Swala la uchafu limekithiri katika Mji aibu Mhe. Mwenyekiti, nchi ya watu wastaarabu Zanzibar katika dola kongwe kuliko zote kusini mwa jangwa la sahara. Leo watu wastaarabu kama sisi tuandikwe katika maneno mazito mazito halafu anakuja mtalii anaona taswira mbili tofauti.

Mhe. Mwenyekiti, juzi tulikuwepo Pwani Mchangani pale katika hoteli kulikuwa na semina. Ukipita pale taswira ile hebu ondoka halafu uje uteremshwe Darajani halafu uone ile chafukoge uliokuwepo pale katika barabara ile. Mtu hawezi kuamini kwamba hii ni nchi moja.

Sasa fedha wanakusanya na maeneo safi ya kuweka Mji Mkongwe tunakamuliwa mpaka basi, lakini pia kwa sababu hazitoshelezi tunawatengea ruzuku kila mwaka. Sasa mbona huduma hazipatikani, majaa mpaka yanafika kufurika, wanaweka yale makontena ya kuwekea taka mpaka yanafurika na kumwagika nje hawayaondoi. Zamani nilipokuwa mdogo nakumbuka ilikuwa

kila siku ya Mungu ikifika jioni lazima linakuja gari la Manispaa linachukua taka zile na kubadilisha lile kontena. Kuna tatizo gani hapo.

Mhe. Mwenyekiti, sheria za Manispaa zinasema kusimamia *public health*, tumepitisha sheria ya kusimamia afya ya jamii hapa. Lakini leo utakuta kila pahala makaro yanafoka yamepasuka, kila unapokwenda wanakuambia hii ni dhamana ya majenzi kwa sehemu za Michenzani, ukenda majenzi wanakuambia hii ni dhamana ya Mji Mkongwe, ukenda Mji Mkongwe wanakuambia hii ni dhamana ya Baraza la Manispaa. Kila mmoja anamtupia mpira mwenzake, wakati hii ni serikali moja. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, bado ni tatizo.

Pia Mhe. Mwenyekiti, hali ya masoko yetu. Sokoni ni pahala pa kwenda kununua chakula kwa ajili ya kula wewe mwenyewe, hali ya masoko yetu hairidhishi tumesema kwenye ripoti ya Manispaa ile tumelitamka kwa urefu sana. Lakini bado hali hairidhishi Mhe. Mwenyekiti, mambo haya anapoanza mmoja halafu ikawa humwambii na humsimamii. Zamani kasema hapa mheshimiwa Bi. Asha palikuwa na *inspectors.* Sasa ukimwacha yule wa kwanza basi ataendelea na wa pili, ataendelea na watatu na wakishafika 50 au 100 ndio tena inakuwa vurugu na kuja kuwahamisha inakuwa kishindo sasa. Kwa hivyo, ingekuwa watu wanafanya dhamana zao, wote wapo hawa kwa mujibu wa sheria na tulipofanya kazi ya kuwatembelea Manispaa tuliwakuta watu hawa wapo. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba tulitizame suala hili sana.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, bado tuna ujenzi holela katika mji. Inawezekana unamjua mtu wako fulani katika Manispaa, ukifika anakukatia kibali anakuambia nenda kajenge. Matokeo yake unakuta shaghala baghala. Sheha anatoa kibali, Diwani anatoa kibali, Manispaa anatoa kibali, Idara ya Majenzi wanatoa kibali. Kila nyumba imetoa mlango upande wake, ile imemgeukia huyu kwa nyuma na ile imemgeukia huyu kwa mbele, hatufanyi yale katika karne hii ya 21.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba nitoe mitazamo sasa. Nchi yetu inakua tumesema katika malengo yale tunataka kufikia kiwango cha chini ya pato la kati. Haya yanakwenda pia baada ya viwango vya ujenzi na viwango vya maisha vya nchi. Kwa hivyo, nilikuwa naomba hili pia tusaidiwe.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba niende katika vikosi. Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nianze kwa kuvipongeza sana vikosi vyetu vya SMZ. Najua mara nyengine na hata mimi nimechangia hapa yalitokea matukio ambayo yanaharibu taswira yake, lakini mimi naamini hawa ni wachache. Lakini vikosi vya SMZ kwa Zanzibar ndio fahari ya Zanzibar. Nchi yoyote Mhe.

Mwenyekiti, jeshi au vikosi vya ulinzi ni fahari ya wananchi wake na ni fahari ya nchi husika. Katiba ya Zanzibar imeainisha vikosi vya SMZ na wenzetu hawa haweshi kuvitaja kwa maneno, vinawashughulisha sana.

Mhe. Mwenyekiti, juzi nilikuwa nasikiliza mdahalo ule wa *Professor Shivji*, vimemkaa na roho wanavizungumzia vikosi vya SMZ, wamevikuta na wataviacha hapa hapa tutavilinda kwa maslahi ya watu wa Zanzibar. Kwa sababu sisi tunapokuwa tumelala tukapumzika, wao hao wanakesha kutulinda na kuhakikisha nchi inabakia katika hali ya amani na utulivu.

Mhe. Mwenyekiti, na vikosi hivi sasa vina hadhi zaidi kwa sababu hatujui hatma yake Katiba mpya itakuaje. Lakini katika hii rasimu hivi vinatambuliwa. Katika ibara ya 232 ya rasimu inasema,

Ibara ya 232 ya Rasimu ya Katiba mpya.

"Polisi washirika wa muungano, bila ya kuathiri masharti ya Katiba hii", ni hiyo rasimu, lakini mpaka ipitishwe ndio iitwe Katiba. "Nchi washirika wa Muungano wanaweza kuanzisha vikosi vya ulinzi vitakavyosimamia masuala ya usalama wa watu na mali katika maeneo yake. Vikosi vya ulinzi na washirika wa Muungano vitatekeleza majukumu yao kwa ushirikiano na Jeshi la Polisi la Jamhuri ya Muungano ili kuepusha mgongano wa mamlaka katika utekelezaji wa majukumu katika maeneo hayo".

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo huko tunakokwenda vikosi hivi vitakuwa na umuhimu mkubwa zaidi kuliko hata hivi tulivyo sasa. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kama vinafanyakazi kubwa basi na sisi tuvitunze. Kwanza nimesikitika kidogo na nimeshtuka na hili alilolizungumza Mhe. Omar Ali Shehe kwamba kumbe katika sehemu zao ndio tunawaingizia kipengele cha uanachama wa chama fulani cha siasa. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, hili na mimi nitatoa kauli kwa sababu hili ndio linaharibu taswira yao, na mimi siamini kama utashi wao hawa, kwa sababu Katiba ya Zanzibar inakataza hiyo. Kwa hivyo kuingiza kifungu kile ni kuivunja Katiba ya Zanzibar. Mimi baada ya kusema Mhe. Omar nimefungua Katiba hapa.

Mhe. Mwenyekiti, Katiba ya Zanzibar ibara ya 121(4) inasema:-

Katiba ya Zanzibar ibara ya 121(4)

"Mtu yeyote aliyekuwa katika utumishi wa Idara Maalum haruhusiwi kujishughulisha na mambo ya siasa isipokuwa kupiga kura katika uchaguzi wowote kulingana na masharti ya kifungu cha 7 cha Katiba".

Sasa leo tunapowaingizia sehemu ya kujaza uanachama wake tunawaharibu taswira yao. Suala hili Mhe. Waziri kama lipo basi walirekebishe tusonge mbele. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba madamu wanatufanyia kazi nzuri basi Mhe. Waziri na sisi tunahitaji kuwatunza. Lakini kuna malalamiko makubwa sana na hii ndio nukta yangu ya mwisho. Nina mifano kadhaa ya kuelezea.

Mhe. Mwenyekiti, hawa wanalalamika sana juu ya haki zao. Mara nyingi tunapiga kelele, wako baadhi karekebisha Mhe. Waziri na mimi nampongeza kwa kazi yake. Lakini yako mengine sijui kama ni ukosefu wa ufuatiliaji au kwamba anadanganywa na wasaidizi wake katika hili. Mimi naamini kwamba hawakudanganyi hawa, kwa sababu haiwezekani ukapokea malalamiko kwa askari wasiopungua 50 wa vikosi mbali mbali wakawa wanakuambia jambo moja, haiwezekani ikawa wanakudanganya Mhe. Waziri.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kuna masuala hapa. Kwanza hawa wanatumia, wengine wameunda kampuni za ujenzi ndani yake. Zaidi wanatajwa KMKM lakini na vikosi vyengine pia vinavyo. Wale wanapelekwa wanakwenda kufanya kazi ya ujenzi Mhe. Mwenyekiti, hawalipwi kazi ya ujenzi, malipo yao ni ule mshahara wao. Lakini zile kazi za ujenzi wanazozifanya zinalipiwa zile, fedha zile wana utafiti wanasema hazijulikani zinaingia katika *account* gani. Wakiulizwa wanasema zinaingia katika *canteen*, wakati *canteen* kwenye chakula Mhe. Mwenyekiti, kila mwaka tunatenga fungu na tumelitononesha fungu la chakula kwa askari wa vikosi vyetu vya SMZ. Sasa tunavyoambiwa kwamba fungu hilo au *account* hiyo anayoijua ni mkubwa wa kikosi na mhasibu wake. Hebu tusemeni, kwa nini tunawatumia hawa tunawafanyisha kazi halafu tija inakwenda kwa watu wengine, sio utaratibu mzuri Mhe. Mwenyekiti.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, hawa askari vile vile mara nyengine wanapelekwa kulinda katika majumba na maofisi mbali mbali, basi pesa zao zingekuwa ni mapato yanayoingia katika vikosi na tungetarajia kuwa mapato yake yanaonekana, lakini basi wao askari hatuwafikirii angalau kuwapa zile peza kwa hizo kazi wanazokwenda kuzifanya, angalau motisha ya posho fulani.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, mazingira yao ya kazi, tumesema sana hapa. Mimi katika kamati zilizopita nilikuwa mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, katika wajumbe wetu Mhe. Bi. Panya anajua hili. Tulikwenda kutizama vyuo vya mafunzo Pemba, makazi yao yanasikitisha sio makaazi ya kukaa binadamu. Nyumba kwanza taabani kwa ubovu lakini katika hiyo nyumba kila askari kapewa chumba kimoja, anakaa yeye, mkewe na wanawe. Wale wanafunzi wa vyuo vya mafunzo au wafungwa wanavyoitwa, basi walituambia sisi tumeshakuwa wafungwa hapa tumefanya

makosa, kwa hivyo sisi tukiwa katika mazingira haya yatupendwi, lakini hata hawa wanaotulinda na wao wanakaa katika mazingira mabaya kama haya.

Mhe. Mwenyekiti, jengine hawa askari wakistaafu bado haki zao hazifanyiki na ndio maana wanaishia mitaani, wanakuja kufanya kazi za kulinda. Mtu kama alikuwa afisa mkubwa sana, basi anarudi anakuwa mlinzi katika duka la mtu tu, tunawadhalilisha Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, jengine katika haki zao ambalo tumelipigia kelele sana na hili hasa ni katika JKU, nafikiri hata kwenye KVZ huchukuliwa wakapelekwa JKT kwa ajili ya kuandaliwa kwa ahadi kwamba wataajiriwa katika Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Lakini baadae hakuna ajira, nani anasimamia haki zetu katika muungano.

Mhe. Mwenyekiti, juzi Mhe. Hija Hassan hapa alisoma orodha yenye asilimia inayoambiwa itatengwa kwa ajili ya....

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, umebakiza dakika 4 kumalizia.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nitajitahidi nimalize.

Juzi alizungumza hapa Mhe. Hija Hassan ile takwimu ambayo waliambiwa hawa askari watapata mgao wa asilimia 25 Zanzibar, lakini walipokwenda katika ajira wameachwa, wengine wamefikia vile viwango vinavyotakiwa, wana digrii na diploma wameachwa wamechukuliwa watu kutoka Tanganyika. Ni nani anayezilinda haki zao?(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, maeneo mengine ambayo nayapigia kelele, mfano kikosi cha JKU. Wanasema miaka kadhaa iliyopita walichangishwa kila mmoja shilingi 2,000/=, wakaambiwa zinakusanywa ili wafanyie mradi. Wengine wakagoma wakasema hatuzioni tuletewe hesabu yake. Ikapigwa kura wakaitwa wakilishi wote kwamba zigaiwa zirudishwe kwa wenyewe, kila mmoja apewe shilingi 42,000/=, tukaambiwa aliyepewa labda ni asilimia 25 na asilimia 75 mpaka leo fedha zao hawakuziona tena.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, jengine ni suala la michezo. Mhe. Waziri katika hotuba yake kataja kuna fungu la michezo. Hili nilimuambia mimi mwaka jana, wachilia mbali hili litakomeshwa kuwachangisha lakini wanatuambia timu zikifika kucheza ligi bado wanakatwa wanaambiwa wachangie michezo. Mhe. Waziri suala hili lifuatilie zaidi. Wewe Mhe. Waziri unatuahidi kwa nia njema hapa, lakini huko chini bado katika utendaji kuna matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu fedha za likizo. Kuna wengine wanafika miaka mitano hawajalipwa fedha za likizo. Wengine wanatuambia wanalipwa fedha za likizo lakini anapokwenda likizo hapewi, anakuja kupewa baada ya mwaka mmoja, wakati zile pesa za likizo unapewa ili zikakusaidie kwenda katika safari yako ya likizo wewe na familia yako.

Kwa upande wa JKU vile vile Mhe. Mwenyekiti, naomba nisaidiwe ule mradi wa Bambi ambao bado unaendelea katika fedha za maendeleo. Mwaka jana uliwekwa, naomba anisaidie imefikia wapi.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye Chuo cha Mafunzo. Pia kuna matatizo ya fedha za likizo. Lakini kuna fedha ambazo walichangishwa hawa wakaambiwa inaundwa *SACCOS* ya Mafunzo, miaka mitano iliyopita wakaambiwa baada ya muda watarejeshewa fedha zao na ile faida inayopatikana ndio ingetumika kufanyia miradi ya uzalishaji. Hawakulipwa, waliolipwa ni kama asilimia 20. Kwa hivyo takriban asilimia 80 hawajalipwa fedha zao na wala hawajui mustakabali wake utakuwaje.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, *pay role* na *pay slip*. Mara nyingi tumezungumza humu ndani wanadai ili wajue wanacholipwa na mikato yao basi wapewe. Lakini kuondoka nyinyi tuliambiwa kwamba ni wengi hawa na karatasi zitakuwa ni nyingi. Lakini *pay slip* ni haki yake mfanyakazi, kwa nini tunashindwa kuwapatia.

Mhe. Mwenyekiti, ulinipa dakika 4 nimalizie. Naomba kuuliza swali kidogo la mwisho. Katika mgao wa fedha kwa vikosi mbali mbali hivi JKU wametengewa zaidi ya bilioni 7, Mafunzo kuna zaidi ya bilioni 6, KMKM kuna zaidi ya bilioni 9. Lakini kikosi cha Zimamoto na Uokozi na Kikosi cha Valantia wametengewa bilioni tatu tatu wao. Kwa hivyo, naomba maelezo kwamba hawa ni askari kidogo au mahitaji yao ni machache, kwa nini imekuwa hivyo. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba hawa ni watu wa kuwatunza sana.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho kabisa naomba maelezo kuhusiana na KMKM. Ninayo barua hapa kwamba kumekuwa na taratibu ya kupandishana vyeo na ni haki ya watu. Lakini wanalalamika askari kwamba ule utaratibu wa kijeshi au wa kikosi haufuatwi. Watu wanawapeleka jamaa zao. Ninayo barua hapa Mhe. Mwenyekiti, ya tarehe 20/06/2013 imetoka Makao Makuu ya KMKM, imesainiwa na Komadoo mmoja namsitiri kwa nidhamu za jeshini. Lakini kawapelekea wakuu wa kamandi na idara. Wanaotakiwa kupandishwa vyeo Mhe. Mwenyekiti, ni wale ambao wamekwishafikia nafasi ya *CPA*, lakini humu ukisoma orodha ina watu 72, wamo wa *PA* na *LS* ambao hawa hawana sifa za kupandishwa vyeo kwa utaratibu wao.

Sasa wameachwa wale waliokuwa na *CPA* wamechukuliwa watu na jamaa zao wakawabandika. Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba tena navipongeza vikosi vya SMZ kwa kazi kubwa wanayoifanya na ninawaomba wasivunjike moyo, wana matatizo waendelee kufanyakazi ya kutulinda. Niwakumbushe, nilipokuwa nikichangia bajeti nilisema kuna bilioni 163 kutoka Serikali ya Muungano ambayo ni haki yetu lakini hatuzipati. Hizi siku zikiingia mkononi kila mfanyakazi wa kikosi cha SMZ askari anaweza kulipwa hata shilingi 500,000 kwa mwezi kwa hapa Zanzibar na maisha yakawa mazuri kabisa, ni suala tu la kujipanga vizuri jinsi ya kuendesha mamlaka yetu, nawapa moyo, wasivunjike moyo wafanyekazi ya kuilinda nchi yetu na watu wake, wakijua hivyo tunakokwenda mbele kuna faraja.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nasema naiunga mkono hotuba hii na nashukuru sana, ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Kazija Khamis Kona: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi ya kuweza kuchangia. Kwanza nimshukuru Allah Subhana Wataallah kwa kutujaalia afya njema tukafika hapa kufanya shughuli zetu ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naanza na vitambulisho. Sheria ya vitambulisho inasema mtu afikie miaka 18 awe na targisi. Lakini Mhe. Mwenyekiti, la kusikitisha ni Masheha wetu wanaomba wananchi targisi wanazo, wameshatimia miaka 18, cha kusikitisha watu hao barua hawaipati hadi watoe shilingi 500. Sasa sijui kwenye sheria hii imo na kama haimo Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri aje anifahamishe vizuri kipengele hiki.

Vile vile suala hili Mhe. Mwenyekiti, mtu akishakwenda kwa Sheha basi anaambiwa aende kwa mjumbe wa Sheha ili akamthibitishe kama anaishi katika kijiji hicho. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli nchi yetu ina masikitiko makubwa kwa kutowapatia haki wananchi wake haki za msingi, ilivyokuwa wananchi tayari utaratibu wote upo, sijui tatizo ni nini linalowasababisha wananchi hao wasipatiwe haki zao za msingi. Namuomba Mhe. Waziri suala hili alifanyie kazi ipasavyo. Kama halipo suala hili kwenye sheria kwamba mwananchi atoe shilingi 500 basi Mhe. Mwenyekiti, wale wananchi wote waliotoa shilingi 500 basi warejeshewe kutokana na hali ngumu za maisha ilivyo, mwananchi ikiwa kila kitu tunamchangisha basi inazorotesha hata uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, tumezipata taarifa hapa ya kwamba Wilaya ya Kaskazini ‘A’, kuna watu zaidi ya 400, tayari wana targisi lakini Masheha hawaambii. Vile vile taarifa tulizokuwa nazo ni kuwa tayari wengine wameshaandikishwa na bado hawajapewa vitambulisho vyao. Sasa namwambia Mhe. Waziri

kwamba hawa walioandikishwa tayari wameshapiga picha na kila kitu, basi afanye jitihada zake leo hii wapatiwe vitambulisho vyao vya Uzanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu cha Mhe. Waziri kimeeleza kwamba kuna Wazanzibari waliokuwa nchi za nje wanahitajia kuchangia maendeleo ya nchi yao ya Zanzibar, na akaeleza katika kitabu chake kwamba wananchi hao waliochangia mradi wa maendeleo, walichangia kujenga maskuli na vifaa vya hospitali. Mhe. Waziri naomba aje aniambie vifaa vya hospitali hiyo ni vipi na wamechangia madarasa mangapi na ni kiasi gani cha fedha kwa mwaka wanachangia Wazanzibari hao walioko nje ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea kuchangia nije kwenye masoko. Mhe. Mwenyekiti, masoko yetu hayaridhishi. Soko la Kinyasini ikinyesha mvua huwa linatuama maji. Kwa hivyo, Mhe. Waziri nakuomba soko hili lifanyiwe matengenezo, litiwe lami, liwekwe na msingi wa kupitia maji ili maji yasituame sehemu zile ili wafanyabiashara waweze kufanya biashara zao kwa ufanisi kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nimuombe Mhe. Waziri kuhusu soko la Saateni. Mhe. Waziri juzi alipojibu swali alitusifia kuhusu soko la Saateni kuwa ni zuri na linavutia. Sasa mimi nimuombe Mhe. Waziri pamoja na uzuri wake soko la Saateni uliopo, soko lile linataka matengenezo ya kuwekwa lami liondokane na vumbi iliokuwepo pale ili wafanyabiashara za nguo zisiingie vumbi.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alifanya ziara hapa ya kuonana na Wawakilishi na Wabunge pamoja na Wakuu wa Wilaya. Lakini kwa masikitiko makubwa ninayompa Mhe. Waziri, mimi ni Mwakilishi wa Wilaya ya Kaskazini ‘A’, lakini hakunialika katika kikao kile, nasikitika sana kwa nini hukunialika. Mhe. Waziri katika kikao hicho kitabu chake kimeeleza madhumuni makubwa uliyoyazungumza ni kuwashajihisha wananchi wakachukue vitambulisho vyao. Kwa maana hiyo vitambulisho inasemekana vimerundikana vingi.

Mhe. Waziri mimi nakuuliza swali kwa sababu mwaka 2005 kuna wananchi walioandikisha vitambulisho hivyo na walipewa vile vishina, wengine vilimi. Je, Mhe. Waziri wananchi hao wapo wenye hivyo vishina na mimi imani yangu inanipa ndio aliyevibakisha vitambulisho vyao. Sasa hivyo vitambulisho vyao bado vipo. Je, ni utaratibu gani Mhe. Waziri utakaotumia ili wale wananchi wa mwaka 2005 tayari wana vishina vyao na hawawezi kuvipata vitambulisho vyao hivi sasa mpaka waoneshe kitambulisho kile kilichopita ndio wapewa chengine. Je, hawa kuna uwezekano wa kupewa vitambulisho vyao walivyovirithi na kama wanao ni utaratibu upi utakaotumika ili wavipate vitambulisho vyao. Ni lini tutapewa taarifa ya

kwamba wananchi hao wote waliokuwa na vishina waende wakachukue vitambulisho vyao.

Mhe. Mwenyekiti, kuna sheria inayosema kama mtu hana kitambulisho basi afungwe. Sasa ni sababu zipi kwa hawa watu waliokuwa hawana wasichukuliwe hatua hiyo.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja pindipo Mhe. Waziri akinipa maelezo ya kutosheleza. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii kuweza kuchangia kwa dakika kumi zilizobakia. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia mchana huu na mimi nikapata nafasi ya kuchangia. Pia nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kutuletea hotuba yao hii nzuri ya makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze na Idara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nianze kuuliza jengo la Ofisi ya Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Mjini. Mhe. Mwenyekiti, jengo ambalo linafanyiwa ukarabati na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, nataka kujua mmiliki wa jengo hilo ni nani kati ya hawa wawili, baina ya Mkuu wa Wilaya na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Mwenyekiti, kama Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na Ofisi Kuu ya Mkuu wa Wilaya zilikuwa pamoja, halafu Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ikawa inafanya ukarabati. Naomba niulize Mkuu wa Wilaya baada ya kupelekwa Bwawani ikawa ofisi yake na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ikawa inalifanyia ukarabati jengo hilo. Je, baada ya kumalizika hiyo Ofisi ya Mkuu wa Wilaya wataweza kurejeshwa pale. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kutupa majibu anipe ukamilifu wa suala hili.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, nije katika Idara Maalum ya Vikosi. Mimi napenda kuvipongeza vikosi vyote vya SMZ kwa kazi nzuri inayofanya. Kwanza niende katika kikosi cha JKU. Mhe. Mwenyekiti, kikosi hiki kinajitahidi kuwapa mafunzo vijana wetu ambao wamemaliza skuli. Ombi langu ninalotaka kuwaomba ni kwamba vijana hawa baada ya kupatiwa mafunzo na pakitokea ajira ni lazima vijana hawa wazingatiwe kwanza ili kupata ajira hizo. Kwa sababu vijana hawa baada ya kupata yale mafunzo halafu tukawaacha warudi mitaani basi kuna hatari ya vijana hawa kujiunga katika makundi yaliyokuwa sio mazuri, kama vile kujishirikisha na madawa ya kulevya na uvutaji wa bangi.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye Baraza la Manispaa, namuomba Mhe. Waziri alisimamie vizuri Baraza la Manispaa, kwa sababu wafanyabiashara wetu wadogo wadogo wanapata shida hasa katika masoko. Mimi nizungumzie suala hili kuhusu wanawake.

Mhe. Mwenyekiti, wanawake wanapata shida katika biashara zao hizi ndogo ndogo, kwa sababu kama tukizingatia wanawake hawa wanahangaika kupata mkopo, halafu wanapofanya biashara zao wanakuwa hawana pahala pazuri pa kutafuta riziki na pia mkopo ule unatakiwa urejeshwe, hivyo hili ni tatizo. Kwa hivyo, namuomba Mhe.Waziri suala hili aliangalie vizuri kuona wanawake hawa wanafanya biashara zao bila ya matatizo yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile nazingatia muda mwisho kabisa, naomba Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ikishirikiana na Baraza la Manispaa kuendelea na zoezi hili la kuwakamata wanyama wanaozurura ovyo. Mimi nataka niipongeze Ofisi ya Mkuu wa Mkoa pamoja na Baraza la Manispaa, kwa sababu kazi hiyo wanaifanya vizuri, hivyo nawaomba waendelee kuifanya kazi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuchangia hayo, kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Mjini Magharibi naunga mkono hoja kwa asilimia mia juu ya mia. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mwanaidi Kassim. Waheshimiwa Wajumbe, mpaka kufikia hapa leo tumemaliza shughuli zetu kwa mchana huu wa leo. Nawashukuru sana kwa utulivu wenu na michango yenu mizuri. Tukijaaliwa tutarudi tena saa 11:00 jioni ya leo. Ahsanteni.

(Saa 6:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea na majadiliano yetu na mbele yangu wajumbe ambao wameomba kuchangia ni 25. Waheshimiwa Wajumbe, tunatakiwa kazi hii tuimalize siku ya Jumatatu asubuhi tukijaaliwa.

Kwa hivyo, nakuombeni sana tuangalie na kuujali muda, ili sote tuweze kupata nafasi ya kuchangia na ikiwa muda umefika ambao nitahisi kwamba hivi sasa tunamaliza basi nitasimama, na Kanuni inaniruhusu kuwataka waliobakia wachangie kwa maandishi, ambapo kama tunavyofahamu kwamba kwa maandishi haiingii kwenye *hansard*. Kutokana na hali hiyo,

ningewaomba sana tujali muda, ili wote ambao wameleta majina yao waweze kupata kuchangia, ahsanteni.

Mchangiaji wetu wa mwanzo atakuwa ni Mhe. Mbarouk Wadi Mussa na baadaye atafuata Mhe. Marina Joel Thomas.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa nafasi hii niwe mchangiaji wa mwanzo jioni hii ya leo katika kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka huu wa fedha 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kujali muda basi na mimi nikuombe kidogo nianze kuyapitia mafungu ambayo niliyaona kidogo, lakini nadhani niende kwenye marekebisho, basi naomba nisiyataje moja kwa moja fungu moja baada jengine, kwa sababu ya kujali muda wako.

Kwa hivyo, naomba niende kwenye mafungu ya jumla na baadaye tena nije niruhusiwe kuja kuyatakia maelezo wakati huo utakapowadia.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye Fungu 08 Ofisi ya Rais Baraza la Mapinduzi nitakwenda kwenye fungu 0701 Ofisi ya Faragha, pia kwenye fungu 10 Ikulu na fungu 1101 Utumishi na Uendeshaji pamoja na fungu 0801 Tawala za Mikoa, nafikiri vimo vifungu vingi sana.

Mhe. Mwenyekiti, nikisema nianze kivitaja kama ulivyosema tujali muda, basi na mimi naheshimu muda wako tusivitaje kwa sasa. Lakini Mhe. Waziri ayaangalie mafungu yaliyonona ajitayarishe na majibu wakati utakapowadia.

UTARATIBU

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, imekuwa vizuri sana Mhe. Mjumbe hayo mafungu anayoyataka ni makubwa mno 08, 07, 011. Kwa hivyo, namuomba ataje *specific* kile kitu ambacho ana matatizo nacho, ili baadaye nipate urahisi wa kuja kukieleza. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, maelekezo yametoka kwa Mhe. Waziri anayehusika. Kwa hiyo, naomba utaje kifungu ambacho utakuwa unahitaji kukihoji.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniruhusu nitumie muda wangu kama Kanuni inavyonielekeza, kwamba nitautumia vizuri ule wa dakika ambazo tunapewa kwa mujibu wa Kanuni na nilikuwa nahofia kwamba nimejaribu kuugawa, ili na wenzangu wengine waweze kuutumia.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, endelea kwenye kifungu.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kwenye mafungu nitaanzia na hili la 08 katika kifungu 220200 viburudishaji fungu 220201 kifungu kidogo, nitakwenda kwenye fungu 220600 Samani za ofisi kwenye kifungu kidogo cha 220603, pia niende kwenye kifungu 220700 matengenezo ya ofisi kifungu kidogo 220702.

Mhe. Mwenyekiti, nikisogea mbele kuna fungu la 263100, niende kwenye 263178 *HIV* ushauri nasaha, nishuke tena kwenye misaada ya kijamii 272100, nisogee kwenye kifungu cha 272108 kusaidia shughuli za kiuchumi.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kifungu cha 311200 ununuzi wa mashine na zana, kifungu kidogo 311202 ununuzi wa gari na kifungu kidogo cha 311216 ununuzi wa jenereta. Kwa hivyo, kwenye kasma 08 hapa ndio limeishia.

Sasa nakwenda kwenye 010 Ofisi ya Rais Ikulu, nitasogea kwenye kifungu cha 220600 samani za ofisi, kifungu kidogo 220601 ununuzi wa mapazia. Mhe. Mwenyekiti, nisogee kwenye fungu la 220700 matengenezo ya ofisi na nyumba kwenye kifungu kidogo cha 220702 matengenezo makubwa ya majengo.

Mhe. Mwenyekiti, niruke kidogo hapo nisogee kwenye Ofisi ya Faragha 0701, pia niende kwenye 220100 gharama za vifaa na huduma kwenye kifungu kidogo cha 220108 huduma za mtandao na 220105 gharama za vifaa vya uchapaji. Halafu nisogee kwenye fungu la 220200 viburudishaji kwenye 220203.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kujali muda wako nisogee kwenye Idara ya Utumishi na Uendeshaji fungu 1101. Kwa hivyo, nitahitaji nipate maelezo kwenye fungu la 211200 mishahara isiyokuwa ya fedha kwenye kifungu kidogo cha 211202 ununuzi wa sare, na niende kwenye 220100 gharama za vifaa 220106.

Nikiendelea sasa nisogee kwenye Kitengo cha Usalama wa SMZ 1601 fungu lake hilo. Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye kifungu kidogo cha 311200 ununuzi wa mashine, niende kwenye fungu dogo 311210.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri kwenye mafungu kwanza nimalizie hapo na nikushukuru kwa kunipa nafasi na sasa niendelee mbele kwenye mchango wangu kwenye hotuba ya Mhe. Waziri.

Nianze kwenye ukurasa wa 19 Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Mapinduzi. Nikiangalia hapa kwenye Ofisi hii ya Baraza la Mapinduzi Mhe. Waziri ametueleza utekelezaji wa kazi ambazo zimefanywa na ofisi hii, lakini nikifungua kile kitabu cha mwaka jana kuna kazi ambazo ameziahidi Mhe. Waziri kwamba zitafanywa katika mwaka huu.

Katika mambo ambayo anatarajia kuyafanya mwaka 2012/2013 katika Ofisi ya Baraza la Mapinduzi, yaani malengo waliyokusudia kwenye lengo la mwisho kule kuna (f) kutathmini utendaji na uwajibikaji wa serikali.

Lakini nikiangalia kwenye kitabu chake hichi ambacho ametusomea hotuba yake hapa sikuona utendaji ambao, yaani hakuuweka kwenye kitabu hichi, kwamba labda kulikuwa na moja, mbili au tatu. Kwa sababu mimi nimejaribu kupitia hapa na sikuangalia vizuri, nadhani Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho, namuomba kupitia kwako Mhe. Mweneykiti, aje atueleze kidogo ile tathmini ambayo wameifanya na kuuona ule utendaji wa serikali namna ulivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa haraka ili niweze kujali muda wako niende kwenye ukurasa wa 30 *paragraph* ya 31 Kitengo cha Usalama wa Serikali (*GSO*). Vile vile nikiangalia na hichi nilirudi kwenye kumbukumbu za kitabu kilichopita cha mwaka jana, Mhe. Mwenyekiti alieleza malengo ya mwaka 2012 kitengo kilitegemea kufanya upekuzi wa awali na upekuzi endelevu kwa watumishi 500 wa serikali.

Lakini katika kitabu hichi Mhe. Waziri anasema katika kipindi hichi anasema kitengo kilifanya upekuzi wa kiusalama kwa wafanyakazi 168 wa taasisi mbali mbali za serikali na kutoa ushauri wa kiusalama kwa taasisi hizo.

Sasa huku alituahidi atafanya kwa watumishi 500, lakini matokeo yake amefanya 168 chini ya kiwango. Kwa hivyo, mimi nataka kujua sababu na ninamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti wakati atakapokuja kufanya majumuisho basi atueleze kwa nini hakuweza kufikia yale malengo yake aliyojipangia.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea sasa niende kwenye ukurasa wa 39 Mkoa wa Mjini Magharibi. Kwa kweli mwaka jana Mhe. Mwenyekiti, alitusomea Mhe. Waziri hotuba yake na kutueleza malengo na mimi niko kwenye malengo, ameeleza humu kwenye kitabu chake cha mwaka jana ukurasa 47 alisema

kwamba Mkoa wa Mjini Magharibi umekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

(c) Kutatua migogoro ya ardhi inayoikabili mkoa kuanzia ngazi ya shehia,
Halmashauri, Baraza la Manispaa, Wilaya, Mkoa pamoja na kushirikiana na
Wizara husika;

(e) Kuanza matayarisho ya ujenzi wa jengo jipya la Ofisi za Mkoa liliopo Amani na kufanya matengenezo ya jengo la Ofisi za Mkoa Vuga.

(f) Kuanza marayarisho ya ujenzi wa jengo la Ofisi la Mkuu wa Wilaya Magharibi.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ipo hapa kwenye kitabu hichi Mhe. Waziri haya malengo ambayo aliyapanga katika kuyafanya mwaka uliopita naona hayakutekelezwa katika kipindi cha mwaka huu.

Sasa nataka kujua kwa nini hakuweza kutekeleza malengo yale basi tukishapata hizo sababu ambazo zenye kuridhisha nafikiri hakuna tatizo Mhe. Mwenyekiti, kwamba maombi ya Mhe. Waziri nitawashawishi Wajumbe wenzangu wamridhie, ili tumpatie fedha kwa ajili ya kwenda kufanya kazi hizi ambazo nyengine ametuomba kwenye mwaka huu.

Mhe. Mwenyekiti, nisogee mbele kidogo kwenye ukurasa 44 wa kitabu hichi cha hotuba ya Mhe. Waziri kwenye Mkoa wa Kaskazini Unguja. Mhe. Mwenyekiti, katika Mkoa wa Kaskazini Unguja Mhe. Waziri mwaka jana kwenye kitabu chake alitueleza hapa malengo yake, kwamba anatarajia katika mwaka huu atakamilisha ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na kuanza ujenzi wa Ofisi za Wakuu wa Wilaya. *(Makofi)*

Nafikiri Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ameieleza kwenye kitabu chake kwamba tayari imekamilika na watu wameshahamia. Ni kweli na tumeshawahi kufika pale na tukaona kuwa Mkuu wa Mkoa yupo pale tayari na anafanya kazi zake. Lakini kwenye hizi Ofisi za Wakuu wa Wilaya sijui Mhe. Waziri atatuambia ameanza kuzijenga wapi, maana yake katika ukaguzi wetu tulipokagua hatukuwahi kupata taarifa ya ujenzi wa Ofisi za Wakuu wa Wilaya ya Kaskazini ‘A’ wala ‘B’.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wakati atakapokuja kufanya majumuisho, basi atusaidie maelezo kuhusu ujenzi wa

ofisi hizi na kama zimejengwa ziko wapi, na hatua gani ambayo imefikia hadi hivi sasa. *(Makofi)*

Lakini kwenye malengo ya mwaka jana Mhe. Waziri pia alieleza hapa kuendeleza juhudi za kupunguza migogoro ya ardhi kwa kushirikiana na wizara husika pamoja na wadau wengine zikiwemo Halmashauri za Wilaya na jamii yenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, pia na humu ameeleza namna ambavyo migogoro ameitatua. Lakini mimi bado kidogo napata shaka na ile migogoro ambayo imetatuliwa. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho atueleze hasa mgogoro wapi na wapi, maana humu ametaja kijumla jumla.

Kwa hivyo, naomba aje atueleze hasa ili migogoro ambayo ameitatua na ile ambayo hakuitatua, na kwa nini hajaitatua mpaka hivi sasa, kwa sababu kama kipindi cha mwaka mzima wenye matatizo ya migogoro ya ardhi bado wanaendelea kusubiri, basi tujue mpaka lini itakuwa imekuwa tayari.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye *paragraph* 34 Mhe. Waziri ametueleza kwamba ukarabati wa jengo la Ofisi Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini 'A' umefanyika, ndicho kile ambacho nilichokuwa napingana nacho, kwa sababu malengo yake ya mwaka jana ni kujenga Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, lakini maelezo yake kwenye kitabu hichi ni ukarabati wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya. Kwa hivyo, hivi ni vitu viwili tofauti, yaani ukarabati na ujenzi.

Kutokana na hali hii namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wakati atakapokuja anisaidie maelezo kidogo, ili niweze kupitisha bajeti yake bila ya kikwazo chochote.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye ukurasa wa 50 kuhusu Idara ya Uratibu wa Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwenye *paragraph* ya 158 Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM).

Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa maelezo yake kwenye kitabu hichi, lakini nataka nieleze masikitiko yaliyokuwepo kwa askari wetu hawa. Kwa kweli kuna malalamiko hata mwaka jana yalijitokeza na niliwahi kama utapata *hansard* ukaiangalia vizuri, basi nilieleza namna askari wetu wanavyopata tabu na malipo yao ya likizo, yaani wanakwenda likizo lakini hakuna malipo ya likizo.

Kwa hivyo, nilimuomba Mhe. Waziri hapa wakati wa kufanya majumuisho anisaidie maelezo, na alipokuja alisema kweli suala hilo lipo na tayari

nimeshalifanyia kazi na muda mchache ujao litakuwa limetatuka. Lakini kwa masikitiko makubwa sana mpaka jana nimewauliza wahusika na wananiambia lile tatizo lipo na bado halijatatuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho atusaidie ni vipi atalitatua tatizo hili, na kwa nini hadi hii leo fedha zao hawa wanaokwenda likizo hawapewi kwa nini kuna tatizo gani, basi ni vyema atwambie ili tuweze kumsaidia na hichi ndicho chombo cha wananchi. Atwambie ili tuweze kumsaidia namna ya kuhakikisha kwamba wananchi wale, maana wale ni askari lakini ni wananchi wanahitaji kupata haki zao na sasa hawazipati.

Vile vile nikiangalia kuhusu masuala ya maombi ya fedha kikosi hichi mwaka jana kilipatiwa milioni 9,660,000,000/=, lakini mwaka huu ni milioni 9,452,000,000/=, yaani baada ya kuzidi imepungua, basi nilikuwa nataka kujua kuna tatizo gani. Mhe. Mwenyekiti, nikiangalia wizara hii, lakini hizi ofisi ambazo nimeziangalia mafungu yake nyingi zimeongeza kiwango cha kuomba zile fedha na zimeongezewa, lakini kikosi hichi naona kimepunguziwa.

Kutokana na hali hiyo, nataka kujua sasa sababu ya kupungua kwa fedha hizi je, wamestaafu wengi sana au kuna tatizo gani mbona fedha zimepungua badala ya kuongezwa maana yake tumeshakuwa na utamaduni hapa kawaida mwaka jana ukiomba 100, basi mwaka huu unataomba 110 au lazima unaomba na ziada, lakini hapa wameomba na zimepungua. Kwa hiyo, naomba ufafanuzi katika hili Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwenye *paragraph* ya 166 Jeshi la Kujenga Uchimi (JKU) nalo lina tatizo kama hili la KMKM kwenye suala la fedha. Kwa mfano, mwaka jana walikuwa wamepewa shilingi milioni 7,504,000,000/=, lakini mwaka huu shilingi milioni 7,457,000,000/= hapa napata kigugumizi.

Mhe. Mwenyekiti, wakati huo huo kuna hoja hapa mwaka jana katika kikosi hichi kilituchukua muda mrefu sana kama utakumbuka Mhe. Mwenyekiti juu ya shamba la mboga mboga la Bambi. Nimeona hapa kwenye taarifa yake Mhe. Waziri hawakutiliwa zile fedha kama ambavyo Baraza liliagiza kwamba msipewe mpaka mtoe taarifa, lakini bahati mbaya taarifa ile hamkuwahi kutoa na fedha zile ndio maana hamkupewa, yaani ile ripoti haikuwasilishwa hapa Barazani.

Lakini mara hii munaomba kwa shamba lile lile. Mhe. Mwenyekiti, nataka nimwambie Mhe. Waziri katika hili ni kwamba msimamo wangu utabakia kama mwaka jana kuzizuia fedha hizi, kwa sababu ile ripoti ambayo

muliambiwa muiwasilishe hapa Barazani hamkuileta na kuna agizo kabisa la Baraza kuwa muiwasilishe ripoti ile na iletwe hapa na tuione, ipokelewe ndipo tukubaliane, ndipo tukuidhinishie kwa hiyo kama ipo basi Mhe. Waziri asitikishe kichwa hakuna tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri, ailete ripoti hiyo tukubaliane kama tulivyokubaliana mwaka jana, ili tuwe kumpitishia fedha zake.

Sasa naomba niende kwenye Idara ya Chuo cha Mafunzo *paragraph* 177. Mhe. Mwenyekiti, kwenye idara hii iko afadhali. Kwa mfano, mwaka jana aliomba shilingi milioni 5,890,000,000/= na mwaka huu naona inaombewa shilingi milioni 6,099,000,000/=. Lakini uafadhali huu najua kwa sababu ya ule mradi wake wa ujenzi wa kile Chuo cha Hanyengwa Mchana kule nimeona hapa kuna maelezo mengi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumshauri Mhe. Waziri katika idara hii kuna kitu mara nyingi sana wakati tunapopitisha bajeti huwa hatukiangalii sana. Katika chuo kile huwa tunaona mafungu ya chakula na mambo mengine, lakini kile chuo kile huwa kinalaza wale wafungwa na hatuoni hesabu ya magodoro au vitanda kwa ajili ya wafungwa wale. Kwa kweli hata ukisafiri Mhe. Mwenyekiti, unapewa fedha za chakula na malazi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, zimebakia dakika tano za kumalizia.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante naendelea. Sasa itakapokuwa chuo hichi tunakiidhinishia fedha kwa ajili ya chakula tu, lakini malazi hatuzingatii nafikiri itakuwa hatuwatendei haki. Kwa hivyo, naomba kumshauri Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba alifikirie hili na bajeti yake ya mwakani tukijaaliwa na uhai ikija iwe na fungu linaloonesha kwamba hawa watu huwa wanalala kule, kwa sababu wanakula, lakini kulala pia wanalala na sasa basi tuwatengenezee mazingira ya kupata malazi.

Vile vile kwenye *paragraph* ya 182 kuhusu Kikosi cha Zimamoto na Uokozi. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nitoe pongezi sana kwa kikosi hichi kwa kazi nzuri wanayoifanya na tulikuwa tunawalaumu sana hapo nyuma.

Lakini kwa kweli Mhe. Mwenyekiti kazi ambayo wanayoifanya mimi mwenyewe nimeshaishuhudia mara mbili. Kwa mfano, ilitokezea moto, unapiga simu hata dakika 10 nyingi kikosi kimefika na moto umeanza kuzimwa na ukazimika. Kwa hivyo, kwanza nitoe hongera kwa kikosi hichi, lakini bado naona serikali haijakizingatia vizuri zaidi, kwa sababu zana za

kufanyia ile kazi, kwani ile kazi haifanywi kwa kupulizwa ule moto kwa kutumia mdomo na kama ingekuwa wanapuliza kwa mdomo basi haina tatizo, lakini kuna zana.

Kwa mfano, tukiangalia humu fedha ambazo wanatengewa na kwa ajili ya kwenda kufanya kazi ile, kwa sababu moto hauna taarifa kama kesho utawaka. Mhe. Mwenyekiti, inawezekana humu ndani ukafumuka pande tofauti humu ndani na ikafika wakati hata ile *fire* haiwezi kufika.

Sasa naiomba sana serikali Mhe. Mwenyekiti, katika bajeti zake hizi wakiangalie sana kikosi hichi katika kuwanunulia zana, kwa sababu mwaka jana tulilalamika sana hapa kwamba wanazo zana za upande wa juu tu, lakini sisi tumezungukwa na mazingira ya bahari. Kwa mfano, leo na Mwenyezi Mungu atuepushie mbali inaweza kuja kutokezea boti pale imetoka na kuanza kuwaka moto, hivi itazimika kwa kitu gani, hawana zana hawa na itakuja kuwa tunatizamana na watu wanateketea pale.

Mhe. Mwenyekiti, naiomba sana serikali katika hili ikiangalie kikosi hichi kuhakikisha kwamba wanafanya utaratibu na tunaweza kupata zana kwa ajili ya kuzimia moto na kwa upande wa baharini.

Mhe. Mwenyekiti, pia kwenye *paragraph* ya 188 kwenye Kikosi cha Valantia KVZ. Na hapa ninayo malalamiko. Tukiangalia kwenye fedha mwaka jana waliidhinishiwa milioni 3,784,000,000/=, lakini mwaka huu wameombewa milioni 3,258,000,000/=, yaani kuna karibu 500 nzima imepunguzwa hapa.

Katika hili namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti wakati atakapokuja kufanya majumuisho anipatie maelezo na baada ya hapo akija kunijibu vizuri na kwenye mafungu yangu na tukaondosha ule utata wa shamba la Bambi, basi mimi bajeti yako sina tatizo nayo, lakini kwa sasa hivi nazuia na wala siungi mkono nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Marina Joel Thomas: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi kunipa nafasi hii kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Pili napenda kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na watendaji wake wote kwa kazi nzuri ambayo yanayoifanya. *(Makofi)*

Vile vile niishukuru wizara hii kwa kupitisha Sera ya Serikali za Mitaa, ambayo itajenga misingi ya muundo wa Serikali za Mitaa, pia itasaidia

kurekebisha, kuongeza kasi ya maendeleo kuwafikia wananchi ambao ni walengwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kupitia sera hiyo tunatarajia kutakuwa na mabadiliko mbali mbali ya kisheria, zikiwemo sheria zenyewe za Serikali za Mitaa Sheria Nam. 3 na 4 ya mwaka 1995. Mabadiliko hayo ya kisera na sheria hizo italazimika kufanya mabadiliko ya Sheria Nam. 1 ya mwaka 1998 Sheria ya Mamlaka ya Tawala za Mikoa pamoja na sheria mbali mbali za kisekta, ili kuwezesha utekelezaji wa sera na sheria za Serikali za Mitaa kwa kadri serikali itakavyoona inafaa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mtazamo wangu jambo hili ni zuri na naishauri serikali ifanye haraka katika utekelezaji wake, ili wananchi wapate tija kutokana na ufanisi mzuri wa watendaji watakaokuwepo na wale watakaokuja. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, naishauri serikali Mhe. Mwenyekiti, kupitia Wizara ya Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kuanzia mwaka wa fedha 2014/2015 ni vyema mipango yake ya maendeleo ya serikali ikaanzia chini, yaani *bottom up approach* katika ngazi ya shehia, wilaya hadi mikoa, na kuacha mpango wa sasa ambao unatumia *top down approach*, dhana ambayo kimataifa haionekani kuwa ni dhana yenye afya. *(Makofi)*

Sambamba na hayo ningeshauri serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Serikali kusaidia kulisimamia suala hili kwa dhati kabisa. Mhe. Mwenyekiti, naamini kuwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ana uwezo wa kiutendaji, muono wa kimaendeleo na ana shauku ya kuwaletea wananchi huduma mbali mbali za kijamii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi sana Serikali za Mitaa inapozungumzwa viongozi wengi hasa katika ngazi za utendaji na hasa wa kisekta, wana dhana kuwa utekelezaji wa sera hii ni mgumu. Kwa sababu watendaji wa ngazi za wilaya na mikoa hawana uwezo. Kwa maana nyengine Serikali za Mitaa bado hazijawa na uwezo wa kutekeleza majukumu yanayotarajiwa kupelekwa huko kwa muono wangu na kwa uzoefu nilionao katika Serikali za Wilaya zina uwezo huo.

Hata hivyo, kuna baadhi ya viongozi wa kisekta wana mtazamo kwamba kukiwepo na hii Sera ya Madaraka Mikoani wanahofia kwamba baadhi ya mamlaka na madaraka yao yataondoka. Mhe. Mwenyekiti, ni vyema serikali katika ngazi ya kisekta ikabaki na majukumu yake ya msingi ambayo pamoja na kuandaa sera, kuandaa rasimu mbali mbali, kuandaa sheria na kuandaa miongozo mbali mbali, pamoja na kufuatilia na kutathmini majukumu yao.

Shughuli za utekelezaji ikabaki kwa wananchi wenyewe kupitia Serikali za Mitaa.

Mhe. Mwenyekiti, suala la uratibu wa vikosi maalum, nitazungumzia kuhusu ajira inapatikana katika ukurasa wa 50 ya kitabu cha hotuba ya bajeti. Hapa napenda kumshukuru Waziri kwa jinsi Idara maalum zinazosaidia katika shughuli mbali mbali za ulinzi na usalama wa nchi yetu. Pamoja na shughuli za kijamii zikiwemo za maafa. Kwa kweli hapa vikosi maalum vikiwemo mafunzo, valantia na JKU vinafanya kazi kubwa na nzuri, wanastahiki pongezi.

Mhe. Mwenyekiti, pia nampongeza Waziri kwa kuajiri vijana katika idara hizo jambo ambalo sio tu litapunguza tatizo la ajira kwa vijana bali litaimarisha ulinzi na usalama na amani na utulivu katika nchi yetu. Ingawa sina hakika sana lakini kwa taarifa niliyokuwa nayo suala hili lilitaka kuingia dosari, suala la ajira. Nampongeza Mhe. Waziri kwa kudhibiti hali hiyo na kulifanya suala hilo liende kwa ufanisi kiasi.

Vile vile kwa ninavyoelewa utaratibu wa ajira katika Idara zinazohusiana na ulinzi na usalama, pamoja na kuwepo Tume ya Utumishi za Idara hizo, lakini kutokana na unyeti wa jambo lenyewe shughuli hizi hupaswa kuanzia katika Mkoa, Serikali za Mitaa, Wilaya hadi Shehia. Hivyo napenda kuchukua nafasi hii kumshauri Waziri kuendelea na utaratibu, kwani kwa mujibu wa muundo wa serikali hizi huko ndiko kwenye wananchi. Hakuna kikosi kinachomiliki raia, vikosi vyote vinamiliki askari.

Mhe. Mwenyekiti, nitazungumza suala la mafao ya askari. Nitarudia tena kusema askari wana majukumu makubwa katika nchi yetu. Hii ni moja wapo kulinda amani na utulivu tuliyonayo. Askari watizamwe kimaslahi Mhe. Waziri. Nasikia kuna muundo wa mishahara katika idara hizi maalum. Ushauri wangu nakuomba Mhe. Waziri muundo huo wa mishahara usiwe wameekewa viongozi tu wa idara maalum, bali uwe na kwa maaskari wenyewe kiujumla.

Mhe. Waziri, kuibuka na uvamizi mbali mbali katika mahoteli yetu ya kitalii. Hapa ningemuomba Mhe. Waziri aunde kikundi maalum hata katika hao wenzetu wa kikosi ili waweze kulinda katika hayo mahoteli ya kitalii. Tukiangalia Sekta ya Utalii ni sekta ambayo inaingiza pato jingi katika taifa letu. Ningemshauri aunde kikundi maalum katika vijana wetu hawa ili waweze kulinda katika mahoteli, sekta yetu ya utalii isitetereke.

Mhe. Mwenyekiti, nitazungumzia suala la Kamati ya Maendeleo za Wilaya na Mikoa. Mhe. Waziri Kamati za Maendeleo za Wilaya ya Mikoa RDC na DDC

ina wajumbe mbali mbali, miongoni mwao wajumbe ni sisi Waheshimiwa Wawakilishi. Uzoefu unavyoonesha Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwetu hatuhudhurii vikao hivyo. Moja ya sababu hizo zinazopelekea tusihudhurie ni suala la posho. Posho linavyolipwa katika Kamati hizi za Mikoa na Wilaya hayalingani na maposho ambayo tunalipwa hapa ya Baraza la Wawakilishi. Huu ni wajibu wetu kuhudhuria vikao hivi ili kujadili na kufuatilia shughuli mbali mbali za maendeleo, katika Mikao yetu na Wilaya zetu.

Mhe. Mwenyekiti, niwashauri Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu tuwe mstari wa mbele katika jambo hili kwa manufaa na maslahi ya wananchi wetu tunaowaongoza. Haipendezi kuja Barazani tukatoa baadhi ya hoja au kusema mambo mengi ambayo tungeyajadili katika vikao vya Kamati vya maendeleo vya Mikoa na Wilaya. Na kama tungehudhuria kikamilifu basi hoja hizi tungekuja kwenye Kamati katika Vikao hivi vya Baraza la Wawakilishi kubwa tungeeleza utekelezaji na majanikio ya kazi zetu.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ukurasa wa 41 ambao umeeleza moja ya majukumu ambayo ameeleza Mheshimiwa. Ameeleza kazi zilizotekelezwa na Ofisi ya Mkoa wa Mjini Magharibi ni miongoni mwa kufuatilia kesi za udhalilishaji. Na hapa imeelezwa katika ripoti ni kesi saba tu ambazo zimeelezwa. Ukitizama vyombo vyetu vya habari vinaripoti kila siku kesi za udhalilishaji. Kwa hivyo hapa nilimtaka Mhe. Waziri labda anieleze ni kesi saba tu kwa mwaka mzima ambazo zimeripotiwa katika Mkoa wetu wa Mjini Magharibi.

Jengine nikienda katika ukurasa wa 42 suala la utoro wa wanafunzi. Suala hili limeripotia katika Mkoa wa Kusini Unguja lakini katika Mkoa wa Mjini Magharibi halijaripotiwa. Ukiangalia Mkoa wa Mjini Magharibi kuna maskuli mengi, kuna watoto wengi ambao wanajishughulisha na kazi nyengine ambazo si haki zao kuzifanya. Kwa hivyo hapa nataka Mhe. Waziri anieleze Mkoa wa Mjini Magharibi hakupata fedha kuzifuatilia shughuli hizo. Kama hakupata naomba alifikirie suala hili ili kuwaingizia fedha ili apate kuzifuatilia kesi hizo.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi jioni hii kupata nafasi ya kuweza kutoa machache kuhusu bajeti hii kwa Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuhusu mapato na matumizi ya Ofisi yake.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha jioni hii kusimama hapa katika hali ya uzima kwa uzima wangu. Pia

nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi na nimshukuru Mhe. Waziri na watendaji wake kwa kubuni vitabu vingi kuliko mara zote kwa mwaka huu. Vitabu ambavyo vinaonesha kuwa kwa kima fulani amejiandaa zaidi kuliko miaka miwili iliyopita.

Mhe. Mwenyekiti, nisiwe na dibaji nyingi nianze katika ukurasa wa 3 wa kitabu hiki. Katika utangulizi wake kwenye paragrafu ya 7 inayozungumzia vitendo vya hivi karibuni vya uhalifu ambavyo watu wamemwagiwa tindi kali na wengine kupoteza maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, vitendo hivi ni vibaya na mimi binafsi navilaani. Kwa sababu si vitendo vyema katika nchi. Lakini kuna vitu viwili tofauti vilivyotumika; kumetumika tindi kali, ambayo mtu yoyote anaweza akaiweka pahala akatumia, lakini katika mauaji kumetumika silaha watu wa kawaida katika nchi hii hawaruhusiwi kumiliki silaha isipokuwa kwa kibali maalum.

Mhe. Mwenyekiti, mauaji yaliyofanyika ilitumika silaha, kwa hivyo tutafute ni nani hapa nchini anayemiliki silaha. Hivyo basi kwa njia moja au nyengine ama alipata kwa kibali au waliokuwa nazo kisheria watakuwa wanahusika na mauaji hayo au kuna ujambazi uliotoka nje na kuingia ndani ya nchi. Kwa sababu kama lilivyosomeka swali langu kwamba usimamizi wetu uko wazi sana inaweza ikatoka silaha nje ya nchi na ikafanyika hujuma katika nchi yetu. Kwa hivyo ni lazima ulinzi wetu uimarike ili kuweza kupekuwa yule aliyehusika kutiwa hatiani.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa huu huu wa 3, nije katika Shabaha za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti, Baraza la Mapinduzi kwenye kifungu cha 9 lengo la pili. Kuwafanya vijana wawe na maadili mema na mtazamo wa kujiajiri wenyewe. Kwanza nije katika haya maadili mema. Sijui hapa Zanzibar maadili mema ni yepi? Kila mtu anakwenda kivyakevyake. Sasa mtizamo wa serikali kusema haya ni maadili mema ya kufuata ni yepi? Kwa sababu watoto wetu, wangu na wako, wa kiume wanavaa suruali chupi unaiona, wa kike anatembea kifua mbele hapa kipo wazi; ni mwanangu, ni mwanao na hizo tunawashonea sisi wenyewe.

Tukizungumza maadili mema hapa Zanzibar ni yepi? Je, serikali inayo hiyo dira ya maadili mema? Je, serikali imekusudia kweli kufunza maadili mema? Mliokuwa humu kama hamjazaliwa wakati wa Mzee Karume, yalikuwa yanafunzwa maadili mema, hata wageni wanapokuja ilikuwa ni lazima wafuate Wazanzibari wanavyokwenda. Leo tumejifunza kutii haki za binaadamu. Haya maadili tunayoyazungumza kwa kweli yatabakia katika makaratasi yetu. Kwa sababu sisi wenyewe hatujawa tayari kufundisha

maadili mema kwa vijana wetu. Lakini pia sentensi hii imemalizia kuwa na mtizamo wa kujiajiri wenyewe hao vijana.

Mhe. Mwenyekiti, hakuna vijana ambao wanahangaika kwa kujitafutia ajira kama vijana wa Kizanzibari wakiwa wako ndani ya nchi yao au wakiwa nje ya nchi yao. Wanajituma kutafuta kujiajiri kwa sababu wanajua ajira ni sehemu ya maisha yao. Lakini je, hapa nchini ndani ya Zanzibar yenyewe tunawapa fursa za kujiajiri? Hatuwabugudhi pale ambapo wameamua kujiajiri? Kwa mtazamo wangu mimi serikali iwatengezee vijana mazingira ya kuweza kujiajiri wenyewe. Wengi wao wapo tayari kujiajiri, tunataka wajiajiri lakini hatimaye tunawazungukia kinyume.

Mhe. Mwenyekiti, vitendo ambavyo wanafanyiwa vijana wa Darajani mara nyingi havina mfano mwema katika nchi hii. Kwa kweli kutumia vyombo vyetu, vikosi vyetu kwenda katika makundi ya vijana ambao wamejiajiri hata kama wamehalifu sheria. Hukumu ya hapa Zanzibar mtu anapohalifu sheria ni kupora mali yake na kupigwa bakora? Tuseme kukaa pale wawe wamevunja sheria. Je, hukumu yake watu wavae ninja na bakora na bunduki wakawanyang'anya mali zao. Tunahubiri Utawala Bora, tunahubiri utawala wa Sheria je, hiyo ndiyo hukumu ya kisheria? Je, ule ndio Utawala Bora? Tunasema nini na tunafanya nini?

Mhe. Mwenyekiti, kosa linapotendeka pahala pa kutolewa hukumu papo inakuwaje hivi. Mimi binafsi Mhe. Mwenyekiti, ningelishindwa kuwa askari. Kwa sababu askari nidhamu yao moja kuwa mnyenyekevu vyovyote unavyoambiwa kufanya ufanye. Mimi hili lingenishinda, kwamba kuambiwa nimpige mtu bila kosa, nisingempiga na naona ningefukuzwa kazi. Au mnyang'anye mtu mali yake, nisingemnyang'anya naona hatimaye ningelitiwa adabu mimi ama ningelifungwa na kufukuzwa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, hawa watu wana kazi ngumu, kwa hivyo tuwaelekezeni vizuri. Hawa ni vijana wetu, wasije mitaani wakalaaniwa kwa kuwaambia kwamba fanyeni hivi, kwani mpaka tuwanyang'anye watu mali zao. Nina hakika kama wasingeliambiwa wasingelifanya. Wanafanya wakati mwengine kwa kutii amri ambayo haiwezi kuepukwa, tunasema kwamba wanalinda ugali wao. Hili si jambo zuri wala mimi halinipi faraja kuona leo pako kimya, kesho bakora na kuwanyang'anya watu mali zao ikiwa inaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kidogo katika ukurasa wa 5 kwenye kifungu cha 13 kinachozungumzia kutimia miaka ya 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar. Sheria hizi zinatarajiwa ziwe kubwa pengine kuliko zote zilizotangulia. Kuna hii sentensi karibu ya mwisho huku inayosema kuandaa na kurusha hewani vipindi mbali mbali vya TV na Redio vinavyoeleza mafanikio hadi mwisho

wa hiyo sentensi. Sasa hivi vipindi vya TV na Redio, naomba viandaliwe viwe vya ZBC. Kwa sababu hivi sasa ni vya UBC, wa Pemba hatusikii matangazo yetu ni Unguja *Broadcasting Corporation* sio ZBC. Tukifika miaka hiyo miaka 50 ya Mapinduzi naomba kweli kweli iwe ZBC wala sio UBC kama ilivyo sasa, vyengine itakuwa hatuwafanyii haki wenzetu waliokuwepo Pemba. Watakosa kuona na kufurahia Mapinduzi yao. Tafadhali *change it from UBC to ZBC*.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Mshikamano wa Kimataifa, Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa hapa kuna swali tu. Hawa Wazanzibari waliokuwepo nchi za nje wamechangia kiasi gani katika pato la Taifa hapa pao. Kwa sababu tunawajengea mazingira ya kuwatambua hapa ili waweze kusaidia, katika kipindi hichi wameweza kuchangia kiasi gani katika pato la taifa hapa nchini kwao.

Mhe. Mwenyekiti, nitoke kidogo nije katika Tawala za Mikoa na nielekee katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani. Naangalia kitabu cha pili cha Mhe. Waziri ambacho Wilaya hii kwa mwaka uliomalizika kilikadiria kukusanya milioni 54, wanavyosema wenyewe ni sawa na silimia 51.9.

Nije kwenye matumizi yao sasa, wanasema kwamba wamefanya mikutano na walipa kodi na wadau wengine wa maendeleo wametumia milioni ishirini na sita laki nane na thalathini na saba elfu, mia sita na arubaini na moja. Pesa walizokusanya ni milioni ishirini na nane, kwa hivyo zitumike kwa mikutano milioni ishirini na sita na ushei, je hizo kazi za maendeleo wamefanya kwa pesa zipi. Pesa zote walizozikusanya wamezila kwa mikutano.

Mhe. Mwenyekiti, hapa Waziri itabidi miye si mpiga buti lakini itabidi niridhike kweli kweli nione kuwa pesa hizi zimetumika vipi kwa zote isipokuwa milioni moja *point some thing* ndio iliyotumika kwa ajili ya hizo kazi zao, zote kwa maana ya zote walizokusanya wamezitumia kwa mikutano kama kwenye kitabu chake cha pili, ni jambo la kutisha. Ina maana sisi watu wa Halmashauri ya Mkoani tunawakusanyia watu pesa kwenye mikutano tu.

Mhe. Mwenyekiti, mambo kama haya siku hizi ndiyo yanayosababisha migogoro mwahala mbali mbali. Ukisikia kuwa mwahala fulani watu wamekataa kulipa kodi, kwa mambo kama haya, mnawakusanyia watu pesa matokeo yake ndio kama haya. Huwezi ukakusanya kodi halafu zote ukafanyie mikutano. Kwa mwaka ujao wameomba kama walivyoombwa mwaka jana, lengo ambalo hawakulifikia. Lakini wao wenyewe wanatarajia kupata zile za kufanyia mikutano tu. Kwa sababu mara hii pesa walizopata milioni 28, milioni 26 wamezifanyia mikutano. Mara hii wanaomba zile zile lakini wanataka milioni 26 wafanyie mikutano, ina maana hakuna jengine

watakalofanya isipokuwa ni kufanya mikutano tu. Hatuwatendei haki watu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani, kuwa tumewakusanyia ili watu wa Halmashauri wafanye mikutano tu.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye ukurasa wa 44 hadi 46 kwenye kitabu chako cha bajeti kwenye Mkoa wa Kaskazini Unguja, kwenye malengo ya Mkoa. Sitaki nisome malengo yote lakini moja wapo ni kuimarisha ushiriki wa wananchi katika utawala wa kidemokrasia. Hili ni jambo zuri kuwa Mkoa umekaa na kutafakari kuwa tuwashirikishe wananchi katika Utawala wa kidemokrasia.

Demokrasi ni pana na ina maeneo mengi ina upande wa uchumi, kidini, kisiasa, kibiashara na kadhalika. Watu wakiheshimu shughuli zao hizi hawafanyi japo isipokuwa wanazingatia kutii sheria za nchi ziliopo.

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa huu huu wenye lengo la kuwafanya watu kwenda kidemokrasia wao wanaanza kutaka kuvunja demokrasia. Kuna chama kinakwenda kufanya mikutano tayari wanawekewa ngumu. Hii demokrasia inayozingatiwa hapa iko wapi. Siasa majukwaani kila mwanasiasa anasema anavyotaka iwe havunji sheria. Je, hawa wanaokwenda kufanya mikutano inasema ilikuwa tayari jeshi la polisi limetoa kibali lakini bado kuna wakubwa wengine wameamua kuwa hapana. Kwa nini? Je, ile dhana ya demokrasia iko wapi? Ndio nyuma huku nikasema kwamba tunahubiri tu lakini hatutendi yale tunayoyahubiri!

Mhe. Mwenyekiti, siasa kila mtu ana siasa yake, kila mtu ana maneno yake, kila mtu anamsema mwenzake, ukisemwa na wewe ukifika mkutano ukamseme. Nchi hii ni yetu sote, nchi hii sio ya CCM peke yake, nchi hii sio ya CUF peke yake, nchi hii ni ya Wazanzibari. Kwa hivyo isiwe kuna mtu akajiona kwamba yeye ndiye ana haki zaidi kuliko mwengine. Kwa hili fuateni sera yangu haki sawa kwa wote!

Mhe. Mwenyekiti, nimesikitishwa sana kusikia taarifa hii ambayo inataka kuturudisha kule tulikotoka. Tunatakiwa tutizame tutokapo, tulipo na tunapokwenda. Lakini tukishatizama kule nyuma basi tusirudi tena. Tutizame tunatoka wapi? Tunatoka katika mambo mabaya ya kufarikiana na kugombana. Sasa tukishayatizama tusiyarejee tena, tukiyarejea ina maana bado tunakaribisha mizozo na matatizo katika nchi. Hivyo kweli jamani mpaka leo kuna Wazanzibari ambao wanataka Wazanzibari wagombane? Hivi huyu Mzanzibari aliyekuwa hivi ni kweli huyo ni Mzanzibari huyo, ambaye lengo lake ni kuandaa mazingira ya kuwa watu wagombane.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika vitambulisho vya Uzanzibari.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa jali muda na wengine wanataka kuchangia.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mheshimiwa najali muda sana. Vitambulisho hivi kwa hapo mwanzo ilikuwa ni kwa ajili ya siasa, kama tunakubali kama tutakataa lakini imani yangu mimi iko hivyo. Vilianzishwa mwaka 2000, mimi mwaka 2000 nakwenda kwenye uchaguzi hali ya kuwa watu wa Tume ya Uchaguzi wamekuja na kusema kwamba watu wawe na vitambulisho ndio waandikishwe.

Mimi nilipanga foleni na kwa wakati huo kitambulisho nilichopewa ni hichi. Kabla ya kufika pale kinatolewa unabandikwa unaambiwa nenda ukajiandikishe. Lakini kwa wakati huo kimeandikwa Kiingereza kitupu hakikuandikwa Kiswahili. Lakini kwa mwaka ule na lengo la kukitumia hiki kisiasa yalikwama, wakaachiwa watu wajiandikishe bila ya kutumia kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kutumia kitambulisho kwa Wazanzibari ni kurudi nyuma, kuna jambo nimelisahau kwa sababu mimi kadi ya uraia ninayo ya Mzanzibari ambayo kaisaini Mhe. Said Washoto ni Mzanzibari si mkaazi, sasa mimi niliyekuwa ni mkaazi nimerudishwa nyuma, nyuma ni raia wa Zanzibar wakati wa marehemu Mzee Karume na kadi akasaini Mhe. Said Washoto, leo ninaambiwa ni Mzanzibari Mkaazi, iko siku mtaamua mtatimua niondoke niende wapi! Siondoki!

Karibuni hapa tumepitisha sheria ya kumpa ukaazi mgeni lakini mtoto wa Sipwese yaani kwetu Kengeja, Sheha anamwambia sikutambui lakini mtu aliyetoka Denmark na kwengineko anapewa, sijui sisi tukoje wale wetu kuwatambua hatutaki kwa nini? Kwa hivyo bado kwa mtizamo wangu mimi pamoja na kuwa tunaambiwa kuwa ni cha ukaazi lakini bado mna *political issues* ndani yake. Ni kuwabana watu kuwakosesha haki zao za kiraia ya kupiga kura kwa viongozi wanaowataka. Ninamuomba Mhe. Waziri ahakikishe kuwa kila anayepaswa kuandikishwa kuwa Mzanzibari Mkaazi aandikishwe vyenginevyo *wallahi* tunajitia kitanzi cha roho. Kwa sababu hapa duniani *ok* tutafanya tutakavyo, lakini kuko kwahala hakuna Waziri, kuna Muumba wetu ndio pekee mwenye nguvu mimi na wewe hata tutetemeke hatuna la kujibu.

Tujengeni mazingira ya hapa duniani na huko tunakokwenda na hata tunaamini kwamba tutakuja na hata tutaamini kuwa tutafufuliwa, ni hata kuwa tutaamini kutahesabiwa na hakika tutaamini kwamba ama utaingia peponi Mungu atujaalie hivyo au motoni, lakini yote mawili haya tutakwenda kulingana na vipimo vyetu tulivyovifanya hapa. Tujengeni mazingira ya kututia peponi wala sio motoni.

Siungi mkono hoja hii hadi pale nitapopata ufafanuzi wa mambo mbali mbali hususan yale ya matumizi mabovu ya pesa za Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti na mimi nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia katika hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame.

Mhe. Mwenyekiti mimi kwa kuanzia nitaanzia Idara ya Mawasiliano Ikulu *page* 26 mpaka 27. Mhe. Mwenyekiti naipongeza sana Idara kwa kazi nzuri ambayo inaifanya ya utekelezaji wa majukumu yake ya msingi ya kupokea na kutoa taarifa za Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuhusu utekelezaji wa sera na mipango ya serikali. Mhe. Mwenyekiti wenzetu Bara wana Idara kama hii ambayo inaitwa Kurugenzi ya Mawasiliano Ikulu.

Mhe. Mwenyekiti mimi nina wivu lakini wa maendeleo, naumia sana nikiona kile kipindi ambacho wenzetu wanacho cha *usione vyaelea vimeundwa;* kipindi ambacho kinaonesha yale mambo yote ambayo Mhe. Rais pamoja na serikali yake kwa pamoja wameyafanya. Sasa Mhe. Mwenyekiti wazungu wanasema '*seeing is believing'* kuona ndio kuamini.

Nasikitishwa sana na Idara hii kwamba nimeangalia kiambatanisho hapa ambacho wamesema tuangalie kwa *reference* ya vipindi ambavyo wamekuwa wakirusha katika TV na Radio. Lakini Mhe. Mwenyekiti ukiangalia karibu vipindi vyote ni hotuba tu ya Mhe. Rais na katika uzinduzi na ziara mbali mbali ambazo zimefanywa lakini ni vizuri Idara hii Mhe, Mwenyekiti ingekuwa inatengeneza *documentaries* maalum ambazo zinaonesha kazi ambazo Mhe. Rais amefanya katika sekta mbali mbali, sekta ambazo zinawahudumikia wananchi kwa ujumla kama afya, elimu, miundombinu ikawa wana-*compile* zile kazi na kupeleka katika TV zetu hizi hasa hii ZBC ambayo ndio wananchi wetu wanaangalia kwa sana ili wananchi na wao wakapata nafasi ya kuona ni mambo gani ambayo Mhe. Rais na serikali yake kwa ujumla wamefanya tangu wameingia madarani.

Mhe. Mwenyekiti ZBC hawa hawana vipindi, Idara hii ikifanya hivi itawasaidia ZBC kuwapa vipindi lakini pia itamsaidia Mhe. Rais kwa ujumla kuoneshwa wananchi wake ni kitu ambacho amefanya. Mhe. Mwenyekiti naomba Idara ipanue wigo na ione mbali zaidi ya kutengeneza hizi *documentaries* wapeleke katika TV na Radio ili wananchi ambao hawakupata nafasi ya kuona haya mambo yote waone serikali yao itafanya nini.

Mhe. Mwenyekiti nikitoka Ikulu naomba niingie nyumbani Mkoa wa Kusini Unguja. Mhe. Mwenyekiti nami naupongeza sana uongozi wa Mkoa Kusini Unguja kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya ya kuhakikisha kuwa wananchi wa Mkoa huu wanapata huduma za kijamii ambazo wanastahiki.

Lakini vile vile kwa niaba ya wana Kusini wenzangu Mhe. Mwenyekiti naomba nichukue fursa hii kumshukuru Kaimu Mkuu wa Mkoa ambaye ni Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi kwa kipindi chote ambacho amekaimu kazi za Mkuu wa Mkoa wa Kusini ambaye hali yake ya kiafya ilikuwa si nzuri na *inshaalla* Mungu atamuafu atampa siha na afya njema.

Mhe. Mwenyekiti *mcheza kwao hutunzwa*. Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi kacheza kwao na sisi hatuna budi kumtunza. Kwa hivyo tunashukuru sana. Lakini pia Mhe. Mwenyekiti nichukue nafasi hii kumkaribisha Mhe. Mkuu wa Mkoa mpya wa Kusini Unguja ambaye amekuja ku-*take off* na kuendeleza gurudumu la maendeleo la Mkoa wa Kusini pale wenzake walipoishia.

Mhe. Mwenyekiti nikiingia katika malengo ambayo Mkoa wa Kusini ulijipangia kutekeleza. Naupongeza sana Mkoa wa Kusini kwa hatua iliyochukua juu ya kukabiliana na utoro wa watoto wa skuli. Mhe. Mwenyekiti wazidi kubuni mikakati imara zaidi kuona kwamba tatizo la utoro linakwisha kabisa katika Mkoa wa Kusini, kwani vijana ni tegemeo katika taifa na hivyo vyema tukahakikisha kuwa vijana hawa wanapata elimu ili kuja kuendeleza nchi yetu leo na kesho.

Mhe. Mwenyekiti pamoja na hayo waswahili wanasema kwamba *maradhi yanavyoingia sivyo yanavyotoka*. Kwa sababu tatizo hili lilikuwa ni kubwa katika Mkoa wa Kusini, sijaridhishwa bado na idadi ya wanafunzi ambao wamerejeshwa maskulini. Katika maelezo wamesema kwamba wanafunzi 18 tu wamerudi maskulini tangu waanze kushughulikia hili tatizo. Hivyo naomba Mkoa ufanye kazi ya ziada kuona kwamba tatizo linaisha kabisa wahakikishe watoto hawaendi maskulini *especially* watoto wa kike kwa sababu *at the end* hawana la kufanya wanaishia kwenye ndoa. Mhe. Mwenyekiti Mkoa wa Kusini una historia kubwa kutoa viongozi wakubwa kwa hivyo waone kwamba watoto wanarudi skuli ili tusifute ile historia na tungependa iwe endelevu.

Mhe. Mwenyekiti pia nipongeze Mkoa kwa mchakato wa kuwatambua watoto wanaoishi katika mazingira magumu na hatarishi. Mhe. Mwenyekiti watoto ni taifa la kesho mimi na wewe tunajua zaidi kuliko hawa wengine, tunapowaacha katika mazingira magumu taifa la kesho halitakuwepo na ni

vyema serikali ikawatupia jicho Mhe. Mwenyekiti na niwashukuru Mkoa wa Kusini kuona hilo.

Mhe. Mwenyekiti pia katika maelezo yao Mkoa wa Kusini wamesema kwamba zoezi hili litakuwa endelevu watasaidia watoto wengi na ninaamini wapo zaidi ya 35 ambao wamewasaidia hawajaonesha maeneo gari ambayo wameyafikia kuwasaidia watoto ambao wanaishi katika mazingira ya hatari, lakini mimi naamini yapo maeneo mengi zaidi kuna watoto zaidi ya 35 ambao wanahitaji msaada kwa njia moja au nyengine.

Mhe. Mwenyekiti hivyo niseme kwamba hili zoezi liwe endelevu kweli kwani hali ya watoto ambao wanaishi katika mazingira ya hatari sio nzuri na ni mbinu nzuri ambayo wameibuni, ni vizuri Mikoa mengine ikaiga mfano.

Mhe. Mwenyekiti nikitoka hapo niingie katika halmashauri za Mkoa wa Kusini pamoja na Wilaya ya Kati niipongeze pia kwa kazi nzuri pia wanazozifanya. Halmashauri ya Kusini kidogo mara hii wametu-*dissapoint* kwa sababu malengo ambayo wamejiwekea kufikia hayakufikiwa, lakini pia niwaombe kwamba wasivunjike moyo wao ndio wanaojua vyanzo vyao vya mapato. Kwa hivyo wanapokisia wanajua nini wanakusanya? Hivyo niwaombe kwamba mara nyengine wakileta wawe wamevuka lengo *as well as* Halmashauri ya Kati.

Mhe. Mwenyekiti nikitoka ofisini naingia Chuo cha Mafunzo kidogo kwa sababu mimi kipindi kilichopita nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Katiba na sheria na mpaka hivi sasa naendelea na ujumbe huo. Mhe. Mwenyekiti tumeona Chuo cha Mafunzo kimechukua jitihada mbali mbali za kuhakikisha kwamba haki za binaadamu zinazingatiwa kwa wanafunzi na mahabusu wanaofikishwa hapo. Hatua mbali mbali zimechukuliwa kama suala la mtondoo linazidi kuchukuliwa hatua, bajeti ya mlo imeongezwa na hivyo tunaamini kwamba milo ya wanafunzi imezidi baada ya miwili sasa wamekuwa wanapata mitatu. Tumeona kwamba katika kipindi cha bajeti kilichopita wamefanikiwa kununua magodoro, kwa kweli hali ya magodoro ambayo tuliyakuta kipindi kile tulichokifanya ziara yamekuwa machakavu sana na uraka.

Lakini Mhe. Mwenyekiti kwa ufupi niseme naupongeza Uongozi wa Chuo cha Mafunzo kwa kazi nzuri wanazozifanya. Mhe. Mwenyekiti katika hili nilikuwa nataka ufafanuzi kidogo katika malengo ambayo wamejipangia, lengo namba moja wameeleza wenyewe walivyokusudia lakini hasa pale waliposema kwamba kuwajengea uwezo wanafunzi wanaporudi katika jamii. Nilikuwa najiuliza je kuna *special program* ambayo imeanzishwa kule inawafundisha hawa wanafunzi labda mambo ya ujasiri amali, au nilikuwa

ninajiuliza ni kitu ambacho kinawajengea uwezo wale wanafunzi ili wakitoka kule wakirudi katika jamii wawe na uwezo.

Mhe. Mwenyekiti kipindi kile ambacho tulitembelea vyuo hivi vya mafunzo, kulikuwa kuna malalamiko makubwa sana, na Mhe. Jussa ameligusia hilo kwamba makaazi ya wale au niseme askari wale ambao wanawashughulikia hawa wanafunzi ambao wapo katika hivi vyuo ni duni sana, na ni kweli tumekwenda tumeona hali ni mbaya kiasi kwamba wale wanafunzi wapo katika hali nzuri ya kulala kuliko walimu wao au maaskari wao. Kwa hivyo Mwenyekiti hili nilikuwa nataka kumuuliza Mhe. Waziri kalichukuliaje kwa ujumla. Kwa sababu mara ile tumekwenda tumemkuta mara hii hatujaona sehemu yoyote ambayo labda amelisemea kwamba litachukua hatua au wamefanyaje?

Mhe. Mwenyekiti kwa kumalizia nilikuwa nataka niingie kidogo kwenye miradi ya maendeleo ambako nilikuwa nahitaji ufafanuzi kidogo. Mhe. Mwenyekiti kwa kuanzia naanza na mradi wa uimarishaji nyumba za viongozi na nyumba za serikali. Mhe. Mwenyekiti tumeona kwamba katika bajeti tofauti za wizara tofauti kwamba viongozi wanakodiwa nyumba. Lakini Mhe. Mwenyekiti nimejaribu kuangalia katika mradi huu katika kazi ambazo walizofanya kutekeleza mwaka jana na mwaka huu, sijaona lile jengo la Ikulu ya pale Kibweni, jengo lile ni bovu lakini sijaona sehemu yoyote ambapo labda Mhe. Waziri ana-*plan* ya kulifanyia matengenezo au kulifanyia ukarabati wowote.

Mhe. Mwenyekiti nikiendelea nataka ufafanuzi kidogo katika huu mradi wa kuimarisha mawasiliano Ikulu na hasa ukizingatia kwamba nilipochangia nilisema sasa ipo haja ya Idara hii kuona mbali zaidi kuliko zile hotuba tu ambazo wanatuletea ili kuona na hotuba zenyewe miezi miwili inaoneshwa hotuba hiyo hiyo. Kwa hivyo nilikuwa nawaomba hapa wamesema mwaka jana mwaka 2012/2013 wamesema kwamba hatua za awali za ukarabati wa chumba cha kutayarishia vipindi katika Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi zimeanza.

Baada ya kusoma hapo Mhe. Mwenyekiti nilijua katika mwaka 2013/2014 kitakachoendelea kwamba mradi huu utaendelea hatua ya pili lakini nimekuta kwamba katika mwaka huu wamepanga kwa ajili ya huduma za Rais Pemba na ununuzi wa vifaa vya matangazo. Sasa sijui huu ununuzi wa vifaa vya matangazo ni *phase* 11 ya huu mradi wa ukarabati wa chumba cha kutayarishia vipindi au vipi nilikuwa ninamuomba Mhe. Waziri akija anipatie maelezo.

Lakini pia nikiingia katika mradi wa nne mradi wa ujenzi wa Chuo cha Mafunzo Mhe. Mwenyekiti sote tulifurahia tulivyosikia kwamba kuna mradi mpya wa Chuo cha Mafunzo ambacho kinataka kujengwa chuo cha kisasa na hasa tukizingatia kwamba kulikuwa kuna kilio kikubwa cha watoto wadogo kuchanganywa na watu wazima katika vyuo vyetu vya Mafunzo.

Mhe. Mwenyekiti lakini nikiangalia katika mradi huu kwa kweli uingizaji wa pesa hauridhishi. Hauridhishi na sina hakika kama serikali hii itatoka madarakani chuo hichi kitakuwa kishamalizika. Hivyo nilikuwa ninamuomba Mhe. Waziri aje atwambie kwamba tatizo ni nini kwamba huu mradi uingizaji wake wa pesa ni kidogo sana yaani unasuasua.

Mhe. Mwenyekiti baada ya kusema hayo naunga mkono hoja na nitaunga mkono zaidi Mhe. Waziri akija kunipatia maelezo. Mhe. Mwenyekiti ninakushukuru.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti nachukua nafasi hii kwanza kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai, uzima na muda huu kuweza kufika hapa kutoa mchango wetu japo kwa ufupi kutokana na muda ambavyo umejipanga.

Mhe. Mwenyekiti kwanza kabisa nimpongeze sana Mhe. Waziri na timu yake kwa jinsi walivyotuletea bajeti mwanana, nzuri iliyofuatana na vitabu vinne au vitano. Ni Waziri pekee aliyetuletea vitabu vingi sana kuliko mawaziri waliopita watatu.

Mhe. Mwenyekiti kwa jinsi Mhe. Waziri alivyotuletea vitabu vitano basi ninaashiria kwamba labda bajeti yake nzuri sana. Sasa kwa msingi huo Mhe. Mwenyekiti naomba nitoe mchango kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti kwanza kabisa nianze na kitabu cha tatu ambacho Mhe. Waziri ametupatia kama ni utekelezaji wa maagizo ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ametuonesha kwamba alipokea maagizo yapatayo 78 na ameyaandika kwenye kitabu maalum ili Wajumbe waangalie jinsi ambavyo maagizo yale yametekelezwa na Wizara yake. Sasa nimejaribu kuyapitia maelezo yale 78 naomba nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuorodhesha maagizo ya Baraza. Ni Waziri pekee ambaye amekuja na maagizo ya Baraza ya mwaka jana ili tuyaone jinsi alivyotekeleza. Sasa kama ametekeleza ni suala jengine lakini angalau amekuja nayo. Nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani kumpongeza Mhe. Waziri kwa kuamua kutufanyia haki yale maagizo yetu.

Lakini nimechagua maagizo kama 5, sasa naomba Mhe. Waziri nichangie angalau maagizo matano jinsi ambavyo Mhe. Waziri ameyatekeleza. Je ni kweli ameyatekeleza au ile ile *business as usual* ambayo tumeizoea?

Mhe. Mwenyekiti nianze na agizo namba 8 ukurasa wa nne wa kitabu cha maagizo. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri anatwambia hoja ilikuwa ni kwamba kunyimwa vitambulisho wakaazi na kupewa raia wa kigeni. Utekelezaji Mhe. Waziri anasema takwimu zimethibitisha kwamba wakaazi hawanyimwi vitambulisho na maelezo tatizo wananchi wenyewe hawaendi kuchukua vitambulisho.

Mhe. Mwenyekiti kwa heshima kubwa na taadhima mimi nakataa kwamba haya sio sahihi, sio sahihi kwamba vitambulisho hawapewi wageni. Tunaendelea kufanya utafiti wa kina na tunagundua wageni wanapata vitambusho, tumeyasema hayo mwaka jana na mara hii tunaambiwa Waziri baadhi ya wageni wanapata vitambusho. Na si sahihi kwamba wazawa kwa maana Wazanzibari halisi wanakataa hivyo vitambulisho.

Mhe. Mwenyekiti Waziri amefanya ziara Pemba na pia nimpongeze tumemwambia waziwazi katika Wilaya zetu kwamba kuna wananchi wazaliwa wa majimbo yetu wamekuwa wakinyimwa vitambulisho kwa msingi wa kisiasa. Sasa Mhe. Waziri akiandika ripoti hii na hili ni andiko limetokea kwenye kumbukumbu kwa kweli inakuwa si sura nzuri. Mhe. Mwenyekiti wananchi hawapati vitambulisho na Mhe. Waziri hili analijua. Ningemuomba Mhe. Waziri kwa sababu ya busara alizonazo asiendelee hili kulizungumza kama nadharia ningemuomba achukue hatua kama Waziri alipewa jukumu kwa niaba ya Mhe. Rais kuendesha Wizara yake aliyokabidhiwa.

Mhe. Mwenyekiti hakuna haja ya utafiti Wazanzibari majimbo yote 50 ya Zanzibar wanabaguliwa kwa msingi huo wa vitambusho wengine hawapewi vitambulisho. Akitangaza Mhe. Waziri leo hapa kwamba wananchi wakusanyike katika mkutano wa hadhara basi atapata wananchi wengi ambao hawana vitambulisho. Hata wale ambao wengine wana vyeti vya kuzaliwa na wana risiti ambazo walipewa wenyewe kwenye vitambulisho. Mhe. Mwenyekiti si sura nzuri ya viongozi wa serikali kuendelea kuwafanya kama Wazanzibari hawaoni.Wazanzibari hawana taarifa na kwamba hili jambo lisiachiwe kiasi hicho. Mhe. Mwenyekiti ningelimuomba Mhe. Waziri azingatie hilo.

Agizo jengine ambalo nimeona lina mapungufu ni agizo namba 15 linasema hatma ya kesi ya wageni waliokamatwa, Mhe. Waziri anasema tangu 2007 Ofisi imekuwa ikipata shutma ya kuwasajili wageni. Ofisi ilifanya jitihada

kubwa ya kufanya uchunguzi wa awali juu ya washukiwa wageni na hatimaye kuwasilisha tu taarifa zao katika Ofisi ya Uhamiaji. Ofisi ilipata majibu kwamba sio watanzania hatua za kisheria zitachukuliwa.

Mhe. Mwenyekiti nakumbuka mwaka jana na mwaka juzi Baraza hili limetajwa majina ya watu waliopewa vitambulisho vya wageni, mmoja Mhe. Mshimba alitoa hadharani kwa ushahidi kwamba kuna wageni huwa wanapewa vitambulisho. Sasa mimi Mhe. Waziri mimi nilitegemea angetwambia wangapi wanapelekwa mahkama au wangapi wamenyang'anywa vitambulisho. Kwa hivyo Mhe. Waziri anatwambia wanafanya utafiti, wakati utafiti umefanywa humu Barazani wametajwa majina watu Barazani. Mhe. Mwenyekiti na vielelezo vipo na akitaka sisi tuko tayari kumsaidia. Bado vielelezo vipo kwa majina nchi wanazotoka zipo, sasa nadhani ni kuchukua hatua sasa Mhe. Waziri akisema kwamba anafanya utafiti sio, utafiti huo unahitaji muda gani ili kuukamilisha?

Mhe. Mwenyekiti agizo jengine ambalo sikulipenda utekelezaji wake ni agizo nambari 28 uzururaji wa wanyama ovyo katika Manispaa ya Zanzibar. Kwamba Baraza la Manispaa kwa kushirikina na *operation* rejesha nidhamu iliyosimamiwa na Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi na hadi sasa *operation* imekamata ng'ombe 68 na mbuzi 58 na punda 7.

Mhe. Mwenyekiti mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani nimpongeze sana Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi kwa kusimamia *operation* hii. Mimi kama Mwakilishi ninaunga mkono juhudi ya kuwaondosha ng'ombe mjini lakini angetwambia sasa mbali ya kuambiwa wale waliokamatwa wako wapi lakini zipo taarifa kwamba wengine wamepotea, wengine wamekufa wengine wamechinjwa. Hebu atwambie Mhe. Waziri kweli wengine wamechinjwa na kama wengine hawajachinjwa ni wananchi wangapi ambao wamekwenda kuchukua ng'ombe wao kwa kutoa fidia. Asilete hivi ilivyo alete sura nzuri.

Mhe. Mwenyekiti agizo jengine ni agizo nambari 57 linalosema kuhakikisha suala la upatikanaji vitambulisho Wazanzibari kwa kila raia kwamba Mzanzibari ambaye ana haki ya kupatiwa vitambulisho. Mhe. Mwenyekiti narejea kusema tena kwamba wazanzibari wapo wana sifa kamili. Jana Mhe. Omar amenionesha orodha ambayo amempelekea Waziri lakini sijui kwa nini hataki kuchukua hatua. Mhe. Waziri mimi nikuombe kwa busara zako kuchukua hatua, ukijua kwamba uongozi ni dhamana na kila mtu ataulizwa mbele ya Mungu vipi amesimamia majukumu yake.

Mhe. Mwenyekiti agizo jengine ambalo ningelichangia vipi ambavyo Mhe. Waziri amechukua hatua ni agizo nambari 28 la kuondosha vizuizi. Mhe.

Waziri anatwambia kwamba agizo nambari 24 samahani kwamba usumbufu unaosababishwa na Masheha katika kutoa huduma kwa jamii. Mhe. Mwenyekiti hili halitaki utafiti, masheha wanaendelea kutuletea usumbufu, tena si kwa bahati mbaya, kwa makusudi wamekuwa wakikaidi hata maagizo ya viongozi wakubwa wa serikali pale ambapo maagizo hayo yanatolewa.

Na mimi nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani kumuomba sana Mkuu wa Wilaya ya Mkoani angalau kwa kuwashtua masheha wake wa Wilaya juu ya maagizo ambayo Waziri ameyatoa na Mkuu wa Wilaya ameyatoa nichukue nafasi hii kumpongeza.

Mhe. Mwenyekiti baada ya kupitia maagizo hayo sasa niseme kwa jumla kwamba kwa haraka haraka nikazuie vifungu ambavyo vina mashaka ya matumizi kwa kila Idara ambayo Mhe. Waziri ametuomba fedha ili nipate ufafanuzi. Naomba niseme hilo kwa jumla ili nisipoteze muda kuchambua moja moja.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti nilipongeze sana Baraza la Manispaa kwa kusimamia mradi wa kuweka taa mpya. Mhe. Mwenyekiti mradi huu wa taa mpya unaashiria kwamba utaleta ufanisi mkubwa. Sasa mimi nimuombe tu Mhe. Waziri kupitia Mkurugenzi wake wa Manispaa basi ajipange kwa kuwasomesha vijana wake taaluma ile ya ufundi wa *solar power* ili wakiondoka wale wafadhili wajenzi kwa maana Wachina iwe rahisi vijana wetu kurekebisha makosa yale ambayo yametokezea.

Mhe. Mwenyekiti nizungumzie pia suala ambalo wenzangu wamezungumza la Wakuu wa Mikoa kujiingiza katika shughuli za kisiasa.

Mhe. Mwenyekiti nakumbuka 2010 Baraza hili liliweka azimio maalum la kuwatoa Wakuu wa Mikoa katika shughuli za kisiasa, na tukasema sasa tunataka Wakuu wa Mikoa ambao watakuwa watendaji kuepukana na shughuli za kisiasa. Sasa mimi nashangaa sana kuona kwamba sasa Wakuu wa Mikoa baadhi yao wanaendelea kujishughulisha na shughuli za kisiasa. Unapofanya mambo ya kisiasa katika Mkoa wako ni dhahiri unakusudia kusababisha vurugu, na mimi niombe sana kwa Mkoa sisi tunawapenda sana, tunaamini kwamba wana wajibu mkubwa wasidiriki kusikiliza mashindikizo ya kisiasa wakaharibu siasa zao. Nadhani ingebakia katika mstari kwamba wao ni Wakuu wa Mikoa; watendaji wanaomuwakilisha Rais katika Mikoa yao mitano.

Mhe. Mwenyekiti kwa msingi huo ningeomba niseme kwamba si sura nzuri leo mkutano wa chama kikubwa Zanzibar kuzuiliwa kwa sababu ambazo hazina msingi. Ningeomba kwa busara ya Waziri, kwa busara ya serikali na

hasa kwa vile juzi Mhe. Balozi kupitia hotuba yake ya ufungaji wa Wizara yake alituomba kwamba tusijaribu kutafuta vishawishi vya kusababisha vurugu. Ninamuomba sana Mhe. Waziri hili alizingatie na mimi nimwambie tu kwamba *Hansard* ya Balozi Seif Ali Iddi ambaye ni Makamu wa Pili wa Rais ipo aipitie jinsi ambavyo aliagiza watendaji wa serikali, Mawaziri na Wawakilishi jinsi ya kujenga demokrasia katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti sasa nitoke hapo niende moja kwa moja kwa vikosi. Mhe. Mwenyekiti niunge mkono kabisa hoja ya Mhe. Jussa kwamba vikosi vyote vya SMZ vinafanya kazi nzuri.

Ukiangalia vikosi unaona kwamba wao wenyewe wako katika kufanya kazi nzuri, lakini kwa nini wanaharibu, ukifanya utafiti utaona wanaharibu kwa sababu kuna mashindikizo ya watu binafsi. Mhe. Mwenyekiti, sikubaliani kabisa kabisa na maslahi ambayo vikosi vyetu wanalipwa, nimefanya utafiti nimegudua kwamba baadhi ya maslahi ya Vikosi vya *KMKM*, Magereza, Zimamoto na wengine, maslahi ya vikosi vyetu sio sahihi, vikosi vyetu tunavipa pesa ambazo hazistahiki kupewa askari wa nchi yoyote, na hiyo labda ndio maana unapoambiwa ukafanye kazi Darajani kuzuia uhalifu wa vijana wanaopanga barabarani sasa wakatumia na wakadiriki kunyang'anya mali za wafanyabiashara wadogo wadogo, na hilo lote linafanywa kwa sababu hali yao ya maisha ni ngumu. *SMZ* inakuwa haipendi vikosi, wanapenda vikosi kwa nadharia tu, wanapenda vikosi kwa njia mbili kubwa, njia ya kwanza vikosi vinapendwa kwa ajili ya uchaguzi, njia ya pili SMZ inawapenda vikosi kwa kuwaambia fanyeni hili pahali fulani, lakini kwenye maslahi *SMZ* haina habari ya vikosi.

Mhe. Mwenyekiti, ninazo *voucher* hapa, nimeona kwamba askari Magereza ambaye amepewa jukumu la kulinda Gereza Hanyegwa Mchana ameekewa posho la shilingi elfu moja na mia tano kwa mwezi, atoke mjini aende Hanyegwa Mchana Chwaka alinde Gereza. Maana yake nini? Maana yake kwa siku askari yule analipwa shilingi hamsini za Tanzania ndio nauli ya dala dala, hiyo sio haki ni lazima tuwapende vikosi vyetu, tuwape pesa kwa sababu wapate maslahi mazuri, leo wanafanya makosa kwa sababu ya dhiki waliyonayo. Baada ya kuchunguza nimeona kwamba kwa nini Wizara hii ndiyo Wizara inayoongozwa kwa fungu kubwa la fedha lakini maslahi ya vikosi ni madogo mno.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia ripoti ya *CAG*, ukurasa wa 97 mwaka 2010/11, ukurasa wa 97 na 98 ripoti imeeleza wazi naomba ninukuu Mhe. Mwenyekiti.

"Kwamba orodha ya wastaafu wa KMKM ambao wamestaafu mwezi wa Disemba 2011 lakini mishahara yao hadi Machi inaendelea kupelekwa vikosini"

Mhe. Mwenyekiti, hiyo inaonesha dhahiri kwamba tatizo la matumizi mabaya ya fedha ambazo vikosi vyenyewe haziwafikii, sasa Mhe. Waziri, atuambie fedha hizi zinamfika nani, kama haziwafiki vikosi mfanyakazi wa kawaida fedha hizi zinamfika nani?

Mhe. Mwenyekiti, fedha ambazo tumeidhinisha ni fedha nyingi lakini kwa nini askari wetu wanalipwa mshahara mdogo na kwa nini wakitumwa wasifanye fujo, nani anafanya kazi na njaa? Kwa hivyo inawezekana mambo yanayofanywa Darajani pale kunyang'anya watu ni kwa sababu ya dhiki waliyonayo, haiwezekani 140,000/= ambayo wanayolipwa halafu atumie mwezi mzima. Mhe. Mwenyekiti, 140,000/= kwa mwezi ni chini ya 5,000/= kwa siku, ni nani humu anayetumia 5,000/= kwa siku akaridhika. Kwa hivyo ukiangalia na fungu ambalo tunalitenga hapa la kila mwaka mabilioni ya fedha na idadi ya askari wetu tulionao kwa nini wapewe 140,000/=, nahitaji ufafanuzi wa kina kwa nini Askari wetu wapewe fedha ndogo wakati wanafanya kazi kubwa, na hasa ukiona kwamba kuna viashiria vya upotevu wa fedha za umma kupitia viinua mgongo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilifanya utafiti mdogo naomba nisome hii barua lakini sisemi nisemee kikosi gani ni barua halali kabisa muone jinsi ambavyo vikosi vinaingiziwa fedha na kuvuja fedha bila ya kuwafika walengwa na Askari wetu wadogo wadogo. Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima naomba uhusike barua hii kama inavyosema hapo juu.

"Watajwa hapo chini walikuwa ni Maafisa wa Jeshi ambao wamestaafu kwa kufikia umri wa juu na wawili wamefariki dunia, hivyo kwa kanuni za Tume ya Utumishi ya Idara Maalum ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wahusika wanastahiki kupata viinua mgongo".

Mhe. Mwenyekiti, nimefanya utafiti hakuna aliyefariki wala hakuna aliyestaafu, kwa hiyo kwa nini tutenge wanachukua watu wachache sskari wadogo wale njaa. Utafiti huu na ripoti ya *CAG* ni vitu sambamba, lazima tuambiwe kwa nini Askari wetu wanapata maslahi madogo, ikiwa mtu hajafariki tayari watu wanafanya kiinua mgongo, maana yake akifariki huyo au akistaafu haki yake itakuwa haipo, ikiwa fedha za Mhe. Jussa tayari zimeliwa leo akistaafu hakuna fedha tena. Sasa nimuombe Mhe. Waziri, atuambie na ukimgusa Mhe. Waziri, anakwambia kwamba vikosi ni siri, mimi nasema hakuna siri ya takwimu na Jeshi, siri katika Jeshi ni *technical* issues na mikakati. Juzi hapa *IGP* Mwema ametwambia wana lengo la kutumiza

Jeshi elfu sitini kwa mwaka 2020 sio elfu mbili takwimu, lakini Mhe. Waziri, ukimwambia tupe takwimu ya vikosi atakwambia maana yake ni siri, siri ya Jeshi si idadi ya Jeshi, mikakati na mambo ya *technical issues*. Naomba Mhe. Waziri, utuambie fedha ambayo inatengwa kwa ajili ya mshahara kwa nini haiwafikii walengwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nashukuru sana Makamanda wa Vikosi vya *SMZ* nimewaomba utafiti mdogo ni utafiti wa Barazani kama haki ya Mjumbe, Baraza la Wawakilishi wanipatie vijana waliofanya utafiti vikosi vyote 5 Zanzibar, wamenileta ripoti ya utafiti kwamba kwa nini vikosi vyetu haviko kwenye mfuko wa Ustawi wa Jamii *ZSSF*, sasa wameshindwa kuwahifadhi Askari wetu kwa kisingizio cha siri ya Jeshi, hakuna siri ya Jeshi wakati huu. Marekani wanatuambia wana Jeshi laki tatu laki nne iwe Zanzibar.

Kwa hivyo tuambieni tujue nini? Tatizo inaelekea kuna watu wanatumia udhaifu wa siri kuzichukua fedha za umma na kuwaonea Askari wetu maskini za Mungu. Mhe. Mwenyekiti, nina hakika Mhe. Waziri, atanambia lini ametembelea Askari wake wa Magereza, lini ametembelea Mafunzo na KMKM, lini ametembelea Zimamoto nina hakika siku haijui. Kwa hivyo anasema ni siri ya Jeshi, siri ya Jeshi sio takwimu ya Jeshi, siri ya Jeshi ni mambo ya kiufundi na hayo Wawakilishi hatutaki tuambiwe, lakini idadi ya Askari wetu na mshahara tuambiwe ili tuwalinde Askari wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nimeambiwa baadhi ya vikosi hutoa mbuzi, vikosi wanatoa mbuzi kuwapa wakubwa wale na mimi nikafanya utafiti nikagundua kuna mkubwa aliyetaka kula mbuzi kama mwanga nikasema Barazani kwamba watu wanakula mbuzi. Mhe. Mwenyekiti, acheni kuwapenda vikosi kijuu kijuu, vikosi wapendeni kwa dhati kwa kuwapa maslahi mazuri ili wakiharibu tuwalaumu, leo wengine wanakufa na njaa hawa, ukiwaambia mkamate Jussa, wanamkamata, kofia wanaiba, simu wanaiba ni njaa! Kwa hivyo wapeni maslahi ili tukiwatuma tuwaamini kwamba hawa vikosi ni halali.

Mhe. Mwenyekiti, tangu juzi Serikali inafanya operesheni pale Darajani na kuwakamata vijana waliokiuka maadili ya Serikali ya kupanga vitu chini, pengine nia ni nzuri ya Serikali. Sasa mimi nimefanya utafiti nimegundua vijana 320 mali zao zimechukuliwa. Mhe. Waziri, nambie mali zile zilizochulikuwa zipo katika ghala gani, katuoneshe vitambaa, viatu, kanzu zipo katika ghala gani la Serikali. Ninavyojua mimi kwamba mali ukikamata peleka Mahakamani mtu aweze kujitetea. Sasa Mhe. Waziri, utuambie mali hii ya madira na vitambaa ipo katika ghala gani ya Serikali ili tujiridhishe kwamba mmechukua kwa nia safi kwa ajili ya kuchukua hatua. Mhe. Mwenyekiti, ukichunguza mali hii utagundua nyengine imepotea kwa sababu askari wetu ni wanyonge.

Mhe. Mwenyekiti, leo nilikuwa Langoni asubuhi nimefanya utafiti. Mhe. Waziri, anatuambia kwamba Askari wanapata mlo, mlo mzuri tu. Nimeenda Langoni mwenyewe asubuhi, wanapewa boflo moja na chai, bolfo la 150/- la pale Mikunguni na usiku boflo moja na chai tayari 300/= hizo na mchana ubwabwa na harage ndio basi, hayo niliyoyaona. Sasa kama askari kama anakula boflo 2 kwa siku mfungwa ale nini si atakula dongo? Mhe. Mwenyekiti, lazima bajeti ya chakula ya Askari tuambiwe ni shilingi ngapi kwa siku ili tuwalinde Askari wetu wasidhalilike baadae na wao wakaingia kwenye makundi ya watu wakadhalilisha watu.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa kuwakumbusha wenzangu kwamba kulikuwa na Serikali ya Kusadikika duniani. Kusadikika ni Serikali moja mbaya sana, ilikuwa ni Serikali moja ya kidikteta, maana viongozi wake majina yake yalikuwa mabaya mno na ninaamini kwamba kumbe jina si ndege, unaweza ukawa na jina baya lakini matendo yako matamu sana, na unaweza ukawa na jina zuri sana lakini ukawa na matendo mabaya sana katika dunia.

Mhe. Mwenyekiti, Kusadikika Waziri Mkuu wake alikuwa anaitwa Majivuno, Mudiri wa Sheria alikuwa akiitwa Utamaduni, Waziri wa Ulinzi wa Kusadikika alikuwa anaitwa Fujo, na Waziri wa Fedha alikuwa anaitwa Komeni ni majina mabaya sana, tofauti na sisi tuna Alhaji Abubakar, Alhaji Dkt. Mwinyi, majina mazuri tu. Kwa hivyo akili ya kawaida utategemea haya majina ya Majivuno, Komeni, Majigambo kwamba yangekosa watu, na siku moja ikatokezea kuna Mzee Karama kwa sababu ya udikteta wa Serikali aliamua kuanzisha skuli ya wanasheria, skuli ile Serikali ikamkamata, lakini pamoja na kumkamata huyo walimpa fursa ya kujitetea Mahakamani na hatimae hoja yake ikashinda. Karama akaachiliwa akawa raia mwema.

Leo kwa nini vijana wetu wa Darajani hamuwapi nafasi ya kujitetea, kwa nini Majivuno na wenzake walimpa Karama nafasi ya kujitetea lakini majina mazuri ya watu hapa hawampi nafasi vijana wetu wakajitetea, kwa nini wanapanga biashara zao chini, ni umasikini tu si jengine, si ubabe, si ukorofi ni umasikini wa vijana wetu. Sasa hili ningelimuomba Mhe. Waziri, kwa busara kubwa sana, ni Waziri mzoefu, una uwezo mkubwa hebu tumia busara ili vijana wetu watulie wafanye biashara zao kwa usalama sambamba na kufuata maadili ya Serikali yaliyo halali.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya mchango wangu huo kama Mhe. Waziri, atanitosheleza kwa maslahi ya Askari wetu pamoja na kunionesha vitu vilivyochukuliwa viko katika ghala gani nitaunga mkono bajeti hii, kama sikuridhika na hayo nitakataa fungu lote la mshahara wake Mhe. Waziri, Ahsante.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kunipa nafasi hii nakushukuru ili na mimi nipate kuchangia mawili matatu juu ya ofisi hii muhimu, Ofisi ya Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwanza nianze kwa kumshukuru na kumpogeza sana Dkt. Ali Mohammed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuisimamia nchi hii na tukawa katika hali ya amani na utulivu na amani na utulivu ndio tunu ya taifa hili. Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuweza kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa vitendo, kwa kweli tuna imani kubwa sana juu ya uongozi wake na kwa sababu tumeshuhudia maendeleo makubwa sana katika nchi hii, katika sekta mbali mbali ikiwemo ya elimu, afya, miundo mbinu na mambo kadhaa wa kadhaa. Kwa hivyo hatuna budi kumshukuru na kumpongeza sana kwa juhudi zake hizi anazozichukua.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuanza mchango wangu niwasilishe kwa Mhe. Waziri, kilio cha wananchi wanaotumia hospitali ya Al-Rahma, na inabidi niwasilishe kwako Mhe. Waziri, ili baadae utoe ufafanuzi na wananchi wakusikie. Hospitali ya Al-Rahma iko barabarani na viongozi wetu wakuu wanaitumia sana barabara ile na wanapopita pale basi ving'ora huwa vinalia mtawalia vinapishana, kwa hivyo wamekuwa wakipata usumbufu mkubwa sana kwa sababu kama tunavyojua hospitali ile pale panafanyika *operation* panafanyika kila jambo ambalo linastahiki utulivu wa hali ya juu kama ilivyo Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kwa hivyo wanaomba sana viongozi wetu wakuu hawa wanapopita pale basi ving'ora vile vizimwe kama vinavyozimwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, ili wapate utulivu katika hospitali ile.

Mhe. Mwenyekiti, mimi si mtaalamu wa masuala hayo, sijui athari yake vikizimwa, sijui faida yake vikiwashwa, sasa nadhani utakapokuja kutoa ufafanuzi wananchi watakusikia huko, mimi ujumbe huu umefika na Mjumbe hauwawi. Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuwasilisha ujumbe huo nije sasa katika Idara au Ofisi ya Usajili wa kadi na vitambulisho vya Mzanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, hapa ametueleza kwenye ukurasa wa 32 kwamba Ofisi ya Usajili wa Kadi na vitambulisho imefanya usajili wa Wazanzibari wakaazi 26,594/= waliotimiza masharti ya usajili ikiwa ni ongezeko la asilimia 151 ikilinganishwa na idadi ya Wazanzibari wakazi 10,574 waliosajiliwa katika mwaka uliopita 2011/12. Aidha Ofisi imetengeneza vitambulisho 18,532 vilivyomaliza muda wake kwa matumizi na imetengeneza vitambulisho 5,178 kwa wananchi waliopoteza na walioomba kufanya marekebisho ya taarifa zao halali binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niwapongeze sana wenzetu wa Idara ya Vitambulisho, wanafanya kazi nzuri na takwimu hizi zinaonesha kwamba wanafanya kazi vizuri na Baraza hili inafaa kuwapongeza. Lakini Mhe. Mwenyekiti, changa moto katika ufanyaji wa kazi haziachi lazima ofisi ile itakuwa na changamoto chungu nzima au mbali mbali, na juhudi tunaiona wanavyokabiliana nazo changamoto hizo.

Mhe. Mwenyekiti, juzi Mhe. Waziri, alijaribu kutuita sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kupitia Wilaya mbali mbali na juzi ilikuwa zamu ya Wilaya ya Mjini aliwaita Masheha, akatuita na sisi Wawakilishi, Waheshimiwa Madiwani na yule Mkurugenzi aliyetambulishwa pale alikuwepo kwa ajili ya kutoa taarifa juu ya maendeleo ya utoaji wa vitambulisho baada ya kusikia malalamiko ya hapa na pale. Kwa kweli ametoa taarifa iliyokuwa ni nzuri na kwa kweli tunastahiki kumpongeza na tunamtaka aendelee na juhudi hiyo, na sisi Waheshimiwa Wajumbe turidhike kwa kazi inayofanywa na Mkurugenzi wa Vitambulisho.

Mhe. Mwenyekiti, tunasema vitambulisho vinatengenezwa, lakini vitambulisho baada ya kutengenezwa wahusika hawaendi kuvichukua katika ofisi za Wilaya. Juzi Mhe. Waziri, Mkuu wa Idara ya Vitambulisho anatupa taarifa katika Wilaya yetu ya Mjini. Katika Ofisi ya Wilaya kuna vitambulisho ishirini na tatu elfu na ushei vimetengenezwa havijaenda kuchukuliwa. Sasa tunaposema kwamba Mkurugenzi hawapi watu vitambulisho sisi tunashangaa hivi vitambulisho vilivyokuwepo pale hivi ni vya nani? Vimetokea wapi? Vimetokea mbinguni? Ni dhahiri kwamba vitambulisho vinatolewa lakini watu hawataki kwenda kuchukua ili wapate nafasi ya kulalamika, jamani hili suala la kulalamika halitusaidii. Juzi juzi tu ofisi ya Vitambulisho imeteketeza vitambulisho chungu nzima ambavyo vilikuwa vimemaliza muda wake, vitambulisho 29,000 vimeteketezwa, vile vitambulisho vimetengenezwa kwa kodi za wananchi. Kodi za wananchi ndio zinazotumika na ndio vile tunavyozungumzia sisi hapa, vimeteketezwa, vimetengenezwa watu hawakwenda kuchukua, sasa tusilalamike tuwapongeze wenzetu wanajitahidi.

Kitu kinachotakiwa ni kufuata taratibu za kisheria ziliopo, unapohama na unapokwenda sehemu nyengine unatoa taarifa kwa Sheha, unakuja na barua, unakuwa na cheti cha kuzaliwa na unatakiwa uwe umeishi mfululizo katika eneo hilo kwa muda wa miaka 3 ili upate uhalali wa kujiandikisha. Sasa hii kulalamika kila siku itakuwa haitusaidii na takwimu hizo zinatolewa na mwisho tutakuja kuonekana Waheshimiwa Wawakilishi kazi yetu kulalamika.

Mhe. Mwenyekiti, mimi natumia nafasi hii kumpongeza sana Mkurugenzi wa Vitambulisho na nimuombe aendelee kufuata taratibu za sheria, asiyestahiki

kupewa kitambulisho asipewe kitambulisho, anayestahiki kupewa kitambulisho apewe kitambulisho ndio utaratibu ulivyo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije kwenye Mamlaka ya Serikali za Mikoa. Mimi nawapongeza sana Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya na Halmashauri. Wakuu wa Mikoa wanafanya kazi vizuri na wana majukumu makubwa. Tukimpongeza Mhe. Rais hapa kwa kusimamia amani na utulivu katika nchi maana yake tunawapongeza Wakuu wa Mikoa kwa sababu wao ni sehemu ya maeneo tunayoishi sisi, bila ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kusimamia utulivu na amani katika maeneo yao Mhe. Rais huwezi ukampongeza juu ya suala hili. Hivyo tunampongeza Mhe. Rais lakini pia tunawapongeza na Wakuu wa Mikoa, kwa sababu Wakuu wa Mikoa ndio walioko chini, wanatembeza bendera za Serikali katika Mikoa yako, kwa hiyo wanafanya kazi vizuri na tuwapongeze Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, mimi tokea asubuhi nilikuwa nasikia malalamiko kwa baadhi ya Waheshimiwa wenzetu wanalalamika, wamezuiwa kufanya mikutano, hivi na hivi, amani itapotea, mimi nikajiuliza kwani kuna nini? Lakini Mhe. Mwenyekiti, kumbe liliopo kwamba mkutano wa hadhara uliotaka kuhutubiwa huko maeneo ya Kaskazini B umezuiliwa, lakini ukifuatilia kwa undani kwamba sasa hivi marekebisho haya ya daftari la wapiga kura liko katika Mkoa wa kaskazini, kwa hivyo huwezi katika kipindi kama hiki ukafanya vurumai za kisiasa katika Mkoa ule, mikutano yetu tunaijua, *movement* zake tunazijua, mkoa ule kesho unaanza daftari la wapiga kura halafu unapeleka wingu la watu katika maeneo yale, lazima tuwe wakweli na tukubali *situation* ilivyo, mikutano tumeshafanya sana katika maeneo mbali mbali, lakini kusubiri kipindi hiki cha uorodheshaji wa daftari jamani hilo ndio tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, juzi wenzetu wa *CUF* walitaka kufanya maandamano Dar es Salaam, kutoka kwenye ofisi yao nadhani kuelekea Ikulu, Serikali ikasema kwamba katika wakati kama huu tunapotea ugeni wa Rais Obama hatuwezi tukafanya maandamano na wamekubali wameridhia wakasema watafanya siku nyengine huo ndio Uungwana. Tusilazimishe kufanya mambo ambayo baadae yakaleta athari katika nchi yetu, na hawa Wakuu wa Mikoa na Wilaya ndio tuliowaweka katika maeneo yale kulinda amani na utulivu katika maeneo yao. Sasa kuruhusu mambo haya maana yake wanaruhusu jambo likijalikitokea hali mbaya basi itakuja kuwa athari katika nchi yetu, sasa mimi niwapongeze sana Wakuu wa Wilaya wa Kaskazini, Wakuu wa Mikoa kwa kuweza kudhibiti jambo hili na hili litakwisha tu, na mimi nimuombe sana mzee wangu Katibu Mkuu wa *CUF* maalim Seif Sharif Hamad atusaidie katika mambo kama haya.

Sisi tushakuwa watu wazima tena, mimi sasa hivi nina umri wa miaka 57 sasa hivi, nitegemee kwamba nitaipata tena miaka 57 huko tunapokwenda, si rahisi kuipata na maalim na yeye kwa umri alionao asitegemee tena kuupata umri kama ule, sasa hivi tujenge mazingira mazuri kwa vizazi vyetu na watoto wetu, nchi hii tusiichafue tena, sisi tumeshakwisha kabisa, sasa hivi sisi tusitoke misikitini tuende tuombe maghfira, tusiwashawishi watu tukasababisha watu walete fujo wakauana bure.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika eneo la Tume ya Utumishi ya Idara Maalum ya vikosi vya *SMZ*. Vikosi vyetu vimekuwa vikifanya kazi vizuri na kwa kweli wanastahiki pongezi na mimi nashkuru sana kwa sababu hatua hii tuliyo sasa na hatua ya nyuma tunakotoka basi ni tofauti.

Katika Baraza lililopita Mhe. Mansoor Yussuf Himidi shahidi, vilikuwa vikitajwa Vikosi vya SMZ kwa upande wa upinzani vilikuwa vinalaaniwa sana, vinaambiwa vifutwe havina maana. Leo tunamshukuru Mwenyezi Mungu Serikali ya Umoja wa Kitaifa imetuletea faraja *Alhamdulillah*, kwamba wale waliokuwa wakisema vikosi havina maana leo wamesimama kuvitetea maslahi yao, tunashukuru *Alhamdulillah*. Tunawaomba sana waendelee kwa sababu sasa inaonekana wamefahamu umuhimu wa vikosi hivi.

Vikosi hivi Mhe. Mwenyekiti, vina umuhimu mkubwa katika nchi yetu, ni alama ya dola katika nchi hii, tunahitaji tuviimarishe lakini pia tuvitumie vizuri. Lakini nataka kukubaliana wote wale waliosema kwamba maslahi yao ni madogo mno.

Mhe. Mwenyekiti, katika nchi yoyote ulimwenguni askari huwezi ukafananisha maslahi yao na mfanyakazi wa kawaida hata siku moja. Mimi mwenyewe nilikuwa mwanajeshi katika Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Nimetumikia Jeshi la Wananchi wa Tanzania na ninajua maslahi yaliyokuwepo jeshini na mpaka leo yanaingia. Sasa leo kama tunafika pahala tunalinganisha wanajeshi vikosi vyetu na raia kwamba mishahara hii maana yake iwe sawa kwa kweli hatuwafanyii vizuri. Askari wana kazi kubwa, kazi ya askari ni kazi nzito.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimestaafu jeshi mwaka 1986, lakini nilijua kama kazi ile ni nzito pale nilipopewa barua ya kuruhusiwa kustaafu niliona kama vile nimenyanyuliwa mzigo kwenye kichwa umewekwa chini, nilijihisi mwepesi. Pale ndio nikajua kwamba kazi hii ya ulinzi ni kazi nzito lakini wenyewe hawajijui. Unapopata ruhusa ya kustaafu sasa pale unajihisi wewe uko huru. Kwa hivyo, kama hatutowatengenezea maslahi yanayolingana na kazi yao kwa kweli tutakuwa tunawaonea. Mhe. Waziri hili tumelisema sana

na Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora yupo anasikia, watu hawa ni lazima walipwe maslahi yao yanayostahiki na kazi zao wala hili halina *objection* yoyote, vyenginevyo tutawaweka katika *position* ngumu.

Kuna Tume hii ya Utumishi ya Idara Maalum. Mimi muundo wake siujui haizidi tumepitisha sheria hapa lakini sijaihifadhi sana. Lakini hizi tume tunazoziunda au tunazozipitisha miundo yake tume nyingi zimekuwa zina matatizo, sijui hii Tume ya Utumishi ya Vikosi Maalum, sijui ikoje. Lakini kama tume hii imeweka raia wamekuwa raia sio wale Wakuu wa Vikosi wenyewe, basi tume hii inahitaji kufanyiwa marekebisho, ni lazima kwanza Tume hii ya Utumishi ya Idara Maalum Makamanda wote wa Vikosi wawemo katika Tume hiyo. Kwa sababu hawa ndio wenyewe wanaojua ujeshi nini, wanajua uaskari nini, wanajua nini dhana ya Mkuu wa Kikosi na wanajua renki zikoje. Sasa kama tume ile haina wenyewe Wakuu wa Vikosi basi matatizo haya yatakuwa hayaondoki, kwa sababu itakuwa inaendeshwa kiraia raia tu. Siku moja mimi niliwahi kusema Tume hizi tumeziweka kutokana na mazingira ya jambo lenyewe lilivyo ndio maana tumekuwa na tume chungunzima.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilipokuwa nikisoma kitabu hiki pana *statement* moja ilinishangaza sana, sijui kama ndivyo! Ukurasa wa 52, Tume ya Utumishi ya Idara Maalum inasema hivi: “Kwa mwaka 2013/2014 Tume ya Utumishi ya Idara Maalum inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo”: Kuna lengo hilo la nne linasema, “Kufuatilia ajira na maslahi ya watumishi wa Idara Maalum za SMZ kwa kushirikiana na Tume ya Utumishi Serikalini”. *This is wrong,* Tume ya Utumishi Serikalini ni sawa sawa na tume hii, sasa pale kinachotakiwa ni kuwa hizi zote ni tume tayari zina mamlaka sawa. Sasa haya malengo utatekelezaje kwa kushirikiana na Tume ya Utumishi Serikalini? Haiwezekani. Pengine wanakwenda wanachukua ushauri ule wa kiserikali, mishahara ya serikalini ni tofauti.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri kwa kweli jambo hili lazima lishughulikiwe, maslahi yaonekane uje utueleze hapa jinsi nyongeza hii iliyopo safari hii tumewasaidiaje, tumewaongezaje, hawa ni watu maalum. Kazi ya uaskari ni ngumu na nzito tusifananishe na watu wengine.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ametupa hapa kielelezo kimoja, naomba katika utekelezaji wa maagizo ya Wajumbe. Mimi nimeiona sehemu moja nina maeneo mengi, lakini nataka aje anipe maelezo katika sehemu ya 18 anasema, “Hoja kuondosha vikuta, vizuizi katika njia ya Forodhani na badala yake kuwe na utaratibu wa kupita gari zenye uzito mdogo”. Akasema utekelezaji kwamba, “Vikuta vya Forodhani vimeshaondoshwa na tayari kumewekwa alama za kuzuia kupita magari yanayozidi tani mbili eneo la

Vuga na magari zaidi ya tani mbili yatakayokamatwa yatatozwa faini ya shilingi elfu kumi". Vile vile ruhusa maalum inatolewa na Manispaa kwa magari yenye uzito wa zaidi ya tani mbili kwa kazi maalum.

Mhe. Mwenyekiti, agizo hili tulilitoa na Mhe. Waziri aliweza kutekeleza kwa siku mbili baadae likarejea. Vikuta kweli vimeondoshwa lakini kizuizi bado kipo. Magari yale hayapiti katika maeneo yale, gari inayotokea katika maeneo yale ya Posta kuja huku inabidi ipite pale, lakini inayotoka pale inabidi lazima izunguke. Tunataka Mhe. Waziri eneo lile kizuizi kile kifunguliwe kama ilivyokuwa zamani. Kwa sababu haiwezekani leo mtu kwenye gari yuko benki ya zamani pale anataka sasa kuondoka pale kuja maeneo ya Serana lazima azunguke apite Darajani haiwezekani wakati njia ile ipo.

Kwa hivyo, hili Mhe. Waziri atakapokuja hapa sasa aje atoe maelezo kwa sababu alituahidi kwamba njia sasa itapitwa anayetoka huku atapita huku, anayetokea hivi atazunguka hivi, lakini inaonekana vizuizi vimeondoshwa lakini ile alama ya kuzuia gari zisipite bado inaonekana ipo.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye Baraza la Manispaa. Taa za barabarani anasema katika malengo ya bajeti ya mwaka 2013 kuhusu kufunga taa za kisasa zinazotumia nguvu za jua. Mimi nawapongeza Baraza la Manispaa kwa kuweza kutekeleza hilo. Lakini tatizo sasa baadhi ya taa zimesha-*collapse* haziwaki, ingekuwa taa zile zinatumia labda ma-*bulb* ya kawaida pengine tungesema *bulb* zimeungua zinataka zibadilishwe. Lakini taa zile zinatumia mionzi ya jua, lakini inaonekana nyengine zinawaka nyengine haziwaki na zimefungwa juzi na inaonekana hazishughulikiwi. Sasa sijui mkataba wao na hawa walioweka ukoje. Kwa hivyo, naomba Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Manispaa lizishughulikie hazileti sura nzuri kwamba moja inawaka nyengine haiwaki na ndio kwanza taa zile zifungwe.

Lakini kibaya zaidi zile nguzo walizozing'oa bado ziko mle hakuna utaratibu wowote uliofanywa, hakuonekani kuwa na usafi. Kwa kweli suala lile linahitaji kuangaliwa ili angalau ule mji uwe mzuri.

Mimi nampongeza Mhe. Mkurugenzi mpya aliyeteuliwa juzi tuna imani atafanya kazi vizuri. Mkurugenzi wa Manispaa aliyechaguliwa keshaanza kazi zake vizuri na tuna matumaini kwamba atafanya kazi vizuri. Lakini ni hilo ambalo tunalitaka Mkurugenzi mpya afuate taratibu za kanuni za Baraza la Manispaa, ili aweze kwenda vizuri asije na yeye akaundiwa tume kama ilivyoundwa kwa Mkurugenzi aliyepita.

Mkurugenzi aliyepita alifanya taasisi ile kama ni mali yake, kila kitu anaamua mwenyewe hana kanuni, sheria wala taratibu. Kwa hivyo, tumuombe

Mkurugenzi mpya aliyeteuliwa afuate taratibu za kisheria zilizopo. Sheria Nam. 3 ya Mwaka 1995 inaongoza kila kitu na kama kanuni anaziona zimeshapitwa na wakati basi afanye marekebisho ili sasa afanye zile shughuli zake za kazi ziwe kwa mujibu wa kanuni.

Mwisho Mhe. Mwenyekiti, kwa kuheshimu muda wako namalizia kwenye suala la mradi. Mhe. Mwenyekiti, kuna Mradi huu wa *ZUSP*, mradi huu unasimamiwa na Baraza la Manispaa kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi, (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Lakini mradi huu ni wa muda mrefu na umetangazwa sana, hata Mhe. Rais amekuwa akiupigia debe sana kwenye vyombo vya habari, lakini kwa kweli tumekuwa na mashaka juu ya utekelezaji wake, na kwa sababu ni wa muda mrefu na Waswahili wamesema mtu anapokanyaga nyoka akikuta ukuti anarusha mguu, tumeshakanyaga sana kwenye miradi mingi. Sasa na huu tumeshakuwa na wasi wasi, kwa sababu mradi huu ni muhimu, ni mradi ambao fedha kutoka *World Bank* zinakwenda kwa wananchi moja kwa moja, haidhuru una *components* nyingi, lakini mbona mradi huu utekelezaji wake unasuasua?

Mimi Mhe. Mwenyekiti, nazungumzia zaidi eneo la ujenzi wa michirizi ya maji ya mvua, ambapo Mhe. Waziri hapa anasema, mshauri mwelekezi tayari ameshafungiana mkataba na Kampuni moja ya Israel katika ujenzi wa mitaro mbali mbali ikiwemo mitaro ile iliyoko katika Jimbo la Magomeni. Mimi nimekuwa nikijiuliza, ipo mitaro mingi tu kama vile Mpendae, lakini inaonekana kwamba bado suala hili ambalo linachukua pesa nyingi utekelezaji wake unaonekana bado. Kwa hivyo, nataka Mhe. Waziri aje atupe maelekezo hapa, ikiwezekana ili aniridhishe basi ile kodi ya mkataba waliyoingia na Wayahudi ambapo kwa mujibu wa taarifa za kitabu chake umetiwa saini mwezi uliopita, basi ili anitoe wasiwasi juu ya ujenzi wa mitaro ambayo humu ameitaja, ambapo mitaro ile kama kweli mradi huo utatekelezwa vizuri basi utakuwa ni mkombozi wa wananchi wa Zanzibar.

Kwa sababu maeneo mengi katika mji wetu yanatuama maji, mvua zikinyesha maji hayana pa kwenda, lakini mradi huu unaonekana unakwenda taratibu. Yale mambo madogo madogo kama ununuzi wa magari, ununuzi wa kitu gani yote yameshafanyika. Lakini lile eneo kubwa la msingi wa mradi ule inaonekana linashindwa kutekelezwa. Kwa hivyo, Mhe. Waziri akija aje atutoe wasiwasi na ningeomba kopi ya mkataba ambayo imetiwa saini ili nijiridhishe. Kwa sababu haya maneno maneno tumeshachoka sasa. Nijiridhishe kwamba kweli kuna hatua ya mkataba uliowekwa saini juu ya huyu mshauri mwelekezi katika masuala mazima haya ya uchimbaji mitaro katika mji wetu wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuheshimu muda wako mimi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na niwaombe wenzangu waipitishe pale ambapo Mhe. Waziri atatoa maelezo katika maeneo yale ambayo tumemtaka ufafanuzi. Eneo la kwanza la barabara ya Forodhani aondoshe vile vizuizi, atakapotwambia na alituahidi na eneo hili la Mradi wa *ZUSP* katika eneo la miradi. Ahsante sana.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa. Pili nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Vile vile naomba nimpongeze Mhe. Waziri kwa jinsi alivyowasilisha hotuba yake.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze na mchango wangu katika ukurasa wa saba (7) kifungu 18. Mhe. Waziri anazungumzia namna ya kumuingiza Sheha katika Mfumo wa Serikali za Mitaa. Mhe. Mwenyekiti, hapa naomba niseme mimi, Sheha ni kiongozi wa Serikali Kuu sio kiongozi wa Serikali za Mitaa na Diwani ndiye kiondozi wa Serikali za Mitaa. Sasa naomba Mhe. Waziri anifahamishe ni vipi anataka kufanya mbinu kumuingiza Sheha katika Serikali za Mitaa hivi si kusababisha kuwa na mivutano.

Mhe. Mwenyekiti, eneo jengine ambalo naomba niseme kidogo ni ukurasa wa 32 mpaka 34, Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho. Mhe. Mwenyekiti, hapa tunaambiwa pana manung'uniko mengi na malalamiko, lakini manung'uniko na malalamiko hayataondoka mpaka pale mtu atakapopewa haki yake na yule aliyekuwa hana haki atakaponyimwa haki ile.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nina masikitiko makubwa kuhusu mizengwe inayofanywa na ofisi hii, sijui ni kwa nini wananchi wasumbuliwe bure wakati kitambulisho ni haki yao. Mhe. Mwenyekiti, hapa nina mfano wa vijana ambao wametaka vitambulisho na wana vyeti vya kuzaliwa na barua ya Sheha lakini wamenyimwa. Miongoni mwa vijana hao mmoja wangu ni mtoto wangu mwenyewe wa kumzaa.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kutumia mfano wa mtoto wangu sababu ni jambo ambalo si la kuambiwa hata moja yote ni mambo ambayo yako ndani ya uwezo wangu. Namuomba Mhe. Waziri atakaposimama atwambie serikali ina lengo gani au dhamira gani ya kuwanyima wananchi wake vitambulisho.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nina mtoto wangu niliyemzaa mwezi wa kumi mwaka 1994 na alipata cheti cha kuzaliwa mwaka 1995 aidha Januari au Februari katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake. Mhe. Mwenyekiti, kipindi kilichopita mimi niko huku mtoto yule alichukua cheti za

kuzaliwa akapita kwa sheha akapata barua na alipofika Ofisi ya Vitambulisho aliambiwa cheti kile ni feki. Sasa kwa kuwa mimi nataka ule uhakika upatikane cheti kile nilikichukua nikaja nacho katika wizara inayohusika, nilifika katika ofisi inayohusika na utoaji wa vyeti nikataka uhalali wa cheti cha mwanangu na wakanambia cheti hakina tatizo.

Kwa sababu tu nataka uhakika nikawaambia hiki cheti kimechanika naomba nipatieni chengine, kilikuwa kimechanika kidogo na nikapewa cheti chengine. Na wakati nilipomrejeshea kijana yule akaenda nacho walikikataa na kile wakasema ni feki. Nilivichukua tena vyeti vile vyote viwili nikaja nikamkabidhi Waziri wa Katiba na Sheria ambaye wizara yake ndiyo inayohusika na utoaji wa vyeti vya kuzaliwa. Mhe. Mwenyekiti, baada ya yote Waziri alinirudishia vyeti hivyo na akanambia kuwa vyeti ni halali havina tatizo.

Sasa niliona kwa sababu yule ni mtoto niende mwenyewe katika ofisi ya vitambulisho, nilipofika Mhe. Mwenyekiti, la kusikitisha vyeti vile walivikataa vyote viwili na tuliondoka na wao mpaka kwa Mkuu wa Wilaya kutafuta uhalali wa cheti kile na kumbukumbu zilikuwepo. Lakini bado wakasimama kuwa vyeti vile si halali na wakasema saini wao wanazozijua za vyeti vya kuzaliwa ni mbili tu ambazo wamepewa kopi ya saini hizo kutoka Ofisi ya Mrajis na walinipa kopi hiyo ya saini. Wakanambia mtu mmoja anayetia saini vyetu vya kuzaliwa ni bwana anayeitwa Mohammed, mmoja anaitwa sijui Mgonjwa, sijui Mganja silijui vizuri, lakini naamini jina litaeleweka.

Mhe. Mwenyekiti, pale pale nilipiga simu kwa Waziri wa Katiba na Sheria nikamwambia mimi ninachotaka ni uhalali wa cheti cha mwanangu naomba unifahamishe niende wapi nipate cheti halali. Aliwapigia wale baadae walivyonijibu wakanambia Mheshimiwa sasa hivi vyeti vyako ni feki lakini mwanao tutampa huduma hii ya kupata Kitambulisho cha Mzanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilisema sikubali hiyo, kwa sababu kitambulisho ni haki ya msingi ya mtoto wangu na cheti cha kuzaliwa hatakitumia kwa kitambulisho tu, atakitumia na sehemu nyengine. Kwa hivyo, nataka uhalali wa cheti cha kuzaliwa. Sasa Mhe. Mwenyekiti, huu ni mfano mkubwa wa kuwa Ofisi ya Vitambulisho inawanyima Wazanzibari haki yao, na mimi walinipa kwa sababu ni Mwakilishi. Je, Mhe. Mwenyekiti, wale waliokuwa si Wawakilishi hawana haki ya kupata vitambulivyo hivi.

Pia Mhe. Mwenyekiti, katika ziara ya Mhe. Waziri aliyefuatana na Mkurugenzi wa Vitambulisho aliyetushirikisha Wabunge, Wawakilishi, Madiwani na Masheha. Mkurugenzi wa Vitambulisho alikuwa kila mara

akirejea kauli kwamba, mtu yeyote liyetimia umri wa miaka 18 na ikawa hana kitambulisho ni kosa na adhabu yake ni miezi sita jela au faini shilingi milioni moja.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atakaposimama anipe majibu mazuri hapa ili wananchi wasikie, serikali ina dhamira gani juu ya wananchi wake. Wakati wameshasema aliyekuwa hana kitambulisho ni jela miezi sita na faini shilingi milioni moja. Mheshimiwa mwananchi shilingi 2,000 ya mkate haipati aje apate faini ya shilingi milioni moja? Bila shaka hapa serikali inaonesha kwamba imeshachoka na hawa wananchi na ndio maana wanatayarisha jela na kuwaweka.

Mhe. Mwenyekiti, vyeti vya kuzaliwa vinatolewa na wizara ya serikali hii, vitambulisho vya Mzanzibari vinatokana na wizara ya serikali hii, sheria zote zinatungwa kutokana na serikali hii, leo serikali inajua kwamba mtu yeyote aliyekuwa ana umri wa miaka 18 na hana kitambulisho ni kosa na adhabu inajulikana kwa nini Mheshimiwa wananchi hawa wanyimwe haki yao hii. Hapa Mhe. Mwenyekiti, lazima Mhe. Waziri anijibu vizuri, la sikupata jawabu itakayoniridhisha mimi na wananchi basi sitounga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka niende mbele kwenye ukurasa wa 37 kifungu cha 106. Mhe. Waziri hapa anaeleza mafunzo aliyoyatoa kwa Waheshimiwa Madiwani. Mhe. Mwenyekiti, mimi nampongeza sana Mhe. Waziri kwa jambo hili, hili ni jambo zuri sana. Lakini Mhe. Mwenyekiti, jambo linalowasikitisha na kuwaumiza na kuwasononesha madiwani ni kule kukosa kulipwa mishahara. Suala hili linawasononesha sana Madiwani.Mimi naamini serikali ina uwezo wa kuwalipa madiwani lakini bado hawajafanya maamuzi tu. Mhe. Mwenyekiti, ushauri wangu kwa serikali mageuzi yoyote yatakayofanywa na Serikali za Mitaa ni lazima wazingatie mishahara ya madiwani, hatuwezi kuwa na viongozi wanaowatumikia wananchi lakini wasilipwe. Mhe. Mwenyekiti, hilo ni tatizo na tutawarudisha nyuma hawa na madiwani ni viongozi wanaosaidia sana kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, pia nataka niende katika ukurasa wa 11 kifungu cha 30 pale Mhe. Waziri alipozungumzia soko la Qatar Chake Chake. Mhe. Mwenyekiti, hapa mimi nadhani panahitajika uangalizi mzuri. Kwa sababu mji wa Chake Chake unakua kwa kasi sana na kila mtu nafikiri anauona, leo Mhe. Mwenyekiti, soko liliopo pale lililopakana na bahari Mhe. Waziri si soko la kujisifia hili kwamba kafungua soko, kile ni kijisoko tu kwa mji unavyokua.

Namuomba Mhe. Waziri aniambie ile kauli ya ujenzi wa Stendi ya Magari ya Abiria eneo la Michakaeni imefikia wapi? Nadhani ni vyema wizara yake ikafufua ile dhana ya ujenzi wa stendi ya magari na soko kuu kwa pamoja. Mhe. Mwenyekiti, kisoko cha Chake Chake na mji unavyokua haliitwi soko lile kile kinaitwa kisoko.

Katika ukurasa wa 113 kiambatanisho nambari 15 kinaelezea miradi iliyosaidiwa na Mkoa wa Kusini Pemba. Mhe. Mwenyekiti, nazipongeza sana juhudi za Serikali ya Mkoa wa Kusini Pemba katika kusaidia miradi. Hapa Mhe. Mwenyekit, nina maswali kidogo ambayo naomba Mhe. Waziri aje anijibu. Fedha zilitumika kusaidia miradi hii ni shilingi ngapi? Na ilitoka katika fungu lipi la Mkoa wa Kusini Pemba? Mhe. Mwenyekiti, hapo nataka majibu na vile vile kwa nini miradi yote ikawa ni ya skuli tu, hivi wananchi hawana miradi mingine? Namuomba Mhe. Waziri na hilo anifahamishe.

Halafu pia suala jengine ambalo namuomba Mhe. Waziri anifahamishe ni mbali ya Mkoa wangu wa Kusini Pemba hakuna mikoa mingine yenye miradi ya kusaidia wananchi. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, mimi sikuiona.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, niende katika ukurasa wa 59 kifungu 183, pale Mhe. Waziri aliposema kuhusu jitihada zinazoendelea za kujenga vituo vipya vya Zimamoto kwa kila wilaya. Mhe. Mwenyekiti, mimi napongeza sana jitihada hizi, kwa sababu hivi vituo vikiwemo kila maeneo pale patapotokea tatizo itakuwa ni rahisi kulikabili tatizo hilo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, si kuwa tuongeze vituo tu na vile vilivyopo viboreshwe. Mhe. Mwenyekiti, mimi nina masikitiko makubwa katika kituo cha Zimamoto kilichoko Uwanja wa Ndege Pemba hee! Mhe. Mwenyekiti, ni aibu hata kusema, katika ziara ya kamati tulipotembelea sehemu wanazolala askari wale vitanda vimewekewa majiti na magodoro mimi siyaiti magorodo wala sponji sijui niite kigodoro, kwa sababu hata mtoto wa mwaka mmoja na nusu ukimtwika kidude kile atakwenda nacho kwa masaa wala hachoki. Hivyo kweli Mhe. Mwenyekiti, wale tunakusudia tutapokutwa na tatizo watuokoe wakati wao hatujawaokoa? Hawawezi kulala katika mazingira yale pakitokea tatizo wakaweza kunyanyuka wakatusaidia. Mhe. Mwenyekiti, kila mmoja anajua umuhimu wa kulala, ukilala pahali ikiwa haparidhishi huwezi ukaamka ukafanya kazi yoyote kwa maumivu na kuchoka.

Kwa kumalizia Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na namuomba Mhe. Waziri maswali yangu yote niliyomuuliza anijibu, hasa lile la kunyimwa haki Wazanzibari waliokuwa wana haki. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru na mimi kunipa fursa hii ya kuweza kuzungumza machache katika hotuba ya Waziri wa Ndchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Lakini pia nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia na mimi uhai wake na uzima nikaweza kusimama hapa ili kutoa mchango wangu mdogo sana. Mhe. Mwenyekiti nitakuwa mchache wa fadhila kama sikumshukuru Mhe. Waziri yeye na watendaji wake wote na vikosi vyake, kwa kutuletea kitabu chao hiki au vitabu vinne kwa mpigo ambavyo vinaeleza malengo na madhumuni mbali mbali ya wizara yao kwa lengo la kupata ufanisi wa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mengi yamezungumzwa lakini wakati yanatugusa kwa namna moja au nyengine tutayazungumzia kwa kiasi fulani kwa vile yanavyotugusa au yanavyotuumiza.
Mhe. Mwenyekiti, mimi nikianza kwanza, nianze kitabu hichi cha Mhe. Waziri alichotusomea ukurasa wake wa 5 sehemu ya 12 amesema: Kutokana na Programu nilizozitaja hapo juu, Ofisi yangu inaazimia kuteleza malengo makuu matano ambayo ni:-

(1) Kuimarisha Ulinzi na Usalama.
(2) Kuwafanya vijana wawe na maadili mema na mtizamo wa kujiajiri wenyewe.
(3) Kuimarisha Utawala Bora na Haki za Binaadamu. Huko kwengine sifiki kwa ajili ya muda.

Mhe. Mwenyekiti, ni malengo mazuri sana ukiyaangalia, kwanza hili la kuimairisha ulinzi na Usalama. Sasa akisema kwa kuwa ana lengo la kuimarisha Ulinzi na Usalama tunategemea kuwa ni wananchi wote wa Zanzibar na mali zao. Lakini japokuwa limeshazungumzwa Mhe. Mwenyekiti, suala hili kwa kusema kweli kwa kupitia vijana wetu walioko Darajani kwa kupigwa na kunyang'anywa mali zao hili ni suala ambalo halikutufurahisha hata kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, mtu anapofanya kosa basi anahitajika akamatwe na kupelekwa Mahakamani. Sasa kama leo Serikali wanashindwa wananchi hawa kuwachukulia sheria na kuwapeleka mahakamani wanaanza kuwapiga wao. Je, na wananchi na wao hawatachukua sheria mikononi mwao?
Mhe. Mwenyekiti, hili ni tatizo na tunamuomba Mhe. Waziri kama wanaokwenda pale wakipiga watu wanawatambua basi hili si suala zuri hata kidogo kwa sababu wale ni watu na wanatafuta rizki kwa ajili ya kujikumu na maisha yao. Sasa kama wana kosa basi vyombo vya sheria vichukue mkondo wake lakini sio kuchukua hatua mikononi mwao. Jambo la kushanganza basi

wanapokwenda pale kufanya vitendo hivyo wanatijia ninja ndani ya nyuso zao. Kwa nini basi kama wao wanakwenda pale kisheria kwa agizo la Serikali kwa nini sasa wanajifunika nyuso zao?

Sasa wangelikwenda hivi hivi ili watu na wao wakawaona wakajua kuwa fulani na fulani ndiye aliyekuja hapa. Lakini leo haiwezekani mtu pengine katumwa au ni kiongozi gani akaenda pale akajifunika uso hili ni tatizo Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo tunasema kwamba haki za binaadamu hazionekani wala hazipo.

Jengine pia kuwafanya hao vijana kuwa na maadili mema. Mhe. Mohammed amekwishayazungumza kuwa maadili haya hayapo kwa sababu tumeshindwa kusimamia watoto wetu na vijana wetu na tunawaachia wafanye watakavyo na haya ndio yanayosababisha mambo mengine kuongozeka kama masuala ya Ukimwi kwa kukosa yale maadili yetu tulionayo.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika Halmashauri za Wilaya. Kwanza Mhe. Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii kuipongeza sana wilaya yangu ya Micheweni kwa mchango wao mkubwa wa fedha walizokusanya katika kipindi cha 2012/2013 milioni sitini na tano. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuwapongeza ili waweze kuchukua juhudi kubwa zaidi katika kutelekeza maagizo haya ya Serikali.

Lakini pia nataka kuchukua nafasi hii Mhe. Mwenyekiti, kumpongeza sana Mhe. Waziri moja kati ya jambo alilolifanya kushughulikia ule mzozo uliokuweko kwenye Halmashauri na watendaji wale wakapata suluhisho zuri kabisa ili kuondokana na migogoro hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye kitabu cha pili ukurasa wa 85 Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni. Mwaka jana shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika Halmashauri ya Micheweni ilikuwa moja ni ujenzi wa ukumbi wa Mikutano. Lakini ujenzi huo haukufanikiwa kwa kipindi hicho. Sasa kilichotekelezwa ni upimaji wa kiwanja na mchoro wa ramani umefanyika.

Mhe. Waziri hapa nakumbuka bajeti ya mwaka jana ulitueleza kuwa kuna shilingi milioni 13 ambazo zilitengwa kwa kushughulikia ujenzi wa ukumbi huu wa mkutano. Lakini la kushangaza ujenzi huu haujaanza na upimaji tu wa kiwanja na uchoraji ramani. Kweli pesa hizi milioni 13 zote zilifanyika kwa upimaji wa kiwanja. Kwa hiyo, Mhe. Waziri ukija unieleze hizi pesa shilingi milioni 13 zilitumika kwa njia gani.
Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ukurasa wa 49 Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Mjumbe umebakisha dakika 5 kumalizia.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mkoa wa Kaskazini Pemba, kuimarisha Ulinzi na Usalama Raia na Mali zao. Mhe. Mwenyekiti, hili usalama wa Mkoa wa Kaskazini Pemba naona kila kukicha unatoweka kidogo kidogo. Kwa hiyo, ili hili kutekelezwa tungemuomba sana Mhe. Waziri ili kufanikisha suala hili basi ashirikiane na vikosi vya Polisi Jamii ili waweze kufanya shughuli angalau za vijijini. Mkoa wa Kaskazini Pemba hasa Wilaya ya Micheweni umekuwa unapata matokeo makubwa ya kusikitisha kitu ambacho hatukuweza kutarajia kutokea kwa matokeo yale.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 55 Jeshi la Kujenga Uchumi JKU. Kwanza nilipongeze jeshi hili kwa kuweza kuanzisha Skuli ya Ufundi na Sekondari katika Jeshi hilo la Kujenga Uchumi JKU. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, hapa ameeleza Mhe. Waziri kuwa Jeshi la Uchumi linaendelea na kushirikiana na mradi wa ufugaji wa kuku, ng'ombe wa maziwa kwa kununua vifaranga elfu mbili, elfu moja vikiwa vya nyama na elfu moja vya mayai.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tulitaka kikosi hichi kiwe ni darasa la Wazanzibari watakapofanya wao vizuri basi baada ya kuchukua vikundi vyengine vya Ushirika wakaenda wakasoma Bara Jeshi hili liweze kutengeneza mazingira mazuri ili baadae vikundi vyetu vya Ushirika waende wakasome katika kikundi hichi.

Mhe. Mwenyekiti, nina suala langu moja maana naona haya hayamalizi. Lakini namuomba Mhe. Waziri na hili suala lilizungumzwa sana kwa JKU na KMKM. Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu hichi cha kwanza kikubwa kuna fungu 211101 mishahara hiyo, bilioni tatu milioni mia tisa na ishirini. Halafu posho maalum kuna bilioni mbili milioni tatu na kumi na tatu na pesa za juu. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, kuna na fungu jengine hili ni Jeshi la Kujenga Uchumi.

Lakini kuna kifungu chengine cha KMKM mishahara kuna shilingi bilioni nne mia nane na ishirini na tatu. Lakini posho maalum kuna shilingi bilioni mbili milioni mia moja na kumi na saba. Mhe. Waziri nataka aje anifahamishe hapa. Je, mbona vifungu vya maposho maalum viko juu sasa ni daraja gani wanaopatiwa posho hili maalum?

Lakini jengine hoja yangu ya pili ni kuwa hakuna uwiano wa mishahara na posho maalum. Kwa hiyo, Mhe. Waziri atakapokuja hapa aje anieleze.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Mjumbe umebakisha dakika moja.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ni sababu gani wa kuwa kuna fungu la mishahara ambalo kuwa na posho maalum karibuni liko nusu na robo. Sasa

atufahamishe hawa wanaopata posho maalum ni wapi na hawa wanaopata mishahara ni wapi? Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti siungi mkono hoja kama sijapata maelezo ya kutosha. (*Makofi*).

TAARIFA

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe labda tu niseme kwamba kwa bahati mbaya sio wote ambao wamepata fursa ya kuchangia kwa sababu wachangiaji wamekuwa wengi sana na mara nyingi kila mmoja akipata nafasi anaitumia vilivyo. Kwa hiyo, mimi ningewaomba tu baadhi ya wachangiaji kwa sababu Jumatatu tunatarajia kumaliza hoja ya Wizara hii. Kwa hiyo baadhi itabidi watapeleka kwa maandishi. Sasa ningewaomba wengine ambao watakuwa wanaona watayarishe maandishi yao ili wamfikishie Mhe. Waziri.

Waheshimiwa kabla ya kuakhirisha nina matangazo mawili muhimu sana. Tangazo la kwanza wale Wajumbe wote ambao wamearifiwa semina kesho Marumbi usafiri utakuwepo hapo nje baada tu ya kumaliza shughuli yetu ya leo. Kwa hiyo, wanaombwa sana wafike hapo nje.

Tangazo jengine wanaombwa Waheshimiwa Wajumbe kuwa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa inawatangazia Waheshimiwa wote na watendaji wa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi ambao hawajapa vitambulisho vyao vya *NIDA* wafike katika Ofisi ya mamlaka hiyo jengo la Uhamiaji la zamani Kilimani kuanzia Jumatatu ya tarehe 1/7/2013 hadi Ijumaa ya tarehe 5/7/2013 saa mbili asubuhi hadi saa nane mchana.

Orodha ya Waheshimiwa na watendaji ambao hawajachukua vitambulisho hivyo inapatikana katika ubao wetu wa matangazo hapo nje. Vile vile Waheshimiwa Wajumbe tunakumbushwa kwamba ile semina yetu inayohusu mzozo na namna ya kuitatua itafanyika kama ilivyopangwa siku ya Jumatatu ya tarehe 1/7/2013 wakati wa saa saba mchana katika ukumbi wetu wa mikutano. Nimemaliza matangazo.

Waheshimiwa Wajumbe nawashukuru sana kwa utulivu pamoja na michango yenu mizuri tunatarajia tena kurudi hapa tukijaaliwa Jumatatu saa 3:00 asubuhi naakhirisha kikao.

(Saa 1.45 usiku Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 01/07/2013 saa 3:00 asubuhi)